

**BUNGE LA TANZANIA**

-----  
**MAJADILIANO YA BUNGE**

-----  
**MKUTANO WA KUMI NA SABA**

**Kikao cha Tano - Tarehe 11 Novemba, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Saba na leo ni kikao cha tano. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mary Pius Chatanda Mbunge wa Korongwe Mjini.

Na. 56

**Ukarabati wa Shule Korogwe**

**MHE. MARY P. CHATANDA** aliuliza:-

Serikali imefanya kazikubwa sana ya ukarabati wa Shule ya Sekondari Korogwe lakini haikuunganisha nyumba za Walimu zilizopo Shuleni hapo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati nyumba hizo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jafo tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari Korogwe ni miongoni mwa shule 45 zilizokarabatiwa katika awamu ya kwanza ya ukarabati wa shule kongwe nchini. Ukarabati wa shule kongwe awamu ya kwanza ulihusisha vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, mabweni, maabara, ofisi za walimu, majengo ya utawala, mabwalo ya chakula na majiko, mifumo ya maji safi na taka na mifumo ya umeme.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa shule kongwe awamu ya kwanza haukuhusisha nyumba za walimu kutokana na sababu za kibajeti. Awamu ya pili ya ukarabati unaoendelea inahusisha shule shule kongwe 19 ikiusisha halikadhalika nyumba za walimu kwenye shule zinazokarabatiwa. Serikali inatafuta fedha ili kukarabati nyumba za walimu ambazo hazikujumuishwa kwenye mpango wa ukarabati wa shule kongwe awamu ya kwanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mary Chatanda, swali la nyongeza.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuishukuru Serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikitukimbilia pale shule yetu imekuwa na majanga ya moto zaidi ya mara mbili. Tunaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili nishukuru kwa majibu mazuri niliyopewa na Waziri.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, katika huu mpango wa pili ambapo watakuwa wametafuta fedha, je, Shule ya Korongwe Girls itapewa kipaumbele cha kwanza hasa ikizingatiwa kwamba pia ina watoto wenye ulemavu ili walimu wale wawe na moyo wa kuendelea kufanya kazi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa tunazo shule za kata katika Halmashauri zetu kwa nchi nzima ambapo tulikuwa tumeweka mipango kwa ajili ya ujenzi wa maabara lakini kwa bahati mbaya sana Halmashauri nyingine zimeshindwa kukamilisha mahabara hizo. Je, mtakuwa tayari sasa kuweka mpango wa kukamilisha zile maabara zilizoko kwenye Halmshauri zetu ili watoto waweze kupata elimu iliyo bora kuliko bora elimu?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la mama yangu Mheshimiwa Mary Chatanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mary Chatanda maana kwa vipindi tofauti tumefanya ziara jimboni kwake Korogwe na awamu ya mwisho tulienda naye katika shule yetu ya Sekondari Korongwe na kuongea na wanafunzi na kubainisha changamoto mbalimbali. Nafahamu kwamba juzijuzi hapa shule ilipata madhara ya bweni kuungua na ndiyo maana nimetuma wataalamu ili bweni lile tulikarabati haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, katika programu hii ya kukarabati, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Chatanda tutakapoanza awamu hii shule ya Korongwe tutaiweka katika awamu ya kwanza bila kigugumizi chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika mpango wa kuhakikisha tunamalizia maabara, kama mnavyokumbuka kwamba hapa katikati tulitoa zaidi ya shilingi bilioni 32.5 kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunamalizia maboma mbalimbali. Tunajua fika fedha hii haitoshi kwani kuna mabweni mengine hayajakamilika.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali hata katika mpango wa bajeti ya mwaka 2019/2020 tutahakikisha katika maeneo mbalimbali tunakamilisha ujenzi wa maabara na vifaa. Juzijuzi tumetumia zaidi ya shilingi bilioni 17 ili tupate vifaa vya maabara vijana waweze kufanya *practically* katika maeneo ya shule.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, litaulizwa na Mbunge wa Mbulu Mjini Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay.

Na. 57

### **Hitaji la Vituo vya Afya Tarafa ya Nambis – Mbulu**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Sera ya Afya ni kuwa na Kituo cha Afya kwa kila Kata na Zahanati kwa kila Kijiji; Tarafa ya Nambis katika Jimbo la Mbulu Mjini haina Kituo cha Afya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya kwenye Kata za Kainem, Murray, Nambis na Nahasey?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tupo TAMISEMI, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Jafo, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Tarafa ya Nambis haina Kituo cha Afya na wananchi wa Tarafa hiyo wanapata huduma kwenye Zahanati 4 za Serikali zilizoko katika Tarafa ya Nambis pamoja na Hospitali ya Wilaya ya Mbulu ambayo iko jirani na Kata ya Nambis.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma za afya katika Mji wa Mbulu, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 3 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya Daudi na Tlawi sambamba na vifaa tiba ambapo hadi Oktoba, 2019 Kituo cha Afya Daudi kimepokea vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 203.8 na Kituo cha Afya Tlawi kimepokea vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi 203.8.

Vilevile Mkoa wa Manyara umepatiwa kiasi cha shilingi billioni 3 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Halmashauri za Wilaya za Mbulu na Simanjiro. Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mbulu utapunguza msongamano katika Hospitali ya Wilaya ya Mbulu iliyoko Mbulu Mjini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati Vituo vya Afya nchini kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha uliopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issaay nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali kupitia Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa hospitali ya Mji wa Mbulu inategemewa na kata zinazopakana kutoka Wilaya ya Babati, Karatu na hata upande wa Jimbo la Mbulu Vijijini; na kwa kuwa hospitali hii inakabiliwa na upungufu mkubwa wa fedha za uendeshaji hali inayopelekea wagonjwa kujigharamikia wakati wa rufaa na ukosefu mkubwa sana wa dawa. Mheshimiwa Waziri ameshafika mara kadhaa na sasa hivi tuko kwenye mpango wa bajeti wa 2020/2021. Je, Serikali ina mkakati

gani wa kusaidia hospitali ya Mji wa Mbulu kwa kuiongezea fedha za uendeshaji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Vituo vya Afya ya Daudi na Tlawi tayari vimeanza kutoa huduma, tunaishukuru sana Serikali. Pia nia ya Serikali ni njema kujenga Kituo cha Afya katika Tarafa ya Nambis ambapo vijiji vyake baadhi vina umbali wa kilomita 30 mpaka 40 kwenda hospitali wa Mji wa Mbulu. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka maombi niliyowasilisha ya gari la *ambulance* kutafutwa haraka ili wananchi wa kata hizo za Nambis na maeneo mengine ya pembezoni wapate huduma ya usafiri haraka kwenda kupata matibabu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la kaka yangu Mheshimiwa Zacharia Paul Issay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na pacha wake Mheshimiwa Flatei Massay hapa karibuni tulienda kufanya ziara katika Halmashauri hizi mbili na niwapongeze Wabunge hawa wamefanya kazi kubwa sana ya kusimamia miundombinu kwa fedha ambazo tumepeleka kule.

Mheshimiwa Spika, ni kweli hospitali ya Mheshimiwa Mbunge siyo suala la mgao wa fedha peke yake hata hali ya majengo haipendezi. Ndiyo maana kwa ombi la Mheshimiwa Mbunge nilipendekeza na nilielekeza kwamba zile shilingi milioni 500 sasa zianze kuibadilisha Hospitali ya Mbulu kwa sababu tunajua itakapokuwa na mazingira mazuri hata suala zima la ukusanyaji wa mapato litaongezeka. Hata hivyo, ni azma ya Serikali Mheshimiwa Mbunge wala usihofu tutaangalia nini kifanyike kuhakikisha mgao wa dawa katika eneo lile ambapo tunajua fedha nyingi sana zinaenda vijijini kuwasaidia Halmashauri ya

Mbulu Mjini kuweza kuongeza ule mfuko wao wa dawa ili waweze kupata huduma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ajenda ya upatikanaji wa *ambulance*, naomba nimhakikishie tutashirikiana na dada yangu Mheshimiwa Ummu Mwalimu, Waziri wa Afya pale tutakapopata gari aina yoyote tutawapelekea. Kwa kweli nimefika kule na nimeona changamoto kubwa katika eneo hilo lazima tupate usafiri.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Shangazi, swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, tarafa ya Mtae katika Halmashauri ya Lushoto ambayo ina kata tano ndiyo pekee mpaka sasa hivi haijapata kituo cha afya. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga kituo cha afya katika Tarafa ya Mtae.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la ndugu yangu Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili amelileta kwa muda na alikuwa na changamoto pale Mnazi na Mtae na ndiyo maana tukaona tuanze katika eneo lingine lakini hii eneo la Mtae lipo katika mpango kazi wetu. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ajenda yetu ipo palepale katika mgao wa fedha tutakaoupata tutahakikisha suala la Mtae linapata kituo cha afya. Kwa hiyo, wala asiwe na hofu, ni jukumu letu kutatua changamoto kwenye maeneo mbalimbali. Kwa hiyo,

Mheshimiwa Shangazi wala asihofu suala hilo liko katika mpango wetu wa kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, Tarafa yako ya Mtae ina kata tano haina kituo cha afya Kongwa nina Tarafa ya Zoisa (Mkoka) ina kata kumi haina kituo cha afya. Kwa hiyo, itabidi tuanze kwetu kwanza kabla yako lakini unastahili pia. (*Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge Viti Maalum.

Na. 58

### **Upungufu wa Walimu – Bukoba**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Kuna upungufu mkubwa wa Walimu katika Shule za Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba:-

Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kutosha katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba.

**SPIKA:** Bado tupo TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri usichoke leo una maswali manne.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la mama yangu Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba ina jumla ya shule za msingi za Serikali 141 zenye jumla ya wanafunzi 80,224. Halmashauri ina walimu 1,172 wa shule za msingi kati ya walimu 1,783 wanaohitajika hivyo kuwa na upungufu wa walimu 611.



Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutatua changamoto ya upungufu wa walimu nchini kuanzia Mei, 2017 hadi Oktoba 2019, Serikali imeajiri walimu 15,480 wa shule za msingi, walimu 7,218 wa shule za sekondari na fundi sanifu wa maabara 297 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba imepatiwa walimu 66 wa shule za msingi yaani 37 ajira mpya na 29 walihamishiwa kutoka sekondari kwenda shule za msingi. Serikali itaendelea kuajiri walimu wa shule za msingi na sekondari kwa kadri fedha na vibali vitakavyopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rwamlaza, nimekuona.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba sasa niulize maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, katika Mkoa wa Kagera, Halmashauri ya Bukoba na hasa Jimbo la Bukoba Vijijini ni mahali ambapo hawafanyi vizuri kielimu katika matokeo na hasa darasa la saba lakini pamoja mambo mengine ni ukosefu wa walimu na ni tatizo la muda mrefu. Kutokana na jibu la msingi bado kuna mahitaji ya walimu zaidi ya 500. Je, Serikali inalichukuliaje jambo hili na kuhakikisha walimu wanapatikana ili Bukoba Vijijini na yenyewe iweze kwenda mbele kielimu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, yapo maeneo mengine katika Halmashauri mbalimbali za Tanzania ambapo yako mbali kabisa yaani tuseme ni *remote areas* ambapo walimu wakipelekwa hawaendi. Je, Serikali ina mpango gani kufanya uwiano kwa kuhakikisha walimu wanaenda katika maeneo hayo ili Watanzania wote waweze kufaidika na mfumo wa elimu uliopo katika nchi?

**SPIKA:** Wakati Mheshimiwa Rwamlaza amesimama ndiyo nikaona kuna watu wamechagua kitambaa kibaya kabisa wala hakipendezi hata kidogo. Wabunge wangu mnapaswa kuvaa *smart* bwana mnavaa vitambaa gani hivyo. (*Kicheko*)

Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la mama yangu Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema ni kwamba tutaendelea kufanya kila liwezekanalo na hasa katika mpango wa kuajiri walimu. Naomba nimhakikishie kwamba tutaweka kipaumbele katika Mkoa wetu wa Kagera tukijua kwamba mkoa huu ni miongoni mwa mikoa ya pembezoni na tunajua kwamba lazima tufanye juhudi ya kutosha. Kwa hiyo, katika mipango ya baadaye suala la walimu katika Halmashauri ya Bukoba tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la nini Serikali inafanya kuhakikisha usambazaji wa walimu unafanyika, kutokana na changamoto hiyo, tulichokifanya kupitia mpango wa *PforR* tumehakikisha tunafanya msawazo wa walimu. Tulipeleka fedha katika maeneo mbalimbali kuhakikisha walimu wanatawanya na tuliwaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri wahakikishe wale walimu waliojazana mijini wanahamishwa kwenda maeneo ya pembezoni kwa kupewa posho maalumu za kuwahamisha walimu ili hata watu wa pembezoni wafaidike na programu hii ya elimu bila malipo ambapo ni jambo jema kwa ajili ya vijana wetu. Kwa hiyo, suala hili tunalifanyia kazi kwa nguvu zote Mheshimiwa.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Mwalimu Salma Kikwete, uliza swali tafadhali.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwanza naomba nitoe pongezi zangu na niwatakie kheri wanafunzi wote wa kidato cha pili kote nchini kwa kuanza mitihani yao ya taifa leo hii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nataka nijikite kwenye swali la msingi. Kwenye Halmsahauri ya Lindi

Vijijini sasa hivi ni Halmshauri ya Lindi Mjini kwenye Jimbo la Mchinga, Kata ya Mpingo kuna shule shikizi. Bahati nzuri hiyo shule shikizi wananchi wamejitahidi, wamejenga na kule kuna wafugaji huenda mwakani ikaanza. Tatizo letu ni vifaa vya vitakavyotumika kwa ajili ya wanafunzi wale kujifunza na kujifunzia.

Je, Serikali itatusaidiaje kwenye tatizo hili kwa ajili ya wale wafugaji waliopo kule? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu ya swali hilo maalumu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la mama yangu Mheshimiwa Salma Kikwete ambapo namuita kama Balozi wa Elimu katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu Mheshimiwa mama Salma amechukua muda wake mwingi sana ku-*invest* kusaidia watoto wa Kitanzania wapate elimu. Kwa hiyo, mama tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, eneo hili ambalo amelizungumzia ni eneo la wafugaji, ni shule shikizi, kwa heshima ya mama yetu, naomba nimuagize Mkurugenzi wangu wa Elimu amuagize Afisa Elimu Mkoa atembelee haraka Shule hiyo Mpingo kwenda kufanya *needs assessment* kuona kuna jambo gani la haraka linatakiwa kurekebishwa mapema ili itakapofika Januari watoto waweze kupata matunda mazuri ya swali hili.

Kwa hiyo, namuagiza Mkurugenzi wangu aweze kufanya kazi hiyo haraka iwezekanavyo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwamoto uliza swali lako tafadhali.

Na.59

**Sifa ya kuwa Halmashauri**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO** aliuliza:-

(a) Je, ni nini sifa au vigezo vya kupata Halmashauri?

(b) Inachukua miaka mingapi kuendelea kuitwa Halmashauri ya Mji Mdogo hadi kuwa Halmashauri kamili?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la wana Kilolo, tafadhali Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la kaka yangu Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, Mkoani Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287 na (Mamlaka za Miji) na Sheria ya Serikali za Mitaa Sura 288 zimeweka utaratibu wakuzingatiwa katika kupandisha hadhi maeneo ya utawala. Vigezo vya kuanzisha Mamlaka za Miji Midogo vimeainishwa kwenye Mwongozo wa Uanzishaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2014, Kipengele Na.4.2.5 (a-q) na miongoni mwa vigezo muhimu ni pamoja eneo linalopendekezwa kuwa na idadi ya watu isiopungua 50,000, kata zisizopungua 3, vitongoji visivyopungua 30 na ukubwa usiopungua kilometa za mraba 150.

Mheshimiwa Spika, vigezo vya kuanzisha Halmashauri ya Wilaya au kuipandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo kuwa Halmashauri ya Wilaya vimeainishwa kwenye Kipengele Na. 4.2.4 (a-q) kama nilivyosema awali na miongoni mwa vigezo muhimu ni pamoja na uwezo wa kujitegemea kibajeti kwa walau 20% kutokana na mapato ya ndani, eneo lenye ukubwa usiopungua kilometa za

mraba 5,000, kata zisizopungua 20, vijiji visivyopungua 75 na idadi ya watu wasiopungua 250,000. Hivyo, upandishaji wa hadhi wa Mamlaka za Mji Mdogo kuwa Halmashauri unategemea vigezo vilivyoainishwa na sio muda wa Halmashauri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwamoto, swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, sasa naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Jimbo la Kilolo na Wilaya ya Kilolo ni kubwa sana na Mheshimiwa Waziri anajua; na kwa kuwa Halmashauri ya Mji Mdogo wa Kilolo ambayo ni Ilula ilianzishwa muda mrefu, zaidi ya miaka mitano, kwa kigezo kwamba ili kupunguza ukubwa wa wilaya na jimbo ili kuwafikia wananchi. Je, sasa haoni ni wakati muafaka sasa wa kupa hadhi ya kuwa halmashauri kamili kwa sababu vigezo vyote vilivyotajwa hapa vimekamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Wilaya ya Kilolo ina ukubwa na sifa zote zinazokubalika; na kwa kuwa vikao vingi vimeshakaliwa, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufika Wilaya ya Kilolo na kujionea mwenyewe jinsi mambo yalivyo tayari kwa kugawa kutupa halmashauri kamili?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya kaka yangu, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la Mji wa Ilula nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, ziara yetu ya kwanza ambayo nilifanya mimi na yeye ambayo *impact* yake ndiyo maana Kilolo leo hii imepatikana hospitali ya wilaya ya kisasa. Licha ya ziara ile, jambo lingine kubwa tulitembelea eneo la Ilula

na maeneo mbalimbali na ni kweli; Halmashauri ya Kilolo ni kubwa sana maana inapatikana mpaka huku na Kibakwe, ukiangalia jiografia yake ni kubwa sana. Kwa hadhi ya eneo lile, hasa Ilula, inapaswa kuwa halmashauri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, maelekezo ya Serikali ya hivi sasa kwamba *status quo* inabakia kwamba mpaka pale Serikali ijipange kwa sababu maeneo yote sasa hivi yamesimamishwa kupandishwa hadhi, lakini japo kuwa hadhi inastahili lakini kwanza kipindi cha sasa itasubiri kwanza mpaka hizi halmashauri ambazo zimeshapandishwa tuweze kuziwekea *infrastructure* za kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jambo hilo naomba nimwambie kwamba lipo katika *pending issue* pale ambapo sasa tukipewa *go ahead* na utaratibu utakapokwenda vizuri tutalifanyia kazi wala Mheshimiwa Venance Mwamoto asihofu.

Mheshimiwa Spika, ajenda ya ukubwa wa halmashauri yake kama nilivyosema awali mimi na yeye tumeshatembea sana mpaka katika yale madaraja yaliyokuwa hayapitiki. Nimhakikishie kwamba tumefanya kazi kubwa, Mheshimiwa Venance Mwamoto asihofu, pale muda utakaporuhusu jambo hilo Serikali italiangalia kwa jicho la karibu sana.

**SPIKA:** Ahsante. Tukubaliane tutoke sasa TAMISEMI twende Wizara ya Fedha na Mipango, swali litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega.

Na. 60

### **Dhana ya Kukua kwa Uchumi**

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Je ni nini maana ya dhana ya uchumi kukua ukioanisha na maisha ya wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya uchumi kukua ikioanishwa na maisha ya wananchi inaweza kutafsiriwa katika dhana kuu mbili. Dhana ya kwanza ni kwa kuangalia upatikanaji, ubora na gharama ya huduma za jamii zinazotolewa na Serikali. Baadhi ya huduma hizo ni pamoja na elimu, afya, maji, umeme na miundombinu ya usafiri na usafirishaji. Mathalani, kutokana na uboreshaji wa miundombinu ya barabara, muda na gharama za usafiri na usafirishaji wa bidhaa zimepungua, sambamba na gharama za matengenezo ya vyombo vya usafiri na usafirishaji. Aidha, upatikanaji wa huduma za afya karibu na wananchi umepunguza kwa kiasi kikubwa adha na gharama ya matibabu kwa wananchi. Pia, ugharamiaji wa elimu msingi bila malipo na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ni miongoni mwa matokeo ya kukua kwa uchumi. Kwa muktadha huu, ni muhimu kutafsiri dhana ya ukuaji wa uchumi na maisha ya wananchi kwa kuangalia kiwango cha upatikanaji, ubora na gharama za huduma muhimu za jamii zinazotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, dhana ya pili ya kutafsiri ukuaji wa uchumi na maisha ya wananchi ni ushiriki wa wananchi wenyewe katika shughuli za kiuchumi. Ukuaji wa uchumi ni matokeo ya wananchi kushiriki moja kwa moja kwenye shughuli za uzalishaji mali na huduma. Wananchi wanaoshiriki moja kwa moja kwenye shughuli za kiuchumi hufikiwa moja kwa moja na matokeo chanya ya ukuaji wa uchumi ikilinganishwa na wale ambao wapo nje ya mfumo wa uzalishaji. Aidha, wananchi wanaoshiriki moja kwa moja

kwenye shughuli za kiuchumi wananufaika kwa tafsiri ya dhana zote mbili; yaani kupitia huduma za jamii zinazotolewa na Serikali yao pamoja na matokeo ya moja kwa moja ya shughuli wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kufanya jitihada za dhati kabisa kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara, ili kila Mtanzania aweze kutumia kikamilifu fursa zilizopo kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali na huduma. Miongoni mwa hatua madhubuti zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ni pamoja na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara Nchini. Lengo ni kuhakikisha kwamba, tunapunguza kwa sehemu kubwa gharama za uwekezaji na kufanya biashara ili kuvutia wawekezaji mahiri katika sekta mbalimbali, hususan viwanda vinavyotumia malighafi za ndani. Ni matarajio ya Serikali yetu kuwa, uwekezaji katika viwanda utaongeza ajira na uzalishaji katika Sekta ya Kilimo, sekta ambayo huajiri idadi kubwa ya watu hapa nchini, lakini imekuwa ikikua kwa kasi ndogo na hivyo kuwa na mchango mdogo katika kupunguza umaskini wa wananchi walio wengi, hususan wakulima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika dhana nzima ya uchumi kukua ukioanisha na maisha ya wananchi, kinadharia kwa kweli alivyosema ni sahihi kabisa na napenda nipongeze kwa Serikali ya Awamu ya Tano ambayo imekuwa ikifanya kazi sasa kurekebisha na kurahisisha maisha ya wananchi yaweze kuwa na unafuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza; uhalisia wa maisha sasa hivi kwa wananchi ni ghali zaidi na hali ya maisha ya wananchi bado ni ngumu. Je, Serikali inaweka mkakati gani pamoja na kuonesha kwamba hata mkulima wa pamba ambaye



anauza pamba yake anakopwa halipwi na bado anategemea ahudumie baadhi ya gharama zake mwenyewe, je, ni lini Serikali sasa itaachana na mtindo huu kwa kutoa *guarantee* kwa wakulima wa mazao yote ili waweze kuwa wanapewa bei ambazo zinawakomboa katika shughuli zao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; sasa hivi bei ya vyakula inazidi kupanda na ukiangalia wananchi wengi wanaathirika na kupanda kwa bei ya vyakula. Gunia la mahindi sasa ni karibu Sh.100,000, je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza gharama hizi za maisha kwa wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo tukianza na swali la pili la Mheshimiwa Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Chegeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya kupanda bei, kushuka bei ni *relative*. Ni Bunge hilihili mwaka jana wakati bei ya mahindi kwa mkulima ilikuwa Sh.150, ni Wabunge hawahawa walilalamika na kusema kwamba kwa nini tunafunga mipaka. Sisi kama Serikali kupunguza gharama za bei sokoni hatua tunazochukua; moja ni kupunguza gharama za uzalishaji, mbili kuruhusu soko ku-*compete*, *competition* ndiyo itakayopunguza bei ya mazao sokoni. Pale ambapo mkulima anapata hasara hakuna mtu anayekwenda kum-*subsidize*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama Serikali hatua ya kwanza hatutaingilia bei kushusha, nini tunafanya; tunayo *National Food Reserve Agency* na nitumie Bunge hili kuwaambia Waheshimiwa Wabunge na Wakuu wa Mikoa; pale ambapo wanaona kwamba kuna upungufu wa mazao ya chakula sokoni wawasiliane na *National Food Reserve Agency* ambayo ita-*supply* chakula katika maeneo hayo ili kupunguza presha, lakini hatutaingilia kupunguza bei ya mazao kwa sababu wakulima wa nchi hii kwa muda

mrefu wamepata hasara kwa kuwafanyia *control* mazao yao. Huu ni msimamo wa Serikali na ieleweke. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, njia ya pili, tunahamasisha Watanzania, ardhi ya Tanzania ni *potential* kwa kilimo, watu wafanye jitihada kuongeza uzalishaji. *Supply* ikiwa kubwa, *demand* ikiwa ndogo mazao yatashuka bei, lakini hatutafanya *intervention* yoyote kwenda kupunguza bei. Njia pekee tunayofanya kama Serikali ni kutumia *National Food Reserve Agency* kwa ajili ya ku-*supply* mazao ya chakula sokoni na kupitia *NFRA* bei itapungua, lakini kusema bei ya chakula iko juu ni *relative*; ni saa ngapi bei ya chakula iko chini, ni saa ngapi bei ya chakula iko juu. Kitu cha muhimu ni kufanya jitihada kama nchi kuongeza *purchasing power* ya watu wetu na wakulima wetu waweze kufaidika. (Makofi)

**SPIKA:** Lile la pamba?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):**

Mheshimiwa Spika, tatizo la pamba lililojitokeza mwaka huu ni *special case*. Ni kama ilivyojitokeza kwenye korosho mwaka jana; Serikali ilifanya *intervention*. *Intervention* tulizozifanya mwaka jana, mwaka huu hatukuzitumia, tumeruhusu soko, minada inaendelea, wakulima wanapata pesa yao *on time* na *competition* iko wazi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pamba lilijitokeza katika msimu uliopita niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, halitajitokeza msimu ujao, tutaruhusu soko, hatutafanya kutangaza *control* ya *price*, Serikali itakachokifanya kwa wakulima wa pamba wasipate hasara ni ku-*control* gharama za *input* kuanzia viuatilifu, mbegu na mambo mengine, lakini siku ya mwisho sokoni tutaruhusu bei ili wafanyabiashara waende wakutane na wakulima sokoni waweze kununua bidhaa ile na mtu apate pesa yake kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa ni *special case* kwa sababu bei ya pamba duniani imeanguka na sababu ya

kuanguka ni kwa sababu ya mtikisiko na mgogoro uliopo kati ya China na Marekani, matokeo yake pamba imekosa bei. Serikali ikaamua kutangaza bei ya Sh.1,200 na ili wafanyabiashara wasipate hasara tukaamua kufanya mazungumzo na *financial institution* kuwapa *incentive* ili waweze kwenda kununua kwa bei ya Sh.1,200.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa wakulima wa pamba mpaka kufikia siku ya Ijumaa wamelipwa bilioni 437, ambacho hakijalipwa ni bilioni 43 tu ndizo ambazo hazijalipwa na sisi tunafanya jitihada kuhakikisha *by the end of this month* wakulima wa pamba waweze kulipwa fedha zao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili ili wasipate shida kwa sababu msimu unaanza tarehe 15, nitumie nafasi hii kuwaambia wasambazaji wa mbegu wote wawasambazie wakulima bila kuwauzia halafu tuta-*recover* gharama ya mbegu msimu utakaokuja. Sasa hivi wakulima waende shambani kwa sababu malipo yalichelewa, lakini wapo ambao hawajalipwa, kwa hiyo wapewe mbegu.

Mheshimiwa Spika, namwelewa Mheshimiwa Dkt. Chegeni, moja ya wilaya ambazo zimeathirika sana ni Wilaya ya Mheshimiwa Dkt. Chegeni, lakini tatizo hili halitajiruudia msimu ujao. Nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Nassir, nilikuona.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Urejeshwaji wa kodi kwa wakati kwa makampuni ambayo yamewekeza nchini kutasaidia kuimarisha uwekezaji nchini na hivyo kuimarisha kipato cha mtu mmoja mmoja; je, Serikali ina kauli gani juu ya hili?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

Waheshimiwa Wabunge, mnaona kitenge hicho?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali moja la nyongeza la mdogo wangu, Mheshimiwa Khadija Nassir, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ameuliza kuhusu urejeshwaji wa kodi, naamini ni Kodi ya Ongezeko la Thamani, kwa wanunuzi na viwanda vyetu. Kama Taifa tunatambua kwamba tulikuwa na changamoto kubwa ya udanganyifu kwenye eneo hili la urejeshwaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Hivyo kama Serikali tulianza mkakati wa kuhakikisha tunajiridhisha na kila muamala ambao unaletwa ili kuweza kurejesha Kodi hii ya Ongezeko la Thamani kwa wazalishaji wetu, wanunuzi wetu pamoja na viwanda vyetu ambavyo viko hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi tayari tumeshalipa zaidi ya asilimia 90 ya Kodi hii ya Ongezeko la Thamani kwa watu ambao walikuwa wanatudai. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hii asilimia 10 iliyobaki Serikali tunaendelea kujiridhisha na uhakika wa miamala yenyewe na tutazirejesha kwa wakati.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Katiba na Sheria, swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum Dodoma. Mheshimiwa Fatma, tafadhali.

Na. 61

### **Mpango wa Kutoa Vyeti vya Kuzaliwa kwa Watanzania Wenye Umri Zaidi ya Miaka Mitano**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza: -

Serikali imeanza kampeni ya kusajili watoto chini ya miaka mitano ili kupata vyeti vya kuzaliwa, lakini bado

Watanzania wenye umri zaidi ya miaka mitano na kuendelea hawana vyeti vya kuzaliwa:-

Je, Serikali imejipangaje kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa Watanzania wenye umri zaidi ya miaka mitano na kuendelea?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Mahiga tafadhali.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA*) imekuwa ikitekeleza Mkakati wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu ili kuboresha hali ya usajili nchini. Mkakati huo una mipango mbalimbali ambayo imekuwa ikitekelezwa na Serikali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Watanzania wote wenye umri wa zaidi ya miaka mitano wanasajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya mipango hiyo ni kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wote waliopo kwenye mfumo rasmi wa elimu na kufanya kampeni za uhamasishaji kwa kuwafuata wananchi katika maeneo yao ya makazi.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu wa kusajili watoto waliopo katika mfumo rasmi wa elimu umefanikiwa kusajili jumla ya watoto 325,583 wenye umri wa miaka mitano hadi 17 katika jumla ya wilaya kumi na tisa ambazo ni Njombe, Ludewa, Makete, Wanging'ombe, Ilala, Kinondoni, Kigamboni, Temeke, Iringa, Kilindi, Musoma, Bariadi, Tarime, Singida, Songea, Bunda, Maswa, Kahama na Manyoni. Wakala utaendelea na utaratibu huu ili kuhakikisha wilaya zote nchini kulingana na mpango uliopo.

Vilevile wakala umeendelea kuwafikia wananchi wasio katika mfumo rasmi wa elimu kupitia kampeni za maadhimisho mbalimbali ya kitaifa na hasa kama vile

maonesho ya Saba Saba na Nane Nane yanayofanyika nchini kwa kutoa elimu ya muhimu wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhadini (*RITA*) unatarajia kuanzisha huduma ya usajili kwa njia ya mtandao ili kuwafikia wananchi wengi kwa urahisi ambapo wananchi wataweza kufanya maombi yao katika mfumo wa mtandao na baadaye kufika ofisi ya *RITA* iliyo karibu na hasa katika maeneo ambapo Serikali za Mitaa zipo.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhadini (*RITA*) umejiwekea malengo ya kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa wananchi wapatao 15,917,602 ifikiapo mwaka 2025. Idadi hii itafanya wananchi wasio na vyeti vya kuzaliwa kupungua hadi kufika 21,508,277 ambao ni chini ya asilimia 50 ya wananchi wote ambao wamefikisha umri wa zaidi ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa wananchi wote ambao hawana vyeti vya kuzaliwa kufika kwenye Ofisi za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhadini (*RITA*) kwa ajili ya kusajiliwa na kupewa vyeti vya kuzaliwa ikiwa ni haki yao muhimu ya kutambuliwa. Kadhalika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kuendelea kushirikiana na Serikali kwa kuwaelimisha wananchi katika majimbo yenu juu ya umuhimu wa kusajili matukio muhimu ya binadamu ikiwa ni pamoja na kujisajili na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Taufiq ameridhika.

**MHE. FATMA HASSAN TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Sambamba na hilo nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na mpango mzuri wa *RITA* kuwa ifikapo 2025 kwamba idadi ya watanzania wasiokuwa na vyeti itakuwa imepungua kwa kufikia 46.5% ambayo bado ni idadi kubwa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya

kampeni maalum ya muda maalum ili kuhakikisha kwamba idadi ya watanzania wasiokuwa na vyeti vya kuzaliwa inapungua hadi kufikia 10%?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuanzisha usajili kwa kupitia njia ya mtandao, na baadhi ya wananchi wengi bado hawajui kutumia mtandao. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka kompyuta katika kila Tarafa hapa nchini ili wale wananchi ambao hawana uwezo wa kutumia mitandao hiyo wakaenda kujisajili katika maeneo ya Tarafa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa maswali hayo muhimu, Mheshimiwa Dkt. Mahiga tafadhali.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mbunge kwa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Moja ikiwa inahusiana na kampeni ya kuwafikia watu waone umuhimu wa kuandikisha watoto kabla ya miaka mitano na kampeni ambayo sasa hivi tunaendelea nayo ya kusajili watoto waliozaidi ya miaka 15. Mbali na mfumo wa kuandikisha katika shule, kampeni zetu zinaendelea, *RITA* wanampango kwenye redio, wana mpango kwenye *television* na pia katika matukio mbalimbali ya kitaifa. Kuna vipeperushi ambavyo vinaeleza kila pale ambapo tuna nafasi, lakini pia tunashirikiana na mitandao mingine kama vile Uhamiaji na *NIDA* ili kupeleka taarifa hii hasa *NIDA* ambao ili kuandisha na kumpa mtu kitambulisho cha Taifa wanahitaji vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, mtandao huu tutautumia kwa makini, na tusaidiane na ninyi Wabunge katika hotuba zenu, katika mikutano yenu umuhimu wa kuwahamasisha wananchi wajiandikishe kwa kutumia ofisi zetu zilizoko kwenye Kata na kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, masuala ya kompyuta na mtandao, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kutuelimisha na sisi Wabunge tuanze kutumia *tablets* na tunajifunza. Hii ni elimu endelevu kwa kuanzia hapa Bungeni

ambayo lazima iwafikie wananchi, hatujauliza gharama za sisi hapa Wabunge kupewa *tablets* lakini kuna gharama. Itakuwa ni busara sana na wazo hili tunalichukua kuweza kufikisha vyombo hivi vya kompyuta siyo tu kwenye Serikali za Mitaa, lakini kufikisha mpaka kwenye Tarafa. Nashukuru Wizara ya Elimu ambayo sasa hivi imeingiza mfumo wa kufundisha kompyuta na matumizi ya *IT*.

Mheshimiwa Spika, suala hili ni changamoto kwa Taifa, nawaomba Wabunge kama kutakuwa katika bajeti za Wizara mbalimbali tukiomba fedha za kuleta mfumo wa *Information Technology* mtupitishie fedha hizo. Katika hili suala la uandikishaji naomba mtusaidie sana ili watu wa kawaida waweze kunufaika na kuwa na kompyuta. Siyo tu kwa ajili ya kuandikisha ili wapate vyeti, lakini kompyuta ni sawa na kujifunza kusoma na kuandika katika karne ya 21. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo swali linaulizwa na Mheshimiwa Senator Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa.

Na. 62

## **Muswada wa Kudurusu Sheria ya Tumbaku**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa kudurusu Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2004 Bungeni?

**SPIKA:** Tunaendelea na majibu ya Serikali, tunaendelea na majibu ya Serikali, Mheshimiwa nakuomba ukae kwenye kiti chako. (*Makofi*)

Mnaweza kujikuta mnamponza tena, *I'm not joking* mnanifahamu! (*Kicheko*)



Tunaendelea, majibu ya swali hilo la Kilimo lililoulizwa na Mheshimiwa Mwambalaswa, Mheshimiwa Bashe.

**NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zao la tumbaku hapa nchini husimamiwa na Sheria ya Tumbaku Na. 24 ya Mwaka 2001 Sura ya 202 ya Sheria za Tanzania pamoja na Kanuni na Sheria ya Tumbaku ya Mwaka 2012 (Tangazo la Serikali Na. 392 la Mwaka 2012). Kabla ya Sheria Mwaka 2001 zao la tumbaku lilikuwa likisimamiwa na Sheria ya Bodi ya Tumbaku ya Mwaka 1984 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 1997 ambazo zilifutwa kwa Sheria ya Tumbaku Mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya urasimishaji uanzishaji wa Bodi za mazao, Sheria ya sekta ya Tumbaku ilifanyiwa marekebisho na Bunge Mwaka 2009 kupitia Sheria Na. 20 ya Marekebisho ya Sheria. Pamoja na mambo mengine Sheria ya Tumbaku iliweka tafsiri ya maneno mbalimbali ikiwemo usimamizi, ugharamiaji wa majukumu ya pamoja, muendelezo wa zao kuwa miongoni mwa majukumu ya pamoja, ugharamiaji wa majukumu ya pamoja, mkutano wa wadau wa wakulima, kilimo cha mkataba, majukumu ya udhibiti na tafsiri yake.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria za Kanuni za Tumbaku yanaenda sambamba na marekebisho ya Sheria za Bodi za Mazao ambapo Serikali inakusudia kuanzisha Mamlaka ya Mazao ya Kimkakati (*Tanzania Strategic Crop Authority- TASCA*) ikiwemo zao la Tumbaku. Aidha, Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Bodi za Mazao kwa ajili ya kuanzisha mamlaka hiyo unatarajiwa kuwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Nane, mwezi Januari, 2020.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambalaswa swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwa kweli sina swali la nyongeza isipokuwa nataka kumpa ushauri Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu nina imani naye sana na nina imani kwamba ataleta mabadiliko katika zao la tumbaku na mazao mengine ya kimkakati na ajue kwamba tutamhesabu kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni huu, mwaka 2009 huohuo ambapo Serikali ilileta mabadiliko kwenye sheria kwa kupitia kwa mabadiliko ya sheria mbalimbali, mwaka huohuo 2009 Bunge hili liliridhia Mkataba wa Kimataifa wa ku-*control* matumizi ya tumbaku. Baada ya kuridhia mkataba huo, ilitakiwa sasa Serikali ilete mabadiliko ya sheria ya 2001 kwa ujumla siyo kupitia *Miscellaneous Amendments*. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri wataalam wako wakupe huo mkataba wa kimataifa ambao tuliridhia mwaka 2009 ambao ukiuchukua huo mkataba utaidurusu sheria hii ya 2001 kwa faida ya wakulima wa tumbaku. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ulichopata ni ushauri, kwa hiyo uchukue tu moja kwa moja. Naendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Ushauri huo ni muhimu sana wa Mheshimiwa Mwambalaswa. Tunaendelea na Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga.

Na. 63

**Kujenga Barabara ya Kalenga – Ruaha *National Park*  
kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. GODFREY W. MGIMWA** aliuliza:-

Barabara ya Kalenga kuelekea Ruaha National Park ni ya muhimu sana kwa uchumi wa Jimbo la Kalenga, Iringa na Tanzania kwa ujumla:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano litajibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mheshimiwa Elias Kwandikwa tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kalenga kuelekea Ruaha *National Park* ambayo inajulikana kama barabara ya Iringa – Msembe ni barabara ya mkoa inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Iringa. Barabara hii ina urefu wa kilometa 104, kati ya hizo, kilometa 18.4 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 85.6 zimejengwa kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inaunganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Iringa na Mbuga ya Wanyama ya Ruaha na inapita katika maeneo muhimu ya Makumbusho ya Mkwawa na maeneo mengine yenye kilimo cha mpunga na mahindi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*), imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami na kazi hii imefanywa na Kampuni ya *ENV Consult (T) Ltd* ya hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya shilingi billioni 4.221 zimetengwa kwa ajili ya

maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Godfrey Mgimwa nimekuona.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi lakini pia niishukuru Serikali kwa majibu mazuri kwa sababu barabara hii imekuwa ni ya muhimu sana lakini sasa tumeenda kupata hizi bilioni 4 kwa hiyo tunaishukuru sana Serikali kwa jitihada hizi.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, swali la kwanza ningependa kujua je, katika utaratibu ambao unaendelea sasa hivi wa upembuzi yakinifu, Serikali imejipaga vipi kuhakikisha kumba fidia kwa wananchi wale katika barabara ile inapatikana kwa wakati na yenye tija?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nilitaka nifahamu, kuna barabara ambayo inatoka Wasa kuelekea Kiponzelo mpaka Kalenga ambapo unaenda kuunganisha katika na hiyo barabara ya Ruaha Msembe. Ningependa kufahamu, kwa kuwa barabara hii nayo ni ya muhimu sana kiuchumi. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inaitengeneza au kuiboresha barabara hii katika kiwango cha lami ili wananchi wa maeneo haya waweze kuungana na wale wanaoenda Ruaha *National Park*? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Elias Kwandikwa tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mgimwa kwa sababu amekuwa akifuatilia sana barabara hii na barabara nyingine hii ya Wasa – Kiponzelo – Kalenga aliyoitaja. Serikali imekamilisha uthamini, wa wananchi watakuwa na stahili

ya kupata fidia katika maeneo haya na takribani shilingi bilioni 2 imekadiriwa kwamba itatumika kuwalipa fidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie tu kabla ujenzi haujaanza kama ilivyo taratibu wananchi hawa wa maeneo haya watalipwa fidia kama wanavyostahili kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara yako ile uliyoitaja Wasa – Kipanzelo – Kalenga takribani kilomita 70 hivi, ni barabara ambayo inasimamiwa na wenzetu upande wa *TARURA* na sisi mkazo mkubwa kupitia Mfuko wa Barabara ni kuhakikisha kwamba wanapata fedha za kutosha barabara iweze kupitika.

Kwa hiyo, utaratibu wa sasa wa Serikali ni kuunganisha maeneo ya mkoa na mkoa, na maeneo muhimu ya uzalishaji. Kwa hiyo, siku za mbeleni pia barabara hii tutaitazama baada ya kuwa muunganiko umekuwa mzuri kwa barabara za lami.

**SPIKA:** Kuna watu hawajaongea siku nyingi humu, Mheshimiwa Halima. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, Moja kati ya barabara ambazo ni muhimu sana hasa katika foleni za Dar es Salaam ni barabara ya Chuo cha Ardhi - Makongo – Goba. Ninatambua kwamba baada ya kero ya muda mrefu sana hatimaye barabara itaanza kujengwa. Sasa swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, changamoto kubwa iliyopo ni fidia ya wananchi ya shilingi bilioni 3 na tumekuwa tukizungumza kwa kipindi kirefu sana.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nipate *commitment* ya Serikali ni lini wananchi hawa ambao wako tayari kuachia maeneo yao watalipwa fidia yao stahiki ili barabara ijengwe kwa viwango ambavyo ilikuwa imetarajiwa kujengwa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi Mheshimiwa Waziri mwenyewe, oooh! Tafadhali.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge Halima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumeanza kujenga ile barabara ya Makongo lakini kuhusiana na swali lako fidia italipwa kwa mujibu wa sheria, sheria ipo ilitungwa na Bunge. Kwa hiyo, siyo *commitment* ya mtu hapana, kwa mujibu wa sheria.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Nsanzugwako nilikuona.

**MHE. DANIEL N.NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona nina swali la nyongeza, shida iliyoko Kalenga inafanana sana na shida iliyoko katika Mkoa wa Kigoma. Barabara ya Uvinza – Malagarasi ni ahadi ya muda mrefu na tumeambiwa huu ni mwaka wanne kwamba kuna fedha za Abu Dhabi *Fund*.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujua hizo fedha Abu Dhabi *Fund* zipo kweli au hazipo ili tujue kwamba barabara hiyo haitajengwa. Maana Mheshimiwa...

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri jibu zipo au hazipo.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, fedha zipo.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunakwenda Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete. Mheshimiwa Mbarouk tafadhali.

Na. 64

## **Pemba Kuunganishwa na Soko la Afrika Mashariki**

**MHE. MBAROUK SALIM ALI** aliuliza:-

Pemba ni Kisiwa kinachozalisha viungo (*spices*) kwa wingi na wajasiriamali huzalisha bidhaa zinazotokana na viungo hivyo:-

Je, ni lini wakulima na wajasiriliamali wa Pemba wataunganishwa na soko la Afrika Mashariki ili waweze kufaidika na soko hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumtaarifu Mhe. Mbunge kuwa, wananchi wa Pemba na wa maeneo yote ya Tanzania wamekwisha unganishwa na soko la Afrika Mashariki kupitia Itifaki za Umoja wa Forodha na ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa mkulima au mjasiriamali yoyote kuweza kuuza bidhaa zake ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki anapaswa kukidhi vigezo vya Afrika Mashariki vya kutambua uasili wa bidhaa (*Rules of Origin*). Nchi Wanachama zilikubaliana na kuweka vigezo vinavyoshabihiana kama bidhaa husika imezalishwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vigezo hivyo vimejengwa katika misingi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bidhaa kuzalishwa ndani ya Jumuiya kwa kiwango cha asilimia mia moja mfano, bidhaa za kilimo, uvuvi, madini na kaadhali; bidhaa kuzalishwa ndani ya Jumuiya kwa kutumia malighafi ya kutoka nje yenye thamani (*ex-works price*) ya kiwango kisichozidi asilimia 70 ya bei ya bidhaa hiyo bila kodi ikiwa kiwandani, mfano *label za plastiki*, kuongeza ugumu wa kioo, utengenezaji wa nyaya za umeme na vifaa vingine vya umeme, utengenezaji wa pikipiki na baskeli n.k; bidhaa zinazozalishwa ndani kwa kutambua mchakato katika uzalishaji (*process rule*) kama vile uunganishaji wa magari na kusafisha mafuta ya petroli (*refining*); na bidhaa kubadilika utambuzi wa uasili kwa kubadilika umbo na matumizi kutokana na mchakato wa viwandani mfano malighafi ya plastiki kuchakatwa kuwa meza, viti, sahani n.k.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia misingi ambayo nimekwisha ielezea hapo juu, nichukue fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwashauri wananchi wa Pemba na Tanzania kwa ujumla kuzichangamkia fursa za kibiashara, ajira, uwekezaji n.k. zitokanazo na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kujihakikishia maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kuwasihii wananchi kuzitambua taratibu za kufuata katika kuzitumia fursa za kibiashara zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na kuwa na cheti cha Uasili wa Bidhaa (*East African Communicate Certificate of Origin*) na vibali/nyaraka zinazobainisha kuwa bidhaa imezalishwa ndani ya Jumuiya kutoka mamlaka husika kutegemea na aina ya bidhaa mfanyabiashara anazotaka kuuza/kununua katika soko la Afrika Mashariki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu hayo nina maswali mawili madogo tu ya nyongeza. Katika majibu yake ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wananchi wa Pemba pamoja



na wananchi wetu wa Tanzania tayari wameshaunganishwa na soko hili la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, bado niko kwa Pemba tu, nataka nijue kwamba hii Pemba imeunganishwa kinadharia au kivitendo kwa sababu karibu mwaka wa saba huu Viongozi Wakuu wa Afrika Mashariki walikubaliana kujenga bandari ya Wete. Hizo ni jitihada na fedha kwa mujibu wa Naibu wa Wazara hii hii aliyepita ambaye kwa sasa hivi ni Naibu katibu Mkuu wa CCM Zanzibar alisema kwamba fedha tayari zilishakuwepo. Lakini mpaka leo hakuna lolote ambalo limefanyika nilitaka kujua ni nadhalia au ni vitendo.

Mheshimiwa Spika, hizo ni jitihada na fedha. Kwa mujibu wa Waziri wa Wazara hii aliyepita ambaye sasa hivi ni Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, alisema kwamba fedha tayari zilishakuwepo, lakini mpaka leo hakuna lolote ambalo limefanyika. Nilitaka kujua, ni nadharia; ni vitendo?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake pia amewataka wananchi kwa ujumla watumie fursa zilizopo ili kullitumia soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Niseme tu kwamba kuna vikwazo vikubwa vya tozo nyingi pamoja na ushuru hasa katika uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa hizo:-

Je, ni lini Serikali nitaondoa tatizo hili hasa kwa wajasiliamali?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Majibu ya Maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, namshukuru Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete kwa kuuliza maswali yake mawili ya nyongeza. Swali la kwanza amesema: Je, Pemba

imeunganishwa kwa nadharia au kwa vitendo? Akitolea mfano ujenzi wa bandari kule Pemba.

Mheshimiwa Spika naomba kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Pemba imeunganishwa kwa vitendo kwa sababu Pemba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jamhuri yote ya Muungano wa Tanzania imeunganishwa kwa vitendo kwa maana ya soko la pamoja, ambapo ndilo swali lake la msingi. Kwa maana ya mradi ya kimaendeleo ambayo ameisema, miradi hiyo inafanyika sehemu mbalimbali, sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuhusiana na Bandari ya Pemba tulishajibu ndani ya Bunge hili kwamba Serikali kwa kushirikiana na Afrika Mashariki inashughulikia mradi huo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, anasema kuna vikwazo vikubwa vya tozo na ushuru. Maana ya soko la pamoja ni kwamba endapo bidhaa inakidhi vigezo vya uasili wa bidhaa (*rules of origin*), haipaswi kutolewa ushuru au tozo yoyote endapo inasafirishwa au kuuzwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bidhaa ambazo hazikidhi vigezo kama niliongea kwenye jibu la msingi, ni kwamba zimetolewa nje ya Jumuiya Afrika Mashariki, lazima zilipe ushuru au *common external tariff* ambayo imewekwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tuendeleo na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Swali la Mheshimiwa Sebastian Kapufi, nimekuona Mheshimiwa Kakoso kwa niaba yake.

Na. 65

**Fedha za Mkupuo kwa Ujenzi wa Hospitali  
ya Mkoa – Katavi**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO (K.n.y. MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI)** aliuliza:-

Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Katavi ni muhimu kwa mustakabali wa afya ya wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani wa ugawaji wa fedha za mkupuo ili kuhakikisha ujenzi huo unakamilika?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Dkt. Ndugulile tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa kipaumbele katika ujenzi wa

Hospitali za Rufaa za mikoa mipya mitano ya Njombe, Katavi, Songwe, Simiyu na Geita ambayo haina Hospitali za Rufaa za Mikoa. Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Katavi umeanza katika eneo jipya lenye ukubwa wa ekari 243.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetoa shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi. Serikali itaendelea na ujenzi wa hospitali hii kwa awamu kwa kutegemea na hali ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru sana Serikali kwa kutoa fedha karibu shilingi bilioni moja kwa ajili ya Hospitali ya Mkoa wa Katavi. Kasi ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Katavi inaenda kwa kusuasua sana na Mheshimiwa Waziri alituahidi kutupa fedha karibu

shilingi bilioni nne ili ziweze kujenga hospitali hiyo: Je, ni lini Serikali italeta hizo fedha?

Mkoa wa Katavi una Chuo cha Uuguzi ambacho ni cha muda mrefu sana yapata miaka 10 hakijaendelezwa: Je, ni lini Serikali itamalizia hiki Chuo cha Uuguzi ili watu weweze kupata huduma za kimsingi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, Serikali imetenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 3.4, tumeshatanguliza shilingi bilioni 1.5 na fedha hizi zipo, kadri Mkandarasi anapokuwa anaendelea na kazi na ana-raise certificate, sisi Serikali tutaendelea kufanya malipo.

Mheshimiwa Spika, lengo na kusudio la Serikali ni kuhakikisha hospitali hii inakamilika na kwamba baada ya hapo, ile Hospitali ya Mpanda ambayo ilianza kama Kituo cha Afya na sasa hivi imekuwa ndiyo Hospitali ya Mkoa, tuweze kuirejesha katika Halmashauri na kuweza kuhudumu kama Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ameulizia kuhusiana na Chuo cha Afya cha Uuguzi kilichopo pale. Ni kweli, nami nimewahi kufika pale Mpanda tumekiona. Wizara ilituma timu kwenda kufanya mapitio na kuangalia hali ya majengo na uhitaji. Sasa hivi tupo katika mkakati wa kuangalia matumizi bora ya kile chuo. Pindi taratibu zitakapokamilika tutawapa taarifa Mkoa wa Mpanda, jinsi gani ya kuweza kukitumia kile Chuo kwa malengo ambayo tulikuwa tumekusidia.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Chiza.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, swali langu lilikuwa upande wa pili, halikuwa hapa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa.

Na. 66

### **Kuwawajibisha Watoto Wanaotelekeza Wazazi Wao**

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA** aliuliza:-

Baadhi ya watoto wakubwa wenye uwezo wameamua kuwatelekeza wazazi wao pasipo kuwapa matunzo wanayostahili:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawajibisha watoto waliotelekeza wazazi wao na kuhakikisha wanatoa matunzo stahili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, Mbunge wa Viti Maalum kama ipasavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa wazee katika ustawi wa Taifa letu. Sote tunatambua kuwa wazazi walitumia rasilimali walizokuwanazo kuhakikisha watoto wanapata huduma za matunzo na malezi ili kuwawezesha kukua na kufikia ndoto zao.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mifumo ya hifadhi ya jamii ya asili, jukumu la kuwatunza na kuwalea wazazi au wazee ni la wanafamilia, hususan watoto. Kutokana kudhoofika kwa mifumo hiyo ya asili, mmomonyoko wa maadili na utandawazi, jukumu hilo limekuwa na changamoto nyingi na kusababisha wazazi kutelekezwa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuhakikisha maslahi ya wazee yanalindwa na wanapata haki zao ikiwemo matunzo, Serikali iliandaa Sera ya Wazee ya mwaka 2003 ambayo inaelekeza jamii kuwajibika kutoa matunzo kwa wazee.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hakuna sheria ya kuwajibisha watoto wanaotelekeza wazazi wao. Serikali itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha jamii kutambua jukumu lao la malezi na matunzo kwa wazazi ambao ni hazina na tunu muhimu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kutoa rai kwa watoto na jamii kwa ujumla kuhakikisha wazazi na wazee wanapatiwa malezi na matunzo yanayostahili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Tisekwa, tafadhali nimekuona.

**MHESHIMIWA DKT.JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake kuonyesha kwamba Serikali inatambua mchango wa wazazi ambao wamehangaika kutulea hadi kufikia hapa tulipo. Tukumbuke kwamba hata vitabu vitakatifu vya Mungu, kwa mfano amri kumi za Mungu ni amri ya nne pekee ambayo inatoa na ahadi kwamba ukiheshimu wazazi utapata baraka na utaishi miaka mingi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutatunza wazazi, wenzetu ambao wazazi wapo hai ni vizuri, *it is a blessing*. Tuendeleo kuangalia wazazi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina maswali mawili ya nyongeza kwamba Je, Serikali ipo tayari kutunga sheria itakayowabana watoto hawa wanaotelekeza, ili waweze kuwatunza wazazi wao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Je, wakati tunasubiri hiyo sheria kutungwa, Serikali ipo tayari kuweka Dawati la

Wazee ili waweze kusikilizwa katika malalamiko yao, hasa kwa wale ambao wanatelekezwa na watoto wao? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu ya maswali hayo kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Jasmine Tisekwa Bunga. Swali lake la kwanza ameuliza kwamba, je, Serikali iko tayari kutunga sheria ya kubana watoto ambao wanawatelekeza wazee? Niseme tu kwamba kwa sasa hivi hatuna mpango huo kama Serikali. Tunajikita na kujielekeza zaidi katika kutoa elimu kwa jamii kuhakikisha kwamba wanatambua wajibu wao na kutimiza majukumu yao ya kutunza na kulea wazee.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameuliza kwamba, je, tuko tayari kuanzisha Dawati la Wazee? Niseme kwamba tunayo mifumo kupitia Maafisa Ustawi wetu wa Jamii ambao majukumu yao ni pamoja na kuhakikisha kwamba huduma kwa wazee zipo. Kwa hiyo, wale wazee ambao wanaona kwamba matunzo au zile haki za msingi hawazipati, ni vizuri wakafika kwa Maafisa Ustawi wa Jamii ili kupata msaada wa kuwaunganisha na watoto wao.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tuna nyumba za kuwatunza wazee 17 na tuna wazee takribani kama 500. Nasi Serikali tunachukua tu wale wazee ambao imedhibitika kwamba hawana watoto, hawana ndugu, jamii ile inayowazunguka haiwezi kuwatunza, ndipo pale Serikali inawachukua na kuwatunza.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Susan, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi. Ilikuwa ni kilio cha

muda mrefu kwamba kwa kuwa Sera ya Wazee ipo toka mwaka 2003, lakini sheria hamna ndiyo maana wazee wanaendelea kunyanyasika. Hata hivyo, kuna Sheria ya Watoto ambapo mzazi asipomlea mtoto au asipompa matunzo, anashtakiwa.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini basi kusiwe na sheria ambayo italazimisha mtoto au kijana, mtu mzima aweze kumlea mzazi wake kwa sababu tunajua kwamba wazee hawa kwa kweli wamefanya kazi kubwa, wamewasomesha watoto, lakini watoto wamewatelekeza. Ni kwa nini kama kuna Sheria ya Watoto, kusiwe na Sheria ya Wazee ambayo itarahisisha sana maisha ya wazee hapa Tanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa, nanyi muwe mnakula mnaweka, siyo mtategemea kuja kutunzwa na watoto tu. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, changamoto ya wazee tutazidi kuiona ikiongezeka na hii ni kwa sababu ya maendeleo makubwa ambayo tumeyapiga katika huduma zetu za jamii. Sasa hivi wastani wa Mtanzania kuishi miaka 64. Kwa hiyo, tunatengemea tutakuwa na idadi kubwa sana ya watu ambao wanaitwa wazee, kwa sababu vifo vimepungua na hali ya afya nayo imeboreka sana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Sera ya Afya ni ya mwaka 2003 na sasa hivi tumeiona kwamba imepitwa na wakati. Tupo katika marejeo ya kuipitia hii Sera mpya ya Afya. Tukapoikamilisha, tuangalia sasa uwezekano kwa kuja na sheria mpya ambayo sasa itakuwa inaweka haki za wazee katika msingi mizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, hili ambalo analisema Mheshimiwa Susan Lyimo ni moja ya jambo ambalo tunaweza tukalizingatia.



**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea. Waheshimiwa wabunge, kwa sababu ya muda, tunajielekeza katika Wizara ya Mambo ya Ndani kwa swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja.

Na. 67

### **Kuongezeka kwa Matukio ya Ajali za Moto**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA** aliuliza:-

Matukio ya watu kupoteza maisha kutokana na ajali za moto yamezidi kuongezeka nchini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukiwezesha Kikosi cha Zimamoto ili kufanya kazi ipasavyo kwenye Miji na nje ya Miji?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pia, Serikali imekuwa ikitenga na itaendelea kutenga fedha za maendeleo katika bajeti ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kuzima moto pamoja na vifaa mbalimbali vya kuzima moto na uokoaji ili kutoa huduma zake ipasavyo ikiwemo kwenye miji na nje ya miji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inashirikiana na Shirika la Nyumbu katika utengenezaji wa magari mapya ya kuzima moto na uokoaji. Pia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limesaini hati ya makubaliano na Kampuni ya *ROM Solution* ili kupata mkopo

wenye masharti nafuu utakaowezesha kupata vitendea kazi mbalimbali ikiwemo magari ya kuzimia moto na uokoaji pamoja na vifaa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo nje ya Miji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutoa elimu kwa Umma ya kuzuia na kupambana na majanga mbalimbali ili kuzuia na kupunguza matukio ya moto nchini. Pia, Serikali inaendelea kuwasisitiza wananchi kumiliki vizimia moto katika maeneo yao ili kuukabili moto katika hatua za awali.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Devotha, swali la nyongeza.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Matukio ya ajali ya za moto, malori ya matenki ya mafuta yanaendelea kughalimu maisha ya Watanzania kwa kushabisha vifo na vilema vya kudumu. Tukio la Agosti 10, 2019 katika eneo la Msamvu eneo la Morogoro watu zaidi ya 100 walipoteza maisha, lakini umbali wa Ofisi za Zimamoto pale Morogoro haifiki kilometa moja kuelekea pale msamvu lilipotokea tukio.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwalipa fidia wapendwa waliopoteza maisha yao pale, kwa sababu *fire* ilifika pale kuzima moto wakati watu wameshateketea na kuwa majivu na kuni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Waziri Mkuu wakati wa mazishi yale pale Msamvu aliagiza kuunda Tume ya Kuchunguza Ajali ya Msamvu.

Je, ni kwa nini mpaka sasa Ofisi ya Waziri Mkuu haijatoa tamko lolote juu ya tume iliyozwa kuchunguza ajali ya tukio la Msamvu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhali.

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili kwa pamoja ya Mheshimiwa Devota Minja Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijajibu swali lake, naomba nisisitize majibu ya msingi ambayo niliyazungumza kuhusiana na mkakati wa Serikali ya kuimalisha Jeshi letu la Zimamoto na Uokoaji katika kulipatia vifaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mbali na jitihada ambazo nimezungumza za kutenga bajeti ambapo kwa mwaka huu peke yake tumeshapokea karibu shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ununuzi wa magari ya moto na vifaa vya uokoaji, lakini pia kuna mipango mbalimbali ikiwemo mkopo ambao nimezungumza, wa takribani *Euro* milioni 408 ambayo tunatarajia pamoja na mambo mengine kujenga vituo katika kila wilaya, kununua vifaa mbalimbali vya uokoaji ikiwemo magari, helkopta, boti na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba tukapokuwa tumekamilisha mikakati hii na ikawa ipo vizuri, basi changamoto zote zinahusiana na majanga ya moto ikiwemo kama hili ambalo limetokea Morogoro, yatakuwa sasa tunayakabili kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja yake *specific* kuhusu ripoti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kamati ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imepewa kazi. Kwa kuwa hii ilikuwa ni Kamati ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nadhani siyo mamlaka yangu kuitolea kauli.

Mheshimiwa Spika, nina hakika kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia Ofisi yake, kuna utaratibu ambao umewekwa wa kuweza kuitolea taarifa pale ambapo mwenyewe ataona inafaa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira ambapo Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hili. Ni imani yangu kwamba Kamati ile imeendelea kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, lengo na dhamira ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kuhakikisha kwamba taarifa ya ripoti ile inatupatia mapendekezo ambayo yanasababisha hatua zichukuliwe, lakini pamoja na kuepukana na matatizo kama haya yasitokeze siku zijazo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuulizwa swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Ngara hatuna gari la Zimamoto na yameshatokea majanga mara nyingi na ya kusababisha vifo; na ni barabara inayopitisha magari makubwa yanayobeba mafuta yakielekea nchi za jirani Rwanda, Burundi na Kongo:-

Je, ni lini Serikali itatuletea gari la Zimamoto Wilaya na Ngara? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niendeleo kumpongeza Mheshimiwa Oliver kwa jinsi ambavyo amekuwa akipambana kuhakikisha kwamba changamoto mbalimbali zinazohusu vyombo vya usalama katika Mkoa wa Kagera zinapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja yake ya kupeleka gari la zimamoto katika Wilaya ya Ngara, nimhakikishie kwamba pale ambapo mikakati ambayo nimeizungumza kwenye jibu la msingi itakapokuwa imekaa tayari, basi moja katika maeneo ambayo tunayazingatia ni Wilaya ya Ngara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel nilishakutaja.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ajali za moto zimekuwa ni kubwa sana katika taifa; katika taasisi za Serikali na hata katika mabweni ya shule. Sasa nauliza, najua ni lazima kuwepo na *fire extinguishers* katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini sasa sheria isije Bungeni ikarekebishwa, au kanuni ikarekebishwa kusudi iwe ni lazima kuwa na *smoke detectors* katika mabweni ya shule na katika taasisi za Serikali ili ule moshi uweze kung'amuliwa mapema na kuzia madhara makubwa yanayosababishwa na moto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali; hizo *smoke detectors* ni lazima pawe na sheria?.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Molel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni ushauri basi tunaipokea na tuitafakari na kuona ni jinsi gani tunaweza tukaifanyiakazi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Kabla hatujavuka, Mheshimiwa mtaalam wa majanga, Mheshimiwa James.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Kwa kuwa majanga yanayosababishwa na binadamu ni zaidi ya asilimia 96 ya majanga yote. Serikali haioni umuhimu wa kuhakikisha kunakuwa na somo rasmi kwenye mfumo rasmi wa elimu wa namna ya kujilinda, kujinga na kujiokoa na majanga hapa nchini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mabtia, Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nao vilevile ni ushauri; nadhani mamlaka husika zimeusikia, lakini kama Serikali tumeuchukua na tutafakari kuona kama kuna haja ya kufanya hivyo kwa wakati huu.

**SPIKA:** Ahsante, bado tuko Wizara ya Mambo ya ndani, Mheshimiwa Asha Abdulla Juma, uliza swali lako sasa.

Na.68

**Kupandishwa Daraja Askari wa Vyeo vya Chini**

**MHE. ASHA ABDULLA JUMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mfumo gani wa kupandishwa daraja askari wenye vyeo vya chini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdulla Juma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi vina mfumo wa Upandishwaji wa madaraja kwa askari wa vyeo vya chini ambayo huzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo umbele kwa maana ya *seniority*, miaka mitatu ya cheo alichonacho, tabia njema, nidhamu, utendaji mzuri, umahiri wa kazi, elimu au utaalumu mahsusi, uwezo wa kumudu madaraka ya cheo anachopandishwa, kutokuwa na tuhuma zinazochunguzwa wala mashtaka ya Kijeshi katika kipindi cha miaka mitatu na bajeti tengefu kwa mwaka husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha, nimekuona.

**MHE. ASHA ABDULLA JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri yaliyosheheni vigezo.

Mheshimiwa Spika, askari wa Jeshi letu la Polisi wanafanyakazi nzuri sana ikiwepo usalama barabarani, usalama wa raia na mali zao na kutuelimisha kutii sheria bila shuruti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wako baadhi ya askari ambao hawakupandishwa cheo mpaka wamefikia kustaafu, na kwa kuwa kutokupandishwa huko si kosa lao, ni kosa la mfumo; je, Serikali ina mpango gani wa kuwafidia ili wasiwe wamepoteza haki zao na hasa kwa vile sasa hivi wako wastaafu wanahitaji sana fedhahizo?

Mheshimiwa Spika, swali langu lingine; Je, Serikali haioni umuhimu wa kuandaa mfumo na utaratibu uliowazi kabisa unaoonyesha namna gani na vigezo gani vya kuweka nafasi ya kwenda *course* ili uweze kupandishwa cheo na utaratibu huo uwe wazi na haki kabisa? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Asha Abdalla Juma, Mbunge wa Viti Maalum kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfumo ambao tunao sasa hivi wa upandishwaji askari vyeo uko vizuri; na nimeeleza katika jibu la msingi vigezo ambavyo vinatumika. Hata hivyo kulingana na wingi wa askari tuliokuwano na uchache na ufinyu wa nafasi hizo inasababisha wakati mwingine askari wengine kutumia muda mrefu zaidi katika kupata vyeo.

Hata hivyo tumekuwa tukifanya jitihada mbalimbali kuhakikisha kwamba wale askari ambao wanatimiza vigezo wanapata fursa ya kupandishwa vyeo; kwa hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Asha Abdalla Juma kuhusiana na hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na hoja yake, kama nitakuwa nimemuelewa vizuri, ya kuwafidia, nadhani hilo halipo katika utaratibu. Kimsingi tu ni kwamba tutaendelea kuhakikisha tu kwamba askari ambao wenye sifa wanapandishwa vyeo. Katika kipindi cha mwaka huu mmoja, hivi karibuni tulipandisha vyeo askari kwa upande wa Jeshi la Polisi pekee kwa haraka haraka nadhani ni zaidi ya askari 9000 ukiachilia mbali majeshi mengine yaliyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Utaona kwamba tunafanya jitihada kama Serikali kuona askari hawa ambao wanafanyakazi vizuri wanapata fursa ya kupandishwa vyeo kadri ya hali na uwezo wa Serikali unavyoruhusu.

**SPIKA:** Tunahamia Wizara ya Elimu, swali la Mheshimiwa Joyce Sokombi; uliza swali lako Mheshimiwa Sokombi.

Na. 69

**Chuo Kikuu cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere Kuwa na Majengo Yake**

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI** aliuliza:-

Kutokana na gharama za pango kuwa kubwa na hivyo kuongeza gharama za uendeshaji kwa Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere kilichopo Mkoani Mara:-

Je, ni lini Serikali itakijengea chuo hicho majengo yake na kuanza kuyatumia rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayani na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kuanzisha Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius Nyerere



Wilayani Butiama kama sehemu ya kumuenzi Baba wa Taifa ambaye aliamini katika umuhimu wa sekta ya kilimo kama uti wa mgongo katika ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia kimeendelea kufanya shughuli zake kwa muda katika majengo ya Shule ya Sekondari ya Oswald Mang'ombe iliyopo Wilaya ya Butiama.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendeleana ujenzi wa majengo ya chuo (*Campus Kuu*) ambapo kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania (*TEA*) ujenzi wa jengo la utawala lenye thamani ya shilingi milioni 200 umefikia asilimia 50. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kiasi cha shilingi bilioni moja kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mingine. Vilevile, Serikali inaendelea na juhudi za kupata fedha zaidi kutoka vyanzo vingine kama vile miradi ya Benki ya Dunia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sokombi, nimekuona.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua, Butiama ni sehemu ambako kila mtu anaelewa Butiama ni nani ametokea kule. Aliyetokea kule ni Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, na chuo hiki kina umuhimu mkubwa sana, na tunajua kabisa kilimo ni uti wa mgongo, na vijana wengi sasa hivi wanakimbilia kujajiri kwenye kilimo. Nataka kujua ni lini Serikali itatenga pesa za kutosha ili chuo hiki kiweze kukamilika badala ya kutegemea pesa au vyanzo kutoka Benki ya Dunia; ukizingatia Serikali haina ajira za kutosha kwa vijana?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Mheshimiwa Waziri anasema ujenzi wa majengo umekamilika kwa asilimia 50. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutembelea chuo kile ilia pate uhakika kama kweli zimefika asilimia 50? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya mswali hayo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sokombi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi; ni kutokana na nia ya dhati ya Serikali ya kumuenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ndiyo maana tumeamua kuanzisha Chuo cha Kilimo na Teknolojia Butiama. Hata hivyo, kama nilivyosema, kumekuwepo na changamoto kiodgo kwenye suala la upatikanaji wa ardhi. Hata pale kwenye shule ya Oswald Mang'ombe Serikali bado haijapata hati kwasababu Mheshimiwa Nimrod Mkono ambaye ndiye aliitoa kwa Serikali bado kuna michakato inaendelea. Hata hapo tunapojenga sasacampus kuu katika kituo cha uhamilishaji cha Butiama bado kuna changamoto ya radhi;na ni vigumu Serikali kuweka fedha nyingi kwenye eneo ambalo bado hati yake haijapatikana.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema, Serikali tayari imeshatenga shilingi bilioni moja kwenye bajeti ambayo tunaitekeleza sasa. Kwahiyoni matumaini yetu kwamba masuala ya radhi yakishakamilika, Wizara na chuo kikishakuwana hati inakuwa ni rahisi kuweka fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo tayari tumeshatoa shilingi milioni 200 angalau kuanza ujenzi;kama tunavyosema juu ya majengo yale, hasa jengo la utawala ambalo linajengwa kwa fedha za TEA limefikia asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ombi la Mheshimiwa Mbunge; kwamba,je, niko tayari kwenda Butiama na kuhakikisha kama ni kweli imafikia asilimia 50? Sina shida kuamabata na Mheshimiwa Sokombi tena nitakwenda kwa furaha sana ili tukaangalie kama jengo hilo kweli limefikia asilimia 50.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Makilagi nilikuona, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri inayoendelea ya kujenga hiki Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, mawazo ambayo mwenyewe aliyaasisi na yakapokelewa na Mbunge wetu Mheshimiwa Mkono ambaye alitoa hata maeneo ningependa kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, kutokana na changamoto ya radhi, Serikali ilishajipanga na tukaainisha maeneo kupitia kikao cha RCC Mkoa wa Mara, kwamba kuna majengo ambayo yapo katika Chuo cha Kisangwa-Bunda na kuna majengo mengine ambayo yako katika Chuo cha Shirati, na kuna majengo ambayo yako katika Chuo cha Wananchi-Bweri; na yale majengo yaliyopo yanaweza hata kupokea watoto.

Ningependa kujua, kwa kuwa Serikali bado inaendelea na mchakato na kwa kuwa pale kuna wafanyakazi sasa ni takribani miaka mitatu hawana kazi ya maana ya kufanya, ni lini sasa Serikali itawapanga watoto waende kuanzisha masomo pale wakati tukisubiria sasa fedha nyingi kwa ajili ya kuongeza majengo na maeneo mengine, ikiwa ni hatua muhimu sana ya kujenga mawazo ya Baba wa Taifa ambaye kwa kweli alijitoa, alitoa mpaka eneo, alijenga mpaka na Bwawa la umwagiliaji ambalo wananchi wameendelea kulilinda kwa muda mrefu sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina kwahiyo unapendekeza ihamishwe Butiama iende Bunda...

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Inabaki pale pale...

**SPIKA:** ...na huko ulikotaja; hebu weka vizuri swali lako.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yaliyokuwepo ni kwamba chuo kitaanzia pale na watoto watakuwa pale na majengo ya kusomea yapo, watakapokuwa...

**SPIKA:** Pale una maana ya Butiama?

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** ...ni Butiama ila wanapkwenda *field* kwa ajili ya masomo kwa vitendo kuna maeneo mengine ambayo yako ambapo wangekwenda kufanya *practice*.

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Makilagi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na mapendekezo mbalimbali ya namna ya kuanzachuo kile wakati tunasubiri ujenzi uanze. Hata hivyo Wizara imekuwa ikiangalia vilevile athari ambayo inaweza ikatokea kama tutatumia majengo ya vyuo vilivyopo ambavyo navyo vina umuhimu Kitaifa katika chuo ambacho tunaanzisha. Kwahiyo busara ambayo sisi tumeifikia ni kwamba hatuna haraka sana tusije tukavuruga utaratibu uliopo kwenye vyuo vingine kama hivyo anavyotaja lakini tsubiri mpaka hiki tuanze kujenga.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuhisiana na maeneo ya kufanya mazoezi, kwasababu Chuo kile sehemu kubwa itakuwa ni kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kuweza kufanya mafunzo mafupi ya kilimo, Wizara inaendelea kutafuta ardhi katika maeneo ya jirani ikiwemo pamoja na Wilaya ya Serengeti ili tuweze kuwa na sehemu ya kufanyia mazoezi. Kwahiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ya Serikali iko pale pale, chuo kile kitaanza na naomba wavute subira, lakini naomba wote kwa ujumla wao tusaidiane kuondoa changamoto za upatikanaji wa

ardhi pale kwenye Chuo cha Uhamilishaji lakini vilevile katika kuweza kupata eneo lile la Oswald Mang'ombe tuweze kupata hati ili hatimae chuo kiweze kumiliki.

**SPIKA:** Wabunge wa huko shughulikieni hati hiyo ndiyo changamoto. Swali la mwisho la leo Waheshimiwa kwasababu ya muda, Mheshimiwa Mabula Shing'oma.

Na. 70

### **Urasimishaji Katika Jiji la Mwanza**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Serikali imeruhusu urasimishaji wa makazi katika maeneo mbalimbali Nchini ikiwemo Jiji la Mwanza isipokuwa maeneo ya Kata ya Isamilo, Mbugani, Mabatini na Igogo.

Je, ni lini Serikali itawamilikisha wananchi hawa maeneo yao kwa kuwa wameishi katika maeneo haya kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stanlaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na zoezi la urasimishaji wa makaziyasiyopangwa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni utekelezaji wa kifungu namba 6.4.1(iii) cha Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 ambacho kinatamka kwamba;

“Maeneo ya makazi holela isipokuwa yale yaliyojengwa kwenye maeneo ya hatarishi hayatabomolewa bali yataboreshwa na kuwekewa huduma za msingi”.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jiji la Mwanza urasimishaji wa makazi unafanyika katika kata mbalimbali zikiwemo Kata za Isamilo na Mbugani. Katika Kata ya Isamilo urasimishaji umefanyika katika Mitaa ya Msikiti, SDA pamoja na National ambapo michoro ya mipangomiji miwili yenye jumla ya viwanja 3,444 imeandaliwa, viwanja 560 vimepimwa na viwanja 101 tayari vimemilikishwa. Aidha, Katika Kata ya Mbugani urasimishaji umefanyika katika Mitaa ya Nyashana na Kasulu ambapo michoro miwili ya mipangomiji yenye jumla ya viwanja 1001 iliandaliwa na viwanja 395 vimepimwa na vipo katika hatua ya umilikishaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufanyika urasimishaji katika mitaa hiyo, maeneo mengine ya kata za Isamilo, Mbugani, Igogo na Mabatini hayajafanyiwa urasimishaji wa makazi kutokana na sehemu kubwa ya maeneo hayo kuwa hatarishi; ambayo yapo kwenye milima yenye miteremko mikali zaidi ya asilimia 15. Hivyo maeneo hayo hayakidhi vigezo vya kurasimishwa kwa kuwa ni hatarishi kwa maisha ya wananchi na mali zao pamoja na ugumu wa kuyafikika kwa barabara.

Mheshimiwa Spika, Mpango Kabambe wa Jiji la Mwanza 2015/2035 umeainishabaadhi ya maeneo ya Kata za Mbugani, Isamilo, Pamba, Nyamagana, Mkuyuni na Igogo kuwa ni maeneo yanayotakiwa kuendelezwa upya (*redevelopment*) kwa kuzingatia hali halisi ya miinuko na ujenzi hatarishi uliofanyika. Kwa sasa wamiliki wamakazi hayo watatambuliwa na kupatiwa leseni za makazi (*formalization*) wakati wakisubiri uendelezwaji mpya wa maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula Mbunge wa Nyamagana, nimekuona.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Naibu Waziri pamoja na Waziri kupitia Wizara ya Ardhi kwa kazi kubwa ambayo kwa kweli katika suala zima la urasimishaji makazi wamejitahidi.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu kubwa ilikuwa ni namna gani wakazi hawa walioko kwenye maeneo ya milima watapatiwa nafuu kubwa hasa angalau kwa kutambulika. Sasa niishukuru Serikali kwasababu imeliona hili na kulifanyiakazi; ni jambo jema sana na mimi nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inaendelea na utaratibu wa urasimishaji wa makazi, na tunafahamu kwamba ili urasimishaji makazi yako maeneo ambayo yalikuwa na michoro ambayo ilikuwa na maeneo mbalimbali. Kwa mfano, maeneo kwa ajili ya maziko, kwa maana ya Makaburi; Serikali ina mpango gani sasa? Maana kumekuwa na mgogoro mkubwa, kwamba eneo lilitengwa kwa ajili ya makaburi lakini linakuta wananchi wameshajenga sana kwasababu halikulindwa na badala yake wanalazimika aidha sasa tuamue wananchi waondoke tubakishe eneo kwa ajili ya makaburi au wananchi wabaki ili tutafute eneo lingine la makaburi. Maeneo ya kule Sawa, Mwalukila pamoja na Igwambiti liko tatizo la namna hii; na namshukuru Waziri amefanya jitihada kubwa amefika kule.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili; ili uweze kupima na kupanga unahitaji fedha na Serikali imekuwa na utaratibu wa kutoa fedha kwenye halmashauri zetu kama mkopo. Sisi kama Wilaya ya Nyamagana, Jiji la Mwanza tulishaomba fedha na mikataba yote ikafungwa kwa ajili ya kupata fedha bahati mbaya sana hatujapata fedha hizi mpaka leo ni nini kauli ya Mheshimiwa Waziri? Ni lini tutapata fedha hizi hizi ili tupime na kupanga maeneo ambayo tunadhani yanaweza kuingizia Serikali na Halmashauri mapato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ili uweze kupima na kupanga unahitaji fedha na Serikali imekuwa na utaratibu wa kutoa fedha kwenye Halmashauri zetu kama mkopo.

Sisi kama Wilaya ya Nyamagana, Jiji la Mwanza tulishaomba fedha na mikataba yote ikafungwa kwa ajili ya kupata fedha bahati mbaya sana hatujapata fedha hizi mpaka leo. Ni nini kauli ya Mheshimiwa Waziri kwamba lini tutapata fedha hizi ili tupime na kupanga maeneo ambayo tunadhani yanaweza kuiingizia Serikali na Halmashauri mapato? (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mabula. Majibu ya maswali hayo kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Stanslaus Mabula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mabula kwa namna ambavyo amekuwa akipigania watu wake kwa ajili ya kurasimishiwa maeneo. Wote kama mnavyojua, Mji wa Mwanza umezungukwa na milima usipokuwa makini unaweza ukapata ajali kwa ajili ya watu pengine kuporomekewa mawe na kadhalika lakini amekuwa mvumilivu, amefuatilia na kuhakikisha kwamba taratibu zilizopangwa na Serikali zinafuatwa, namshukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali yake mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anazungumzia habari ya maeneo ya maziko ambayo tayari yameshavamiwa na ni kweli nilitembelea katika eneo lile nikakuta sehemu kubwa ya eneo lililokuwa limetengwa kwa ajili ya maziko limevamiwa na watu. Nitoe rai kwa Halmashauri zote kusimamia maeneo haya kwa sababu tunapanga maeneo hatuyasimamii matokeo yake watu wanavamia halafu kuwatoa inakuwa ni kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini katika eneo alilolisema kwenye Kata ya Sawa, kuna maeneo ambayo yako wazi



kidogo ambayo hayajavamiwa na kama wako watu hawazidi watano, bado tunaweza tukafanya mabadiliko katika ramani ya eneo lile ili watu wakapangwa kwenye maeneo yale wakaendelea na maisha yao halafu sehemu ya maziko nayo ikapatikana kwa sababu huduma zote tunazihitaji. Kwa hiyo, hilo ni suala la kumuelekeza Mkurugenzi wa Mipango Miji aweze kusimamia shughuli hiyo ili upangaji ufanyike upya katika eneo lile tupate eneo la maziko na watu warasimishiwe maeneo yale waweze kuishi kwa amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anazungumzia suala la Halmashauri kuwezesha ili waweze kupata pesa za upimaji. Napenda tu nitoe taarifa kwenye Bunge lako, Wizara ilitoa zaidi ya shilingi bilioni 6.2 katika Halmashauri zipatazo 24 kwa ajili ya kuwapa mkopo usio na riba ili waweze kupima na kurejesha na wengine waweze kupewa. Nasikitika kusema kati ya Halmashauri 24, ni Halmashauri tatu tu ambazo zimeanza kurejesha mikopo yake. Kati ya hizo shilingi bilioni 6.2 ni shilingi milioni 906 ndiyo zimerejeshwa ambapo Halmashauri ya Ilemela imerejesha shilingi milioni 800 kati ya shilingi bilioni 1.5 iliyopewa; Halmashauri ya Ukerewe imerejesha shilingi milioni 20 kati ya shilingi milioni 73 na Halmashauri nyingine ambazo zimepelekewa bado hazijarejesha mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai ili na wengine waweze kufaidika na pesa hiyo tunaomba sana Halmashauri hizi waweze kurejesha pesa hizo ili wale wengine waweze kupata. Sifa ni moja tu, ni kuandika andiko ambapo utaonesha mchanganuo mzuri namna utakavyofanya upimaji wako, utakavyolipa fidia na utakavyorejesha mkopo. Kwa hiyo, ni kitu kidogo tu watu wanafahamu wafanye kazi hiyo na Wizara itapokea lakini kwa kusubiri pesa zirejeshwe.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi kwamba muda hauko upande wetu, sasa tusonge mbele. Tutaendelea na uchangiaji wetu baadaye kidogo.

Ningewaomba sana Waheshimiwa Mawaziri kama una udhuru basi angalau kama una msaidizi akawepo. Haipendezi kabisa Wizara nzima watu wanakuwa hawapo. Kawaida ya Mabunge yetu yaani Bunge ndiyo *priority* namba moja wakati Bunge liko kwenye *session* mambo mengine yote huwa ni *priority* inayofuata. Kwa hiyo, itakuwa haipendezi kama Wabunge wanasafiri kutoka huko kuja kuzungumza kwa niaba ya wananchi halafu baadhi ya Mawaziri wanakuwa hawapo. Nawakumbusha tu.

Sasa nije kuhusu wageni, mtaona jukwaa langu leo limesheheni wageni wangu muhimu sana ambao napenda kuwatambulisha. Kwanza ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Charles Kichere. (*Makofi/Vigelegele*)

Karibu sana Bungeni. Hapa ni uwanja ambao tutakuwa nawe mara. Kwa mara ya kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote hawa nakuahidi kabisa kila aina ya ushirikiano. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wana matarajio makubwa sana nawe kupitia Kamati zao zote na kipekee zile Kamati za Fedha. Naamini baadaye saa saba tutaonana ili kuzungumza mawili matatu nikiwa na baadhi ya Wenyevitwa Kamati. Nikuhakikishie kwamba kwa upande wa Bunge sisi hatuna tatizo hata kidogo. Karibu sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Pia amefuatana na Mkaguzi wa Ufanisi, Ndugu Benjamin Mashauri. Ahsante na karibu sana. Hiyo ni timu ya CAG. (*Makofi*)

Wengine ni Mkaguzi wa Hesabu, Ndugu Jasphar Mero na Msaidizi wa Mkaguzi (Bunge), Ndugu Edwin Rweyemamu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Pia yupo Mkaguzi wa Serikali Kuu, Mwadawa Mgendela. Ahsante sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Yupo pia Mkaguzi wa Mashirika ya Umma, Ndugu Salhina Mkumba. Yuko Afisa Masuuli, Ndugu Omari Mkomwa, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine saba ambao ni wageni wangu ni Wabunge kwa maana ya Wajumbe wa Kamati ya Kilimo kutoka Bunge la Uganda na wameongozana na Maafisa wawili. Yuko Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo kutoka Uganda akiitwa Akugizibwe Lawrence, karibu sana. *(Makofi)*

Karibuni sana Wabunge wote kutoka Uganda ninyi ni majirani wapendwa. Mtakaporudi basi mumsalimie Spika Kadaga na mumpesalamu nyingi sana. *(Makofi)*

Bunge la Uganda waliandaa Mkutano Mkuu wa CPA ule wa *International* Septamba mwaka huu, kwa kweli waliandaa kwa kiwango cha juu sana. Nawapongeza sana, mtupelekee salamu. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Opondo Julius Mukasa; Ndugu Chemutai Evelyn; Ndugu Nanyondo Veronica; Ndugu Eceng Kenneth na Katibu wa Kamati Nadunga Esther. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wabunge wetu wa Uganda *I believe you have had some time to see how we run things here in Kiswahili and that it is very possible to run Parliament in Swahili. So this is one of the messages you have to take with you back to the Parliament of Uganda. All the best. (Makofi)*

Wageni watano wa Katibu wa Bunge ambao ni Maafisa kutoka *Senate* ya Kenya, Ndugu Njenga Ruge, Mkurugenzi; Ndugu Lawrence Amollo - Katibu Msaidizi Mwandamizi; Ndugu George Otieno - Katibu Msaidizi Mwanadamizi; Ndugu Angela Macharia - Katibu Msaidizi na Ndugu Lydia Nyagol - Katibu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa ni pamoja na wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa

Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoka Kituo cha Sanaa na Utamaduni kwa Viziwi Tanzania wakiongowwa na Mwenyekiti wao Ndugu Joseph Hiza. Wale kutoka eneo la viziwi, ahsanteni sana na karibuni sana ndugu zetu. *(Makofi)*

Wageni 57 wa Mheshimiwa Fakharia Khamis ambao ni Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Zanzibar wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT wa Mkoa, Ndugu Ghanima Mbawara na mtoto wake Ndugu Asha Daud. Karibuni sana UWT Zanzibar, mnaona walivypendeza jamani? Karibuni sana. *(Makofi/Kigelegele)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Justin Monko ambao ni marafiki zake na wadau wa maendeleo kutoka Tanzania na Kenya wakiongozwa na Askofu Dkt. Christopher Masika. Wako pale wageni wetu. Mbarikiwe sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni walioko Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 100 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Dodoma. Dodoma Sekondari majirani zetu, ooh wanapendeza. Karibuni sana watoto wetu, hiyo ndiyo Dodoma Sekondari. Jirani zetu kabisa na Bunge hapa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Bunge *Sports Club* walikuwa na mchezo mwishoni mwa wiki wa mpira wa miguu ambapo timu yetu ilitoka sare na Watumishi Combania. Kwenye *netball Bunge Queens* walipata magoli 18, Watumishi Combania magoli 17. Tunaendelea kuwapongeza sana *Bunge Sports Club*. *(Makofi)*

Mtakumbuka tulitangaza kwamba kutakuwa na zoezi la kulenga shabaha kule Makutupora JKT, Kikosi cha Jeshi 834. Matokeo ya mazoezi haya yalikuwa kama ifuatavyo. Aliyekuwa wa kwanza kabisa ambaye naomba mumpigie makofi, mlenga shabaha hatari kabisa yaani huyu alipiga akapata maksi 68 ni Mheshimiwa Profesa Adelardus Kilangi. Mheshimiwa Profesa kuanzia leo tunakuogopa, tunakupigia *salute*. Muwe mnapita mbali jamani, ana

shabaha huyu hatari. Safari ijayo na mimi nitakwenda tuone kama utanizidi na walenga shabaha wengine safari ijayo tujiunge huko tukamshinde AG. *(Makofi/Kicheko)*

Wa pili ni Mheshimiwa Justin Monko alipata maksi 61. Wa tatu ni Mheshimiwa Zainab Katimba, yeye alipata maksi 50. Nawapongeza Wabunge wengine wote mlioenda kwenye kulenga shabaha akiwemo Katibu wetu wa Bunge, Ndugu Kagaigai. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo, sasa nataka tuendeleo.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara Mjini, bado una yale yale tu?

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, kidogo tu, kidogo tu.

**SPIKA:** Si usharuhusiwa rafiki yangu?

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, kidogo tu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafo yuko hapa ameshakuruhusu, watu wako wote waingie kwenye kilinge, mpambano sasa. *(Kicheko)*

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, bado.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafo kasema hakuna kuweka mpira kwapani. Haya nakupa dakika mbili.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, naomba busara yako iweze kutumika kwamba tuliomba hoja ya kuahirisha mjadala kwa Kanuni ya 69(1), kwa nini Bunge lisiahirishe mjadala unaoendelea tuweze kujadili suala la hatari kwa Taifa letu hili. Wewe ulitugiza kwamba tukuletee ushahidi na tuliwasilisha ushahidi kwenye Meza yako.

Mheshimiwa Spika, jana ni kweli Mheshimiwa Waziri ametoa ufafanuzi kidogo lakini bado kuna mambo ambayo katika ufafanuzi wake hajayataja. Kuna baadhi ya maeneo nchi nzima, kwa mfano, Wilaya ya Liwale, wagombea wa vyama vya upinzani wote walinyimwa fomu. Asilimia 99 ya wagombea wote Wilaya ya Liwale hawakupewa fomu. Pia kuna baadhi ya maeneo wagombea wetu walifungiwa ofisi, zile fomu walizopewa hawakuweza kuzirejesha kwa sababu wasimamizi wa uchaguzi walifunga ofisi na wakawakimbia wapinzani. Pia kuna baadhi ya maeneo Kamati za Siasa za Chama cha Mapinduzi zilikuwa zinawajazia watu fomu usiku ili ionekane kwamba wamejaza fomu mbilimbili ikiwemo Mtwara Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba busara yako iweze kutumika angalau tutenge dakika 30 kujadili suala hili kwa sababu mambo ya hatari yameshaanza kujitokeza huko ambayo yanaenda kuliahiribu Taifa letu hili. Suala hili ni nyeti na kubwa kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu, hatuwezi kujadili Mpango wakati hali ya amani haiko sawasawa kutokana na suala hili la uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja, Waheshimiwa Wabunge waweze kuniunga mkono.

**SPIKA:** Mheshimiwa, ngoja kidogo kwanza. Unachotaka Serikali ifafanue hapa ni nini hasa?

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, nachohitaji ni kwamba Mheshimiwa Jafo jana amezungumza...

**MBUNGE FULANI:** Muda, muda.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, alisema kwamba wale ambao walichukua fomu wote waweze kushiriki hata kama wameondolewa lakini kuna baadhi ya maeneo watu hawakuruhusiwa kurejesha fomu na watendaji. Pia kuna baadhi ya maeneo watu wamenyimwa zile fomu zenyewe, kwa mfao Wilaya ya Liwale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali langu, unaomba nini sasa yaani unataka nini?

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja Wabunge tujadili kwamba kwa nini imetokea hali hii ambayo ni mbaya kwa mustakabali wa Taifa letu. Nilikuwa naomba busara yako, nitoe hoja ili Wabunge waweze kujadili suala hili kwa sababu haioneshi mwisho mwema kama Taifa.

**SPIKA:** Unajua unajipotezea uelekeo kwa sababu mpaka sasa hivi hujaongea unapendekeza nini wewe mwenyewe, hata kama watajadili wengine lakini wewe ulikuwa unapendekeza nini? Unatuelezea historia tu, kuna mtu sijui alifungiwa mlango, kuna mtu alifanya nini lakini sasa hapa unataka nini?

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nakihitaji ni kwamba yale manyanga yote ambayo yamefanyika kwa makusudi kwa mfano kuwanyima wapinzani fomu ambapo nimetoa mfano wa baadhi ya maeneo lakini pia kuna wagombea wetu ambao fomu zao zimekataliwa, naomba Mheshimiwa Jafo azungumze kinagaubaga kwamba wale watu na manyanga yaliyofanyika Serikali inatoa kauli gani juu ya hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, sijui kama umemsikia na kumuelewa Mheshimiwa japo amechukua muda mrefu lakini basi kama una la kusema, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Maftaha.

Sisi wote ni Watanzania, inawezekana tunatofautiana nia zetu ndani ya mioyo yetu. Hili ndilo jambo moja kubwa sana. Kwa ufafanuzi niliutoa jana na kusema kwamba watu wote waliochukua na kurudisha fomu, hii ilikuwa ni hoja watu wanasema hatuendi kushiriki kwa sababu watu wengi wamekatwa, sasa tunasema watu wote wawe uwanjani watu waende wakacheze demokrasia ifanye kazi leo hii tunahamisha goli tena.

Mheshimiwa Spika, sina *comment* zaidi ya hiyo kwamba kama kuna watu kweli wanamuogopa Mwenyezi Mungu na siku wataenda kujibu haki mbele ya Mwenyezi Mungu, nadhani kwa hekima iliyofanyika ni binadamu na Watanzania wachache wenyewe watatafsiri nini nia ya Watanzania hao.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, jambo langu ni hilo tu kama kweli watu wana hofu ya Mungu walikuwa wanasema kwamba fomu watu wamekatwa, bahati nzuri tumesema majina yao yarudi wakagombanie lakini bado watu wanahamisha goli, *I have no more comment. (Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ufafanuzi.

**SPIKA:** Ufafanuzi wa nini? Hukusimama mwanzoni. Ufafanuzi kanuni ipi? Maana aliyesimama peke yake alikuwa Maftaha peke yake, wengine wote hamkusimama. Kwa hiyo, kama mmejiorodhesha kwenye Mpango basi mtachangia, bado Kambi yenu sina jina hata moja, jiorodhesheni kwenye Mpango. Nitawapa nafasi mimi dakika 10, 10. Andikeni majina mtaniletea nitawapa nafasi, mtachangia. Katibu tuendelee.



**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Majadiliano yanaendelea. Waheshimiwa Wabunge, ili tuokoe muda sasa naomba tuendelee. Kama nilivyosema nileteeni majina kweli nitawapa nafasi, *I am not joking. Ooh*, nilishasahau haya mambo ya Meza hii. Kamati ya Mipango.

Waheshimiwa Wabunge naomba tukae, tunaanza uchangiaji mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Peter Serukamba na atafuatiwa na Mheshimiwa John Kadutu.

Kabla ya Mheshimiwa Peter Serukamba Waheshimiwa Wabunge nilipowatambulisha lile kundi la wenzetu viziwi kumbe yuko mtu maalum kabisa ambaye wamefuatana naye, bahati mbaya watu wangu hawakuwa wameniandikia ambaye ningeomba kumtambua, naomba Waheshimiwa tukae kidogo, hapo kwenye jukwaa la wageni naomba tukae. Katika kundi lile Waheshimiwa Wabunge yuko *Miss Word* ambaye ni kiziwi kutoka Tanzania ambaye alitwaa taji hilo Urusi mwaka huu, kule *Miss World* tafadhali, karibu sana, sana, karibu sana umelibeba Taifa letu, umetupatia sifa kubwa sana tunajivunia kuwa nawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Habari atatuambia hata kama ni baadaye kama kuna namna Waheshimiwa Mawaziri mtakapotoka hapo nje mjaribu kupiga naye picha na kadhalika aondoke akiwa na kumbukumbu za hapa Bungeni, ahsante sana na Waheshimiwa Wabunge pia. Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye Mpamgo wa Taifa wa mwaka 2020/2021. Kwanza naomba nimpongeze Waziri wa Fedha kwa kuja na mpango mzuri, leo nitatoa ushauri kwa badhi ya mambo. Nimeusoma mpango wetu, nashauri sasa nadhani umefika wakati kwenye mpango ningetamani tuoneshe mwaka kesho baada ya mwaka mmoja kama ambavyo tumesema tutajenga barabara, tunajenga madaraja, lakini nataka tuoneshe *production*, kwa sababu ili tuweze kupata fedha nyingi tuweze kuendelea cha kwanza lazima tuhakikishe *production* yetu kwenye mpango wetu ionekane na hapa nitatoa mfano kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tunakaa hapa tunapitisha Bajeti ya Kilimo, nadhani umefika wakati kwenye mpango basi tuseme kwa mfano kwenye kahawa; kwenye kahawa tunataka tuafanye kazi ili mwaka kesho tutoke kwenye tani 50,000 twende kwenye tani 200,000, lakini hili kwenye mipango yote haionekani na ndiyo maana kwa miaka yote minne kahawa haijawahi kuzidi tani 60,000, lakini wenzetu Uganda ni tani 2,88,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, twende kwenye chai; tunazalisha chai tani 19,000, tani 20,000 au 25,000; wenzetu Kenya hapa ambao sisi tuna ardhi zaidi, wanazalisha tani 350,000. Sasa lazima na sisi tunapokuwa tunapanga, tupange kwa kuweka matarajio, haiwezekani tunajadili tu kilimo, lakini tuweke *deliverables* ili tuweze kuwapima hawa wenzetu. Tukifanya vizuri kwenye kilimo nina hakika tutapata *export* nyingi, tutapata fedha za kigeni na kwa sababu hiyo *balance of payment* itaondoka kwenye *negative*. Tanzania kama nchi katika vitu ambavyo ni *advantage* kwetu cha kwanza tuna ardhi kubwa sana, Tanzania tuna maji mengi sana, Tanzania tuna mifugo, sasa kama tuna vitu vikubwa hivi vitatu, lakini zaidi ya hapo tuna jiografia ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tunapopanga tupange kuona ambavyo vitu hivi vitatu kwenye mifugo,

itatuletea nini baada ya mwaka mmoja, bada ya miaka mitano, hatuwezi kuwa tunasema kuwa ni wa pili Afrika tuna mifugo lakini ukienda kwenye mchango kwenye *GDP*, ukienda kwenye mchango wa pesa ya mmoja mmoja siyo kubwa. Tuna uvuvi, wenzetu tukienda kujifunza hata pale Namibia, wanafanya uvuvi mkubwa sana kwenye bahari kuu, sisi tuna eneo kubwa la bahari kuu lakini tujiulize maswali, mwaka huu tulivua kiasi gani mwaka kesho tutavua kiasi gani. Kama hatujiwekei namna ya kwamba mwaka huu tutoke hapa kwenda pale, tutakuwa kila siku tunajadiri tunamaliza mpango tunakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakuja na mawazo kwamba umefika wakati Wizara ya Fedha inapokuwa inapanga mpango tuwekeane, wakae na Mawaziri wasainiane mikataba kwamba tunataka kwenye kilimo, kwenye kahawa iwe hivi, kwenye katani iwe hivi, kwenye mkonge iwe hivi. Kwa mfano mkonge sasa hivi, una bei kubwa sana kwenye soko la dunia, lakini unajua tunazalisha tani ngapi? Tunazalisha tani 34.6 kwa mwaka, wakati ardhi tuliyonayo tunaweza tukazalisha tani milioni moja na hela hii ikaingia kwenye *economy*. Ardhi tuliyonayo tunaweza tukatoka, leo korosho inaleta fedha nyingi sana, lakini korosho ni tani ngapi, laki mbili, laki tatu, lakini uwezo tulionao tunaweza tukaenda tani milioni moja. Sielewe watu wanaopanga mipango yetu kwa nini hatujiwekei *target*, tukiweka target nina hakika tutafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haikuwa bahati mbaya kuwepo hapa ilipo, jiografia yetu lazima tuitumie kukuza uchumi; hatuwezi kuwa tunasema tuna amani, nchi imetulia, tuna jiografia nzuri, lakini inaleta nini, tuangalie tunafanye biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimelisema kila nilipoingia kwenye Bunge hili, ni suala la miradi ya *PPP*. Kwenye miradi ya *PPP* sielewi kuna ukakasi gani Serikalini, kwa sababu *PPP* wako watu wanasema tumeshajaribu *PPP* ukisikia inatajwa wanataja *TANESCO*, haikuwa *PPP* ilikuwa ni *management*, wanataja *RITES*, *RITES* haikuwa *PPP* ilikuwa

ni *management*, wanataja maji ya Dar es Salam *City Water*, hiyo haikuwa *PPP*, it was a *management*. *PPP* ni lazima mtu alete fedha, awekeze, azalishe, mgawane na mfano thabiti wa *PPP* ni daraja la Kigamboni, tumefanya, Serikali na *NSSF* na watu wanalipa pale, lakini wananchi hawajazuiliwa kwenda kupanda pantone, mwenye haraka ataenda kwenye daraja. Tukifanya hivi tuta-*leverage* haya tunayofanya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano, leo Mheshimiwa Rais anafanya miradi mikubwa sana mmoja ukiwepo mradi wa maji wa Nyerere wa Rufiji, jambo jema, jambo nzuri sana. Hata hivyo, lakini ukisoma sera ya Tanzania ya mwaka 2003 sera ya *energy* inasema *energy mix* maana yake nini? Tuna *geothermal*, tuna upepo, tuna gesi, tuna makaa ya mawe, mpango wetu unasemaje? Kama hatuna fedha kwa sababu tunafanya kwenye maji tutafute watu wafanye, wakifanya tutagawana zile fedha na Tanzania tutapata umeme mwingi. Nataka niwaambie leo wenzangu umeme ni bidhaa, umeme ni biashara, nina hakika tukizalisha umeme mwingi tutauza Kenya, tutauza Uganda, tutauza Rwanda, Burundi, Kongo, Zambia na Malawi, tunaweza, lakini hatuwezi kuyafanya yote kwa wakati mmoja lazima mengine yafanywe na *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo barabara, tumekalia tunataka kila kitu kijengwe na Serikali, wewe umetembea duniani barabara za *express way* zipo; hivi tunaona tabu gani kujenga *express way* ya Dodoma Dar es Salam halafu hii barabara ya zamani iendelee kuwepo mwenye haraka atakwenda kwenye kulipia, wako watu wanakuja na hoja kwamba tunajenga *SGR* hakuna ya barabara siyo kweli hata kidogo, nenda China *bigger as it is population one point four billion people* wanajenga mabarabara, wanajenga reli yanaenda kwa kasi, reli haiwezi kuchukua nafasi ya barabara, wala haiwezi kuchukua nafasi ya ndege, vyote tunavihitaji kama Taifa. Ili mtu akitoka hapa aende Mwanza haraka, akitaka aende taratibu kuna barabara hii atakutana na ma *Traffic*, hii ya haraka atalipa, shida iko wapi? Leo wenzetu Uganda kutoka Entebbe kuja

Kampala wamejenga express way, maana yake kule watu watalipia, lakini ile barabara ya zamani itaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe wenzangu *PPP* ni lazima, ndiyo *way to go* kama nchi. Kama na kwa sababu *PPP* itatusaidia, leo Serikali inajenga sana hospitali kila mkoa, kila wilaya, hivi tunaona tabu gani kuingia *PPP* mtu akaleta vifaa; kwamba vifaa vile yeye ndiyo anahangaika na vifaa, teknolojia ikibalika atalipisha yeye, kinachotokea yeye anaweka hela zake. Kwa hiyo maana yake tunaweza tukajenga hospitali nyingi zaidi kwa sababu vifaa ni gharama, lakini *somebody yes will do it for us*. Kwa nini wenzetu hawataki kuhangaika na *PPP*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee miradi mitatu, ukisoma kwenye Mpango haitajwi sawasawa. Mradi wa kwanza ni wa *LNG plant* wa gesi kule Lindi, Mradi wa pili ni Mchuchuma na Mradi wa tatu ni Engaruka. Nataka wenzangu tuelewane miradi hii mitatu leo ingekuwa inatekelezwa ni zaidi ya bilioni 40 zingekuwa kwenye *economy* yetu. Leo Tanzania kila mtu angekuwa ana kazi, leo Tanzania shilingi yetu ingekuwa na thamani kwa sababu kuna dola nyingi zingekuja *in our economy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Msumbiji muuza hata *toilet paper* ni tajiri pale Msumbiji kwa sababu ya Mradi wa *LNG*, watu watasema tatizo ni mikitaba, mimi nasema mikataba kwa Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Magufuli itakuwa mizuri tu, kwa nini tusi-*negotiate*, hatuwezi kuwa tunakaa tunasema tatizo letu ni mikataba mibaya, hapana, mikataba tuisahihishe mbona mkataba wa *Barrick* tumeubadilisha. Tunaogopa nini ku-*negotiate* vizuri na haraka kwenye *LNG*, huku kwenye Mchuchuma huku kwenye Engaruka, tunaogopa nini? Tatizo ni nini na hatutumii fedha zetu *somebody* yeye si analeta pesa. Pia kinachotokea tukitekeleza hii miradi, mradi wa *PPP* wa reli kutoka Mtwara kwenda huku Liganga utawezekana, lakini kama Liganga haiwezekani hiyo reli haitokuwepo. Hata Mradi wa Bagamoyo tukiamua kufanya hii miradi tuka-

*renegotiate* upya, tuwaondoe wale wezi tulete watu wazuri, hii miradi tunaitaji kwenye hii *economy*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mambo mawili makubwa; naomba sana wenzetu mpango wetu lazima uje na mambo makubwa mawili, lazima mpango uwe *clearly* kwenye *job creation*, mpango lazima uwe *clearly* kwenye *foreign currency* tunazipata wapi, kwa maana *exports*, kwa sababu kama hatutengenezi *jobs*, tunasomesha kila siku hizo kazi zitatoka wapi? Lazima *PPP* ndiyo ije na ili *PPP* ije mambo mawili yafanyike; moja, lazima tuangalie sheria zetu upya, tuweke *legal framework* yenye *clarity*, pia tuhangaika na education kwa maana kuandaa *skills* zitazofanya kazi kwenye hivyo viwanda vipya, kwenye hiyo miradi mikubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale mnaojua *trend* ya dunia, *trend* ya duni sasa hivi kule China gharama za kazi zimeanza kupanda kwa sababu wanakwenda *first world*; Asia, India gharama za kazi zinapanda maana yake ni nini? Wanakuja Afrika lakini watakakokuwa wamejiandaa, ndiyo maana leo unaanza kuona viwanda vikubwa vinatoka China vinakuja Ethiopia kwa sababu wamejiandaa, wameweka mazingira wezeshi na kwa kufanya vile wanapata *jobs*, wanapata *technological transfer*, pia *above all* wanaweza kupata hela za *exports*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanawezekana, naamini tukiamua haya yanawezekana, naomba mpango wetu uhangaike na haya mambo, kwangu mimi ni makubwa sana. Niseme, umefika wakati siyo vibaya *copy* vitu vizuri, ukisoma historia nchi zote zilizoendelea miaka ya 60; China, India, Singapore, Malaysia, South Korea, vitu vitatu vimewapeleka haraka sana. Cha kwanza wame-*embrace free market* na *free trade*, wameweka tu *governance* ya kuhakikisha inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili ni *pragmatism*, hii *means* yake *what*? Maana yake ni kwamba, hutojali kama

huyo paka ni mweusi ama ni mweupe, cha msingi akamate panya tu. Kama mtu anaweza akaja akajenga barabara, *express way* kwa hela zake, shida yetu nini? Mtu akishajenga barabara hawezi kuibeba akaondoka nayo, mtu akija akawekeza *LNG plant* hawezi ku-*assemble* akaondoka nayo haiwezekani, lakini pia lazima tuanze ku-*impress meritocracy*, tuanze kuhangaika na watu wenye maarifa, tutengeneze Taifa ili lihangaika na watu wenye maarifa, tuweze kwenda haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kama Tanzania kipindi hiki cha Mheshimiwa Rais Magufuli, ni Rais anayefanya maamuzi, ni Rais mwenye nia ya kutaka kuleta maendeleo kwa kasi, ni jukumu letu sisi Wabunge na watu wa Serikali, tumsaidie aende kwa haraka. Haya anayoyafanya lazima yawe *leveraged* na kitu kingine na kwa sababu anafanya maamuzi haraka, naombeni Serikalini na ninyi mfanye maamuzi haraka. Nchi hii itaenda kwa kasi sana kwa sababu tuna kila kitu unachoweza kusema hapa duniani, tuna madini, tuna gesi, tuna *everything*, kwa hiyo mipango yetu iwe ya kusaidia kwenda haraka kwenye maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la, kuna kitu kimeletwa Serikalini Mheshimiwa Waziri Mkuu amekianzisha kinaitwa MTAKUWA. MTAKUWA ni utaratibu wa kuhangaika na kuondoa unyanyasaji wa akinamama na watoto ni *initiative* kama ilivyo *initiative* ya UKIMWI, lakini nimesoma mpango wote hawaongei chochote kuhusu MTAKUWA. Taifa lolote lenye heshima ni Taifa ambalo linajali haki za watoto, haki za akinamama na haki za jinsia yote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kwenye Mpango na bajeti ijayo kila Wizara ije na *gender budget statement*, tuoneshe tunavyojiandaa kuhangaika na mambo haya, huu ndio ustaarabu, hamwezi kuwa na Taifa la watu kila siku akinamama wananyanyaswa; watoto wananyanyaswa; ukiyasikiliza yanayotokea huko ndani, sio Taifa la Tanzania. Naombeni tukusanye nguvu za kifedha,

za mikakati, za kisheria, kuhangaika na unyanyasaji wa akinamama na watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba, umetuanzishia msingi mzuri sana wa kujadili Mpango, natumaini na wengine watapita katika nyayo hizo kwa sababu mawazo yenu ni muhimu sana. Kama kuna Mheshimiwa Mbunge ambaye unawiwa unaona kabisa una kitu na hukupata nafasi katika wiki hii nzima, wewe niandikie tu, mimi nitaangalia hapa kwenye meza yangu, nikipata dakika chache nitakupatia, kwa hiyo usikae ukajiona kama umekosa nafasi, wa chama chochote, wewe niandikie tu hapa mimi nitaangalia meza yangu inavyoenda.

Nakushukuru sana ulivyotukumbusha mambo ya Asia lakini pia rafiki zetu, ndugu zetu wa China wao wana kitu kinaitwa *reform and opening up* ndio iliyowasaidia Wachina, *refrom and opening up*, ndio maana kila wakati tukikaa hapa tunamwambia Mheshimiwa Angela Kairuki tulettee *blue print* tunaamini kabisa huenda itakapokuja itakuwa na *same element za reform and opening up, if we don't open* tunaendelea na ukiritimba tulionao hata tupange uchumi wetu utakuwa huu. *We have to open up*, maana tulikuwa na *close economy* kule nyuma na tulifunga sana, sasa ni lazima *to open up* na tufanye *reform* tuweze kwenda.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Peter. Mheshimiwa John Kadutu anafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate, halafu Mheshimiwa Katani jiandae.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kabla sijachangia niombe niseme maneno mawili, matatu, hasa ni shukurani. Nakushukuru wewe, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Katibu wa Bunge na Wakurugenzi wote pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa upendo ambao mlionesha wakati



nikiwa hospitali *ICU*. Ni jambo kubwa sana limefanyika kuokoa maisha yangu. Kwa hiyo nawashukuruni sana kwa moyo wa ukunjufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili tu, la kwanza hili lililotokea na kukaa *ICU*. Tunazungumzia mipango hapa ukiniuliza sana nitakueleza labda ukiacha mkono wa Mungu ni vifaa pamoja na mabingwa walloweza kuokoa maisha yangu, sasa ni wakati muafaka Serikali imeshafanya mambo mengi sitaki kuyataja, imeshafanya mambo mengi, lakini sasa tujikite kuhakikisha watu wetu wanapata uhai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema, ukipelekwa Muhimbili ndugu zangu umepona. Muhimbili ya sasa sio kama zamani, wewe omba ufike *emergency* utaona jinsi gani madaktari mabingwa tena vijana watakapokufanyia kazi hapo mpaka ukafikishwa kama ni wa *ICU* au wa wadini unajua kabisa kwamba hiyo hospitali ina vifaa na ina wataalam, hivyo vitu ndio tunakosa mikoani. Badala ya kudhani kwamba kila siku... naogopa kidogo kuyataja mengine, tupeleke sasa pesa kwenye hospitali za mikoa ziwe na vifaa, ziwe na wataalamu ili watu waokolewe huko huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba mimi ningeweza kupona nikiwa Tabora lakini kama tutategemea tu hospitali moja ya Muhimbili maana yake maeneo mengine yote kwa sababu ukiacha bima nani atakuwa na uwezo wa kusafiri mpaka Muhimbili ni tatizo, nadhani hata wanaotibiwa nje watapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nadhani Serikali sasa iwe na uwamuzi tu wa makusudi, hizi *MRI* zikipelekwa kila mkoa watamalizana huko *CT-Scan* nini watu watapona. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali na bwana Mipango jaribuni kuliona hilo ili kuokoa maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuchukua muda mrefu, la pili ni maji. Maji limekuwa tatizo na haya maji

tunazungumzia maji ya Ziwa Victoria tu. Hivi wataalam wana mipango, wanashindwa kutupatia mbinu mbadala au vyanzo vya maji vingine, hivi kama tunaweza kukinga Rufiji tukapata umeme huku mikoa mingine hatuwezi kukinga maji. Kwa mfano Mkoa wa Tabora maji yako mbali sana chini, ndio maana shida ya maji ipo kila siku, matokeo yake tutazozana mimi hamjanipangia sijui lakini maji ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumeweza kwenye umeme kwa nini maji tusiweze lakini shughuli ya maji inakwenda polepole sana. Kwa hiyo, nilikuwa nawashauri hebu na kwenye maji tujaribu kupaona pakoje ili watu wetu waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho tunapanga mipango hapa huku tukijua mapato yetu yatakuwaje. Leo hii tumbaku makampuni yanaondoka na kwa utaratibu wa kilimo cha tumbaku mpaka upewe makisio usipopewa makisio huruhusiwi kulima. Eneo kubwa kwa mfano tunakolima tumbaku Lyakulu wapi na wapi hawajapewa makisio na makampuni yanaondoka maana yake hiyo mipango tuliyopanga kama kulikuwa na pesa ya tumbaku hatutaipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri Serikali hivi imeshindwa na hawa wazungu wa tumbaku mbona wa korosho wanaweza. Tumbaku tu ndio imekuwa shida, hiyo mipango kama imepangwa na hela ya tumbaku imo nataka nikwambie kwamba tumbaku itakuwa kidogo sana na maeneo ambayo yanalima tumbaku sana hayatakuwa na tumbaku. Mojawapo huko Lyankulu kampuni zinaondoka lakini Serikali imeshindwa majadiliano na hawa watu! Lakini unasikia kabisa wanaenda jirani, wanaenda Zimbabwe manake sisi mipango yetu kwenye kilimo hiki cha tumbaku haiku vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena nakushukuru sana na uongozi mzima kwa yale mliyonifanyia na nina imani kabisa nisingeweza kutoka ICU kurudi Bungeni, ningekuja hapa nikiwa ndani ya sanduku ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa John Kadutu, Mungu ni mwema siku zote tunawashukuru sana pia kwa niaba yako madaktari wote kuanzia kule Tabora pia Muhimbili na kwa mpango wetu wa Bima ya Afya tuliweza mku-*airlift* Mheshimiwa Kadutu ndio tukaweza kuokoa maisha yake. Kwa hiyo tunashukuru sana, nilikuwa nataka kuwaambia watu wa kilimo tumbaku anayoisemea hii ya Zimbabwe China wananunua tumbaku yote ya Zimbabwe *let us work with China*, tufanye kazi na China. Dunia ya leo usipofanya kazi na China unapishana na gari la mshahara huo ndio ukweli, China ndio kila kitu, tunaweza kuuza korosho yote, tumbaku yote, pamba yote na kila kitu, kwa hiyo tujitahidi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, na hawa jamaa wamezoea kutudanganyadanganya na vikampuni vyao na nini wanatuzulumu miaka yote tuko nao lakini maneno ni hayo, sasa tujaribu upande hu pia. Pamoja na yote lakini ni *negotiation* tu mradi sisi tuwe kwenye *negotiation* tuweze kupata kile cha kwetu, tukizubaa kwenye *negotiation* tusilalamike na ndio umezubaa mwenyewe. Na sisi kwenye *negotiation* tuko wazuri kabisa kuliko wakati wowote mwingine kama Serikali kama nchi kwa hiyo tumesomesha vijana kila mahali *we are good*, nakushukuru sana Mheshimiwa Kadutu, Mheshimiwa Innocent Bilakwate atafatiwa na Mheshimiwa Katani na Mheshimiwa Dkt. Peter Kafumu ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi kuchangia kwenye mpango huu kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uhai na nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kutuletea mpango huu pia kwa ujasiri ambao ameendelea nao kusimama imara kuhakikisha anaisimamia wizara yetu inafanya vizuri kwa kweli tunampongeza hajatetereka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa maamuzi magumu ambayo amekuwa

akiyachukua kwenye mambo mbalimbali ambayo ameyafanya na watanzania wanaona kwa kweli tunampongeza sana tunaendelea kumwombea afya njema, Mwenyezi Mungu amlinde aweze kutimiza majukumu yake ya kuwatumikia watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuchangia kwenye mpango huu kuna mambo ambayo nitaishauri Serikali, nishauri upande wa miundombinu. Maeneo mengi ya uzalishaji ni vijijini tunaposema tunaingia kwenye Tanzania ya viwanda lazima tuangalie kule vijijini ambako tunategemea kuzalisha ambako kuna wakulima wengi zaidi ya asilimia 70 lakini ukija kwa upande wa miundombinu kama barabara kwa kweli Serikali pamoja na jitihada ambazo imekuwa ikionyesha lakini bado kuna maeneo mengi ambayo hayajafikiwa vizuri, mimi nitoe mfano kama kule kwangu Kyerwa, Kyerwa tunazalisha sana kwa mwaka sisi tunalima zaidi ya mara tatu lakini ukija kuangalia barabara zetu kwa kweli sio nzuri na ukienda upande wa pili kwa kweli ukaangalia barabara za wenzetu na ukaja kidogo kwenye upande wa Kyerwa kwa kweli inasikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri tuwekeze nguvu sana kwenye miundombinu ili hawa wakulima wanapozalisha mazao yao yaweze kufika sokoni kirahisi ndipo tutaweza kuinua kwanza kipato cha mkulima pia kuinua kipato cha Serikali. Kwa hiyo, niombe hilo Mheshimiwa Waziri uliangalie tunazo barabara zetu za Mgakorongo kwenda Murongo mpaka Uganda lakini tunayo barabara ya Mulushaka kwenda Nkwenda Murongo hizi ni barabara ambazo ni muhimu ukilinganisha na uzalishaji ambao tunaupata kule Kyerwa kwa hiyo niombe sana hilo tuliangalie hatuwezi tukasema tunaingia kwenye uchumi wa viwanda wakati miundombinu ambayo tunategemea kupata mazao yaje kwenye viwanda vyetu kama sio mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilizungumzie tunayo mazao yetu ya kimkakati tunategemea kuwa viwanda vingi lakini hivi viwanda lazima tuhakikishe

malighafi zinatoka hapa ndani kama tunataka kuinua uchumi wa Taifa lakini tukitegemea malighafi zinazotoka nje tutakuwa tunawanufaisha wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana nchi yetu Mungu ameibariki tunaweza kulima maeneo mengine kama nilivyosema kule kwetu tunalima mara tatu kwa mwaka sasa niombe sana tuwekeze sana kwenye kilimo. Tumekuwa tukiongelea suala la mazao ya kimkakati, kahawa na haya mazao mengine lakini hatuoni jitihada za Serikali kuongeza uzalishaji wa hizi kahawa. Kwa hiyo, niombe sana kwenye haya mazao ambayo ni ya kimkakati ambayo tunategemea yeweze kuleta malighafi kwenye viwanda vyetu kama hatujawekeza nguvu. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri hili uliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lilemee ni kwa upande wa afya, Pamoja na jitihada za Serikali kuwekeza kwenye vituo vya afya, kuwekeza kwenye hospitali lakini bado hatuna madaktari wa kutosha, tunategemea tuwe na madaktari tuwe na wataalam wa kutosha ili watanzania wawe na afya nzuri ndipo tutaweza kuwa na uzalishaji ambao ni mzuri. Kwa hiyo, niliombe sana Mheshimiwa Waziri hili mliangalie na muwekeze nguvu lakini pia pamoja na jitihada za Serikali tuna vituo vingi vya afya ambavyo vimeongezeka nchini pamoja na hospitali za Wilaya lakini bado vifaa havitoshi. Kwa hiyo, niombe sana hili la lenyewe tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ili tuweze kufika kwenye uchumi wa viwanda lazima tuwe na maji safi na salama kwa wananchi wetu. Wananchi wetu wanatumia muda mwingi kwenda kutafuta maji wakati mwingine masaa hata mawili, matatu lakini hakuna maji ambayo yanaweza kuwasaidia wananchi wetu waweze kuzalisha. Mwananchi ameondoka saa 11 ameenda kutafuta maji halafu unategemea atarudi saa nne aweze kwenda shambani kulima, na hao wakulima ndio tunaowategemea waweze kuzalisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeiti, kwa hiyo, niombe sana Serikali pamoja na jitihada zake niombe sana muendeleo kuwekeza upatikanaji wa maji safi na salama na nimwombe sana Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikikusumbua sana kwenye miradi ambayo iko kule Kyerwa tunao mradi wa vijiji 57 niombe sana miradi hii iangaliwe ili wananchi wetu ambao hawa tunategemea ndio wawe wazalishaji wakubwa kuinua uchumi wa Taifa letu waweze kuwa na muda mwingi wa kwenda kuzalisha kuliko kuwa na muda mwingi wa kwenda kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona sana huu mpango ni mzuri lakini haya mengine tukiyazingatia nimeongelea suala la maji, miundombinu, kilimo hivi vitu vikiangaliwa vizuri ninaamini tutapiga hatua kutoka hapa tulipo na uchumi wa Taifa letu utaongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru asante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Asante sana Innocent Bilakwate lakini leo Bilakwate umeongelea mambo ya jimbo peke yake bwana unatakiwa u-cover na nchi siku nyingine kidogo upanue wigo Tanzania inasogeaje zaidi najua *contribution* ya jimbo inasaida nchi lakini nafikiri umenielewa. Mheshimiwa Katani nilishakutaja, utafata Mheshimiwa Peter Kafumu

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema lakini nikushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi hii kuchangia mapendekezo ya mpango huu. Niende moja kwa moja kwenye suala la kilimo ambapo ndio pananigusa sana kwa sababu natoka sehemu ya kilimo. Ukisoma mapendekezo ya mpango ipo sehemu inazungumzia kujenga maghala kwenye mazao ya mpunga lakini niliwahi kutoa pendekezo mwaka jana na leo narudia tena wakati anachangia Mheshimiwa Musukuma alisema ipo miradi inapelekwa maeneo ambayo haina *return* binafsi nilimwelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo unajenga soko lakini *return* ya soko unalolijenga inarudi kwa muda gani, kuna eneo kama Tandahimba ambalo tunazungumza la korosho unashindwa kupeleka fedha ya kujenga ghala wakati kutunza korosho ghalani ni shilingi 38 kwa kilo moja. Yaani ukiwekeza bilioni 5 Tandahimba *return* yake kwa Serikali ni miaka miwili kama umewapa mkopo wanakuwa wamerejesha hiyo fedha. Lakini unapeleka kujenga soko sehemu ambayo hakuna hata wafanyabiashara wenyewe. Nilizungumza hizi mwaka jana na leo narudia tena kwenye huu mpango mnazungumza kujenga maghala ya mpunga kwenye kuhifadhi korosho ghalani shilingi 38.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tandahimba wakizalisha tani 74,000 kama walivyozalisha msimu iliyopita maana yake wanakusanya bilioni 2 na milioni mia nane na, ukipeleka fedha hii inaweza kurudisha kwa miaka miwili tu. Niwaombe kwenye mpango wenu muangalie *factor* hizi mupeleke fedha maeneo ambayo wanaweza kuzirejesha kwa wakati zikaenda kutawanywa maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo hapa nataka nilikumbushe sitaki kukumbusha yaliyopita lakini nikumbushe kwenye bajeti ya mwaka jana wakati tunabadilisha sheria ya fedha ile ya korosho sheria namba 203 ninukuu maelezo ya Waziri wa Fedha alisema " kufatia pendekezo hili shughuli za uendelezaji wa zao la korosho pamoja na gharama za uendeshaji wa bodi ya korosho zitagharamiwa kupitia bajeti ya Serikali chini ya usimamizi wa Wizara ya Kilimo kama inavyofanyika hivi sasa kwa mazao mengine ikiwemo pamba, kahawa na pareto." Jambo la kusikitisha tarehe 07 mwezi wa Kumi tulivyokuwa kwenye kikao cha wadau pale, bodi ya korosho na wizara imeleta mapendekezo kwa wadau ya mkulima kukatwa shilingi 25 kupeleka TARI Naliendele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima akatwe 25 kupelekwa Bodi ya Korosho, *OC* ya bodi ya korosho itozwe kwa mkulima na haya yalikuwa ni maelezo mazuri ya Waziri japo mwanzo tulikuwa tunafanya *argument* ya kukataa ile

15% kwamba ibaki bodi ya korosho lakini Serikali ilivyoshawishi tukakubali tukaona kabisa kwamba hiyo 15% ya *export levy* ambayo inapoinunua korosho leo 2700 maana yake kuna zaidi ya 380 na inakwenda kwenye mfuko mkuu, leo wanakatwa mkulima shilingi 50 inakwenda TARI ambayo mmeingia makubaliano na *Ox-farm* mnapata zaidi ya bilioni 70 leo mnakwenda kumnyonya mkulima huyu tena. Kikao kimekataa lakini wizara mnasema mmetumwa na wakubwa, wakubwa gani ambao hawana huruma na mkulima? Ni wakubwa gani ambao wamewatuma ambao hawana huruma na mkulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kwenye mapendekezo ya mpango mwaka jana mmezungumzia uzuri mara nyingi tunaenda mbele tunarudi nyuma. Ni mwaka juzi Waziri Mkuu alisimama hapa akasema kumwondolea mzigo mkulima anaondoa tozo tano, tozo tano leo zimerudi tena mkulima yupi anayesaidiwa Tanzania? Niombe sana kwenye mpango huu tunapotafakari mapendekezo ya mpango wa maendeleo tuguse maslahi ya watu kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani kuna taarifa, Mheshimiwa Naibu Waziri kifupi

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu nilitaka nimpe taarifa ndugu yangu Katani kwamba tozo hii imejadiliwa kwenye kikao cha wadau ni kwa mujibu wa sheria na hakukuwa na mkubwa yoyote aliyeongoza kile kikao, kikao kile kiliongozwa na wadau wa kilimo.

Kwa hiyo, hakuna maagizo kutoka kwa mkubwa yeyote. Kama kuna *any concern* kuhusu tozo hii, utaratibu upo wazi, kikao cha wadau kikae kifanye maamuzi. (*Makofi*)



**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani unapokea hiyo taarifa

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake lakini pia na wewe nataka upate uelewa pia. Wadau wanaozungumzwa ndio walikataa kwenye kikao na *clip* ya *audio* ya mazungumzo yale yapo hili ni jambo limeletwa na Serikali sio jambo ambalo wadau wamelipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unayo Mamlaka, unayo nafasi tukisubiri wadau tu, wadau ndio walileta baadhi ya sheria ambazo tunazibadilisha humu, wadau hao ndio wamekataa, huu ni mpango wa Serikali kutaka kumnyonya mkulima, tusitengeneze maneno mengine. Wabunge walikuwepo hao waulize wote tulikataa pale sasa hili ni jambo ambalo inawezekana ulikuwa hulijui, nimeamua niliweke hapa kwa sababu nimeona kwenye suala la mapendekezo ya mpango na hili lilizungumzwa na Serikali mwaka jana vizuri kwamba fedha za bodi zinatoka wapi, fedha za kuendeleza zinatoka wapi hao *TARI* wana bilioni 70, dola milioni 32 *ox-farm* wameshafikia makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unakwenda kwa mkulima huyu mnyonge na ninyi mawaziri mnajua kwamba tunatoka kwenye mazingira magumu mliangalie hili kwa namna pana sana wala halihitaji majibu ya mhemuko, linahitaji kufanyiwa kazi kwa kuwajali wakulima wa Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ana dhamira njema na wakulima. Waziri Mkuu ametoa tozo ambazo zimerudi hapa kwa namna nyingine, kwa mlango wa nyuma. Naomba sana, kwenye mapendekezo haya ya mpango mwangalie mambo ambayo yanaweza yakatupa tija kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, mimi natoka vijijini. Naendelea kuungana na wenzangu walioshauri, fedha zile zinazokwenda *TARURA* kwa kweli hazikidhi mahitaji. Mfano

mzuri, leo ukienda Jimboni kwangu ambako korosho zinatoka vijijini ili zifike bandarini pale, vijiji vile havipitiki. Fedha zinazokwenda *TARURA*, mbovu. Toka Nanyanga, pita pale unaenda Mdimba barabara haipitiki, lakini ni sehemu ambayo uzalishaji wake wa korosho wanazalisha zaidi ya tani 3,000 za korosho kwenye kata moja, lakini barabara ni mbovu, magari yanachakaa.

Mheshimiwa Spika, sasa badala ya kuzipeleka fedha *TANROADS* kuwe na uwiano aidha unaofanana, nusu kwa nusu; nusu mpeleke *TARURA* kwa sababu wanahudumia wananchi wengi kuliko hata *TANROADS* ambayo tunaitumia au 60 kwa 40. Asilimia 60 iende *TARURA* ili barabara za vijijini nazo ziweze kupitika. Mtakuwa mmewasaidia Watanzania wengi kuliko sisi ambao tunapata fursa tunapita kwenye ndege, siku nyingine kwenye magari, lakini vijijini wao kila siku shughuli zao zinahitaji barabara ziwe zinaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tafakari kwenye hili ikiwezekana mnavyoleta Mpango wenyewe sasa, basi tukute *TARURA* inakwenda asilimia 60, *TANROADS* inabaki asilimia 40 ili tusogeze mbele gurudumu la maendeleo la Taifa letu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Katani. Mheshimiwa Dkt. Peter Kafumu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy. Mheshimiwa Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ya Mpango iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi njema anayofanya pamoja na Serikali yake. Kipekee pia namshukuru Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake, tumekuwa tukipambana huko kwenye Kamati ya Bajeti, kwa kweli tunakushukuru wakati mwingine unasikiliza maneno yetu na mapendekezo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu tunaokwenda kuutekeleza au tunaouandaa ni mpango wa

mwisho kwenye Mpango wa Miaka Mitano; na mambo yote inayoyazungumza yalitokana na Mpango wa Miaka Mitano, ule wa 2016/2017 – 2020/2021. Mambo mengi tuliyojiwekea kule, sasa tunakwenda kumaliza kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme mambo mazuri ambayo Serikali imeyafanya, ni pamoja na miundombinu. Kama nilivyosema mwaka 2018, ukitaka kujenga nchi ya viwanda ni lazima uwe na miundombinu. Kwa kweli Serikali imefanya vizuri sana kwenye ujenzi wa reli, barabara, chanzo cha umeme na miundombinu mingine inafanywa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto kidogo ambapo nitatoa ushauri kidogo kama wenzangu walivyosema, kwamba Serikali ichapue kidogo, iongeze *speed* kidogo katika kutekeleza ujenzi wa miundombinu. Naomba tena na mwaka 2018 nilisema, Mpango huu basi mwangalie, kuna barabara nyingine za kiuchumi kama barabara ile inayotoka Shinyanga, inapita katikati ya Igunga inaelekea Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kuna mabasi huwa yanatoka Shinyanga yanaenda Mbeya kupitia katikati ya Igunga. Hii barabara naomba iwekwe kwenye Mpango, nasema tena kwa sababu barabara hii inatoka Ukenyenge, inakuja Igurubi, inapita Mwamakona, inakwenda Igunga, inaenda Rugubu, inaenda Itumba, inenda Loya, inaenda Tura, inaenda kuunganisha na barabara inayotoka kwa wachimbaji madini kule Mbeya na barabara inafika Mbeya. Najua kwa upande wa kule imeletwa mpaka Rungwa. Naomba sasa iunganishwe barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii sasa hivi kuna kipande cha kutoka Igunga kwenda Itumba, kimepewa fedha kidogo, lakini utekelezaji umcheleweshwa. Naomba basi katika Mpango, hii barabara ni ya kiuchumi inapita kwenye pamba, kwenye mpunga na kwenye ufugaji wa ng'ombe. Ni muhimu sana tuharakishe miundombinu ili tuweze kujenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la miundombinu ya maji. Kama Waheshimiwa Wabunge wengine wanavyosema, maji ni shida kubwa katika nchi yetu. Tunaishukuru sana Serikali kuanzisha ule mradi wa maji wa Ziwa Viktoria na sasa hivi unakwenda Tabora – Igunga – Nzega. Ahsante sana Serikali kwa kutukumbuka. Igunga ni nchi kame sana, lakini nadhani maji haya yatatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kwenye Mpango huu basi tuongeze fedha kwa ajili ya kupeleka kwenye zile kata ambazo zimebaki. Sasa hivi tunapata kata kama nane hivi; zinabaki nane kwenye Jimbo la Igunga. Pia kuna Kata nyingine nyingi zinabaki kwenye Jimbo la Manonga ambalo ni Wilaya ya Igunga. Basi tuweke Mpango mwaka 2010 tumalizie kwani wananchi hawa wako kwenye ukame mkubwa, waweze kupata maji. Tutawashukuru sana Serikali mkitukumbuka mkaweka kwenye Mpango jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda ni suala ambalo Serikali ilijiwekea kwenye mpango wa mwaka 2016/2017 mpaka 2021. Ilikeleza mambo machache mle ndani yakiwa ni pamoja na kutekeleza miradi ya kimkakati. Miradi mingi ya kimkakati imeshindikana kutekelezwa. Mwaka wa tano leo au mwaka wa nne tunamalizia, mingi bado inasuasua. Naiomba Serikali tena, tuendeleo kuiweka kwenye mpango na tutafute fedha ya kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, miradi ya kuendeleza maeneo maalum, kwa mfano, mradi wa kuendelea eneo la Mtwara ambako kuna gesi; tulianza vizuri, lakini kuna mahali tukalega tukaenda pembeni. Kwa hiyo, mradi wa LNG unahangaika, leo mwaka wa tano haujatekelezeka. Naiomba Serikali, hebu malizieni mazungumzo na hawa wawekezaji. Mradi huu ni muhimu, tutapata gesi ya kutumia ndani na pia tutapata gesi ya kupeleka nje tupate fedha za kigeni. Ni jambo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi hiyo pia tutaweza kujenga kiwanda cha mbolea, ambacho kimetajwa vizuri sana kwenye Mpango, lakini leo mwaka wa nne tunasema tu. Naiomba Serikali, hebu yaangalieni mambo haya, maeneo haya yako mengi, ila Mtwara kwa kweli, hebu tulitazame vizuri, hii gesi itumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine tumeusema sana kwa muda mrefu, ambao ni mradi wa Mchuchuma, Liganga. Pale kuna chuma cha kutosha kinachoweza kututosha nchi hii kujengea barabara zetu, reli, madaraja na kujenga maghorofa kama tukichimba kile chuma. Kwa miaka mitano sasa hatujaweza kutekeleza. Naomba tena kwenye Mpango isisitizwe na tuweke fedha kidogo huu mradi uweze kutekelezeka. Vinginevyo kwa sababu viwanda vinategemea sana viwanda vya chuma, tutaweza kuwa na chuma cha kuenea kwenye viwanda vingine vyote vya chuma katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lililosemwa kwenye Mpango ule wa miaka mitano na Mpango wa mwaka 2018 na wa mwaka huu 2019, limesemwa vizuri, ni jambo la kufundisha wataalam na kuchukua teknolojia, hasa wataalam wa ngazi ya kati. VETA tunafanya vizuri, tunapata mafundi mchundo vizuri sana. Na mimi Wilaya ya Igunga tumeletwa ujenzi wa VETA, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ngazi za kati, mafundi sanifu, Vyuo vya Mafundi Sanifu vimekuwa vichache na bahati mbaya wakati mwingine Serikali inavigeuzi hivi vyuo kuwa Vyuo Vikuu au inaviruhusu vianze kutoa *degree*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni Chuo cha Madini Dodoma, kilianzishwa ili kupata mafundi mchundo, nami nilishiriki kukianzisha wakati nikiwa Serikalini, lakini sasa hivi kinalelewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Matokeo yake ni kwamba kitakuwa na hamasa na tamaa ya kuwa Chuo Kikuu na kukibadilisha kuwa Chuo Kikuu. Tutakosa

mafundi mchundo watakaoshiriki katika ujenzi wa viwanda.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali mliangalie jambo hili kwa makini kidogo. Nakumbuka nilihudhuria Kamati ya Madini na Nishati, pamoja na Wabunge wengine wa kamati hiyo, tulisema maneno haya kwamba msiwe na hamu na haja ya kubadilisha hivi vyuo kuwa Vyuo Vikuu, mtachelewesha uanzishwaji na uimarishaji wa viwanda yetu kwa sababu tutakosa mafundi sanifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kilimo. Ukiangalia kwenye Mpango, tulijiwekea mipango mizuri sana. Kilimo kinaweza kuendeleza viwanda sana kwa sababu malighafi nyingi zinatoka kwenye kilimo. Kwa mfano, pamba; tuna mkakati wa *C to C (Cotton to Clothing)* ambao unasema tuzalisha pamba kwa wingi, tutengeneze nyuzi hapa hapa na tutengeneze nguo hapa hapa, lakini mpango huo hauendelei kabisa. Hiyo *C to C* imekuwa *document* ambayo iko kwenye *shelf*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara pamoja na Idara zake na Wizara ya Kilimo kwa umuhimu wake muufufue huu Mpango, pamba itumike kujenga viwanda. Tusifikirie tu kuuza pamba nje. Tunapata taabu sasa hivi hatujalipa wakulima wetu, lakini tungekuwa na viwanda hapa hili tatizo la pamba, tatizo la bei lisingekuwa shida kubwa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la mifugo kwa mfano na lenyewe kwa kuwa tuna mifugo mingi, tunaweza kuwa na viatu hapa hapa, lakini hatutazami. Mpango huu uyatazame mambo haya tena ya kujenga viwanda kwa kutumia malighafi katika nchi yetu. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililila kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Malizia Mheshimiwa.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba niseme tena kwamba, Mpango umalizie yale mambo ambayo umeyaacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nami hapa niwaagize Kamati ya Nishati na Madini, kwa kweli, hili jambo la *LNG* hebu sisi Bunge Zima siyo rahisi sana kulifuatilia kwa undani, lakini kama Kamati, mna uwezo mkubwa sana wa kuibana Serikali na kujua *exactly what is*; siyo *what is happening*, ila ni *what is not happening* kuhusiana na *LNG*? Kwa sababu ni jambo kubwa.

Hata hiyo Mchuchuma pia, yaani Kamati ya Nishati na Madini tusaidieni kwenda kwa undani zaidi tuweze kujua. Kwa sababu, hayo ndiyo yatakayokwamua uchumi na kuupeleka mbele kwa haraka sana.

Nilikwishakutaja Mheshimiwa Kessy, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh. Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi jandae.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nami nimepata muda wa kuchangia Mpango wa Maendeleo wa 2020/2021. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Ndugu Dotto na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha. Kusema kweli wanakusanya fedha jinsi inavyotakiwa, lakini nasi Wabunge ndio tunapanga matumizi hapa. Matumizi yanakwenda jinsi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kidogo, mtaniwia radhi Waheshimiwa Wabunge. Sisi Wabunge lazima tuwe na uchungu na nchi hii kwa sababu, tumeletwa na kura za wananchi ambapo tulikotoka huko wana matatizo ya maji, tunadai barabara mbovu, tunadai sijui *TARURA* wapewe

pesa, sijui nani apewe pesa. Nasi Wabunge vilevile ndugu zangu, tuwe na moyo wa kumsaidia Waziri wa Fedha kuhusu matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku mimi nakwenda kwenye mazoezi kasoro Jumapili, lakini Waheshimiwa Wabunge hawa; humu ndiyo kuna Kamati za Michezo, Mwenyekiti wao yuko Mheshimiwa Ngeleja na ataniunga mkono mwana-mazoezi mwenzangu ambaye kila siku tuko naye kwenye mazoezi Mheshimiwa Naibu Spika atasema ukweli *lillah* hapa leo Jumatatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wako wanakuangusha. Hawaendi kwenye mazoezi hata mara moja. Ni wachache sana. Wanakwenda kwenye mazoezi wakisikia kuna safari, kwa sababu wanafuata maslahi. Hawaoni huruma na wananchi waliowaacha kule Majimboni kwetu hawana maji wala chochote. Leo nimeshuhudia, wamesikia kuna safari ya kwenda Uganda, wamejazana kule *Jamhuri Stadium* kwa makundi, sio akina mama wala akina baba. Mimi nimewaambia, leo naenda kuwachafua Bungeni, naenda kusema ukweli Bungeni, mmezidi nyie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anakusanya fedha, huwezi ukamtuma mtoto wako akutekee maji kwa kutumia msege. Akutekee maji kwa kupitia msege au kajungio, maji hayawezi kufika. Sasa ni baadhi ya Wabunge hawa, ni sawa na msege, sawa na chujio la kuchujia chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama ndiyo mhimili wako, sisi ni mhimili, lazima tuchunguze safari za Wabunge kwa michezo wanapokwenda nje. Watatuletea aibu kubwa, kwa sababu huwezi kwenda kucheza mpira huna mazoezi; huwezi kuvuta kamba huna mazoezi; au kucheza *netball* bila mazoezi. Hii lazima tuchunguzane ndugu zangu. Siyo tunapiga kelele hatuna maji, hatuna barabara, hatuna umeme wakati nyie mnatanua, mnakwenda kustarehe huko. Hamna faida yoyote kwenda nje. (*Makofi*)



(Hapa, baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia sasa. Mheshimiwa Waziri nisikie vizuri, wewe umetoka katika Mkoa wa Kigoma. Mkoa wa Kigoma umepakana na *DRC Congo*. Katika nchi tajiri katika ukanda wetu ni *DRC Congo*. Lazima akili yako, macho yako, Wizara yko ielekeze kufanya biashara na *DRC Congo* kupitia Ziwa Tanganyika. Lazima tuunde meli pale kubwa ya kupakia ma-*container* kupeleka Miji ya Kalemii, Uvira, Moba na Bujumbura kupitia reli ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma enzi ya Mwalimu Nyerere tulikuwa na meli ya mafuta pale, inapeleka mpaka Zambia kupitia Bandari ya Kigoma, leo hakuna kitu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, yeye anatoka Kigoma, anafahamu kabisa, *DRC Congo* mzee ndiyo nchi pekee tajiri katika ukanda huu wa kwetu na ina watu wengi na kila kitu. Tushirikiane na *DRC Congo*, ukikaa chini ya uaridi utanukia kidogo. Utafanya na masikini mwenzako, utapata kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima akili yetu ielekee *DRC Congo* kufanya biashara nao. Tusidanganyane hapa, *Congo* ndiyo pekee inayoweza kutuokoa. Leo nasikia kuna ujumbe mkubwa toka *DRC Congo* uko Uganda kule, wafanyabiashara wa *DRC Congo*. Nasi tuelekeze nguvu zetu kule, itatuokoa ile nchi...

**MWENYEKITI:** Wanataka kujenga barabara ya kilometa 1,000 kutoka Uganda kwenda *DRC Congo*. Uko sahihi Mheshimiwa, endelea.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tujitahidi. Vilevile wafanyabiashara wetu wote, leo wanachukua ma-*container* China, biashara ni China. Cha ajabu kule China kabla hujatoa *container* kuna *inspection*, unaacha dola 1,000 kukagua eti bidhaa zao. Wakati wanatengeneza wenyewe! Ukifika Dar es Salaam tena, *TBS*

wanakagua ile bidhaa, wanalipa dola 1,000 kule. Sasa sijui kama Wizara ya Fedha inafahamu hiyo dola 1,000, inarudi ngapi katika nchi yetu? Inachukuliwa China yote, kwa maslahi gani wakati tunanunua bidhaa kutoka China zao wenyewe, ulipie *container*? Ma-*container* mangapi kwa mwezi yanakuja Dar es Salaam? Tunapoteza shilingi ngapi? Dola ngapi tunapoteza kwa kila *container* kwa ma-*container* yanayoingia nchini kwetu kutoka China?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila *container*, uliza vijana wafanyabiashara wa Kariakoo, lazima waache dola 1,000 wanaita *inspection* kule China. Ukifika Dar es Salaam, lazima hilo *container* tena *TBS* wachukue pesa. Sasa tutafanyaje biashara, wanatuchukulia dola 1,000 Wachina kila *container*, wakati tunanunua bidhaa zao wenyewe? Je, kama hiyo dola inakuja kwetu Tanzania, tunajuaje kama inakuja yote dola 1,000 kwetu Tanzania? Lazima tuwe macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa ma-*container* nimeshamwambia Mheshimiwa Waziri, lazima nipate majibu haraka sana kuhusu hiyo, kama wanakagua ma-*container* yetu au namna gani. Kuhusu Bandari ya Kigoma, imekufa, haina maslahi kabisa, imekufa Bandari ya Kigoma. Ukifika pale wanakula tu mishahara. Lazima tuifufue kwa ajili ya kusaidia kwenda Bujumbura na Kalemii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani ni kitu cha ajabu kusema kweli, tunaacha hela. Sisi bandari yetu tumezungukwa na nchi, tumezungukwa na Zambia, Malawi, Burundi na Rwanda. Akili yetu yote kwa sasa tuhakikishe bidhaa zote za kwenda Malawi, Zambia, Mashariki ya *DRC Congo*, Burundi na Rwanda zinapitia katika nchi yetu. Lazima akili yetu ilenge hapo. Akili yetu ilenge bidhaa zote za kwenda Rwanda, Burundi, Mashariki *DRC Congo*, Zambia na Malawi, lazima zipitie kwenye bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Tunduma pale lazima tufanye mikakati kupanua barabara. Msongamano wa magari ya pale Tunduma lazima tuupunguze ili biashara

iende haraka haraka pale Tunduma, siyo gari inakaa siku tano, siku sita au saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fanya ziara, nenda pale Tunduma, utaona huruma. Magari yanalala mpaka 1,000 au 1,500. Sasa hii biashara mzee, nchi lazima tuwaze biashara. Haiwezekani kuweka magari mpaka 1,000 pale Tunduma kwa muda mrefu. Kuna malori ya mafuta, ukitokea moto pale Tunduma, mji mzima utaungua. Mji mzima wa Tunduma utakwisha. Malori yanayojaa Tunduma pale ni ya ajabu, msongamano ni wa ajabu, kwa nini msifanye taratibu za kuvusha magari haraka haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtafute mpaka mwingine kutoka nje ya Tunduma kule yapite magari, *custom* waongeze, tupate hela haraka haraka, tunakawaiza biashara. Ndiyo maana sisi Watanzania ukiambiwa saa 3.00 uje unakuja saa 5.00; ukiambiwa uje saa 6.00 unakuja saa 9.00. Hatuendi namna hiyo. Ukiambiwa saa 6.00 iwe saa 6.00. Kama hujafika saa 6.00 unaachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuamke tufanye biashara. Sasa ni kipindi cha kufanya biashara. Tumwige Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli anataka mambo ya papo kwa papo. Aliyofanya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli hakuna mtu aliyetegemea, miradi hii ya kujenga reli ya mwendokasi, mambo ya umeme nani alitegemea? Kununua ndege haraka haraka, nani alitegemea? Inataka uamuzi wa ujasiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa, unatamka kabisa wewe mkuu wa chama kabisa mwenyekiti wa chama au katibu wa chama unamuhusisha Rais Magufuli na uchaguzi wa Serikali za Mitaa wakati kila siku kwenye redio na television Rais anahamasisha wananchi chagueni kiongozi yeyote akiwa wa CCM akiwa CHADEMA, ACT Wazalendo chagueni; anatamka mwenye Mheshimiwa Rais; leo utamsingiziaje Rais anaingia kwenye mchakato wa uchaguzi, anahusika wapi? Pambaneni na Tume ya Uchaguzi, hamasisheni wenyewe huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wenyewe wameshachoka,kazi anayofanya Rais, Mheshimiwa John Pombe Magufuli inaonekana, sasa mgombea gani atakwenda kugombea kwenye chama kingine aonekane? Wenyewe walikuwa wanadai ufisadi amepigana na ufisadi amemaliza, amewabana watu wote, amefungua mahakama ya ufisadi. Kila kitu walichokuwa wanadai kwenye mikutano ya hadhara Mheshimiwa Rais katanguliza mbele; sasa hawana hoja, hakuna hoja.

Mheshimiwa Spik, jana Mheshimiwa Waziri Jafo kawaambia, jamani hamna kuweka mpira kwapani, wote nendeni kwenye uchaguzi. Sasa mnataka kudai tume huru hiyo tume huru utaitoa wapi?Mbinguni kwa malaika? si binadamu wetu hawa hawa? Kwahiyo ndugu zangu hakuna haja ya kubabaika, tarehe 24 twendeni kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu zingine kama kule Nkasi chama kama cha CUF wala hukisikii kabisaa!Wala hatukijui kabisaa!Sasa nashangaa unasimama hapa unasema fomu zetu sijui umetunyima sijui zimefanya namna gani; nani anayekufahamu? nani anakujua?Ni mambo ya miujiza kabisa.

Ndugu zangu tusisingiziane mengi twendeni kwenye uchaguzi. Mambo yalijionesha mapema kabisa; madiwani wangapi wamehama, inajulinana, Wabunge wangapi wamehama, wenyeviti wangapi waliacha kazi. Sasa ninyi wenyewe mnavyojiona na mnavyojipima mmeona hamna hoja. Mmebak wachache ndugu zangu, mti unaokauka hata ukiumwagia maji mizizi imeshakauka, hauwezi kustawi

**MHE. MCH. PETER S. MSINGWA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**SPIKA:** Mchungaji unamnyanyukia Mheshimiwa Keissy?

**MHE. MCH. PETER S. MSINGWA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimpe taarifa tu.

## T A A R I F A

**SPIKA:** Haya mpe taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSINGWA:** Mzungumzaji anayezungumza kwamba kuna vyama vingine havipo kwenye maeneo yake; inawezekana kweli vyama vingine havipo kwenye maeneo yake lakini vyama vingine vipo. Isipokuwa nataka nimjulishe kwamba malalamiko ambayo wengine wanayatoa hapa; mfano mzuri ni mimi mwenye pale Jimboni kwangu Kata ya Gangilonga tangu siku ya kuchukua fomu ilifungwa mpaka mwisho mtendaji anaondoka; haijawahi kuchukuliwa fomu hata moja, hayo ndiyo malalamiko nilitaka apate taarifa; na maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema, hatukimbii uchaguzi tunataka tuwe na uwanja *fair*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa, siipokei taarifamaana *clipya* Mheshimiwa ninayo. Alipokwenda Rais, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kule kwake Iringa alimsifu vibaya. Kwamba nakushukuru Mheshimiwa Rais miradi yote naiona Mheshimiwa Rais, kwahiyo sisi hatuna tatizo lolote. *Clip* yako tunayo Mheshimiwa na inatembea Mheshimiwa; wewe mwenyewe Mheshimiwa ulimpongeza Mheshimiwa Rais kwa hali na mali ulimpongeza Mheshimiwa sasa sijui kama wananchi wako watakuielewaje Mheshimiwa

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## T A A R I F A

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko nimekuona, taarifa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kumpa taarifa ndugu yangu Keissy, na mimi nakubaliana naye, kwamba kwa mfano Jimbo la Kakonko yule aliyekuwa mpinzani mkubwa wa Chiza kwenye *by-election* na timu yake yote wamerudi CCM leo. Kwahiyo ni kweli hawana wagombea. Nilitaka tu uwe na amani katika jambo hilo.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Keissy muda umeisha.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa, anayosema unaona anayadhihirisha kabisa napokea taarifa Mheshimiwa Msigwa mwenyewe *clip* yake inatembea kabisa anaiona; sijui kama alikuwa si Msigwa huyu au namna gani, kavaa hivi hivi kila kitu na suti. Sasa nadhani *clip* yake labda nitamkumbusha, nitakutumia *clip in box*, labda utaisikiliza vizuri. Wewe mwenyewe ulikiri kwamba awamu ya nne imefanyakazi.

**SPIKA:** Awamu ya tano.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Awamu ya tano imefanyakazi nzito. Jana nililala lringa kwa Mheshimiwa hapa, hata uchaguzi watu wamesharidhika, watu wamesharidhika Mheshimiwa Msigwa umebaki peke yako, usione aibu kurudi Mheshimiwa Msigwa rudi haraka tunakuhitaji. Ahsante sana nashukuru sana. (*Makofi/Vigelegele*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ally Saleh sasa unachangia.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwanza kabla ya yote napenda kwa mara nyingine tena ku-*register* kwamba bado sioni mantiki ya kutengeneza mpango wetu bila ya kuwa na *connectivity* yoyote ile na Zanzibar, bado akilini mwangu nataabika. Unawezaje kutengeneza uchumi wa nchi pasiwe na

*connectivity*, hiyo bado najiuliza, na kwanini kila mara hili halifanyiki? Napenda iwepo *on record*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili na katika mpango umezungumza...

**SPIKA:** *Connectivity* gani Mheshimiwa Ally Saleh, kwa dakika moja tu ili akupate vizuri.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano wakati ule wa mpango wa mwanzo kulikuwa kuna miradi kielekezi, na tulisema angalau mradi mmoja ukiwekwa Zanzibar utasaidia kazi, utasaidia ajira, utasaidia kila kitu. Si kila kitu kiwekwe huku, hata kama cha muungano kikiwekwa kule kinaweza kikasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Bandari ya Bagamoyo. Unaweza ukawa na Bandari ya Bagamoyo lakini kuweco na *connectivity*; kazi fulani inaweza kufanywa Zanzibar; kwa mfano namna ya ku-*repair* au ya kufanya vitu gani hiyo ndiyo *connectivity* ambayo nazungumzia lakini huu mpango tunachoambiwa ni kwamba Zanzibar wanampango wao lakini *at the end of the day* hii ni nchi moja hakuna *connectivity*, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu dhima; dhima nimeipenda kwasababu inaelezea juu ya kuongeza mauzo ya nje na uwezo wa ushindani, hii ni dhima nzuri sana kwa nchi kujiwekea kwasababu hapa nikieleza itaonekana kwambanaiunga mkono kwasababu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevie tumechagua maeneo matano ya mkakati ambayo mimi nitataja matatu ambayo yamenipendeza; nayo ni uchumi wa viwanda, uchumi wa watu na uwezesaji biashara na uwekezaji, na ninataka nianzie hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kuungana na Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Wilfredy Lwakatare na Mheshimiwa Peter Selukamba, nafikiri na

mmoja mwingine yoyote ambaye amesema. Kwamba kuwepo sisi hapa kama nchi *coordinance* kadhaa mpaka *coordinace* kadhaa Mwenyezi Mungu ametaka tuwepo na fursa zimetuzunguka. Kwa mfano amezungumza Mheshimiwa Lwakatare juzi, wanasema walipo wao kuna fursa mpaka *South Sudan*; leo Mheshimiwa Ally Keissy anasema kwamba tunapakana na moja katika nchi tajiri Afrika ingawa *per capitallyake* ni *dollar 627* lakini wana *strength* ya watu na pia wanautajiri wanchi.

Kigoma tunapakana na nchi nyingine nyingi pale, pamoja na Kongo je tunazitumia vipi fursa ya uwepo wetu katika maeneo hayo? Kama nchi tunajielekeza vipi maeneo yaliyo pembezoni kwa jina tu lakini ndiyo ambayo yalitu-*open up*. Kwahivyo bado nahisi hata kama tutatekeleza maeneo ya kilimo, maeneo ya *deep sea*, uwekezaji, biashara elimu, nishati na LNG *inparticulama energy mix*, kama alivyosema Mheshimiwa Selukamba bado tunataka *outs* tunataka tutoe vitu vyetu. Umesema hapa China, lakini *it is not only China*, kuna nchi nyingi. Urusi *per capital* yao *24 thousand per person*, Uchina yenyewe ni *per capital* yao *16,000* lakini Uturuki *per capital* yao ni *26*. So, *it is not only China*. Nakubaliana na mtu aliyesema nikutafuta *new markets*; kama tunavyotafuta *new market* kwenye utalii, basi tutafute *new market* kwenye uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uturuki/s so *strategicallylocated* kwa Asia na Europe. Ni njia ya kuingia Europe kirahisi, ni *eighthours* from Dar es Salaam. Uturuki wanaleta ndege mbili kila wiki, wanaleta ndege tatu kila wiki lakini *almost nothing leaves here to go to Turkey* kwasababu hatujajitayarisha kibiashara. Pia Uturuki na kama vile tunavyokaribisha Urusi, wanauwezo mkubwa sana wa kuwekeza, *the money is there for them* wanachotafuta wao ni waziweke wapi. Sasa mimi nafikiri kuna haja ya kutazama hili hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine; kwamfano tumezungukwa na bahari, kila siku tunasema; tunaambiwa kutakuwa na bandari ya utalii, bandari ya uvuvi. *Issue* si



bandari ya uvuvi, *issue* ni kuwa na mipango kwanza kabla hujajenga bandari, watu hao wanaokuja kutuvulia ndio watakaotupa pesa ya kujenga bandari. Una uvuvi unaotoza kilo moja unaotoza dola 0.4 kwa kilo moja ya samaki, unawavunja moyo wanaokuja kutaka kuwekeza kwenye habari ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo *issue* si kuwa na mipango, lakini ni kupanuka, ni kutazama fursa mpya. Kila siku fursa mpya zinakuja, kila siku watu uchumi wao unaongezeka duniani; soko la Arabuni Qatar, Dubai pamoja na Oman. Tumefanya nini kama nchi? Kwahiyo mimi nafikiri kama ilikuwa mpango ule upo sasa haupo, kwamba pale mwanzo wa awamu hii walikuwa Mawaziri au safari za nje zilikuwa kidogo kwa watendaji mimi nahisi ni wakati sasa tupanue safari kwa watendaji ili waende wakatafute masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu gani utapeleka India kirudi, kitu gani utapeleka India kirudi kitu gani utapaleka China kirudi, kitu gani utapeleka Qatar kirudi, kwasababu wao hawalimi *as such*. Lakini bado, nchi kama Oman pamoja na kwamba wana utajiri mkubwa na wana gesi wana kitu gani lakini bado hawana kilimo cha kutosha na sisi tunaweza tukajazia mazao yao huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, kuna jambo moja ambalo limo katika mpango lakini limetajwa *just in passing*; kidogo tu limetajwa, nalo ni utawala bora. Dunia ya leo ni wazi kabisa huwezi kuwa na uchumi mzuri kama hujawa na utawala bora, nchi chache tu zimepenya; labda Indonesia zamani, zilizokuwa *Tiger* zile, walikuwa na ukandamizaji kandamizaji lakini bado wakapenya. Hata hivyo bado, ukiwa na utawala bora ndiyo unakusaidia kwenye uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la utawala bora bado mimi nina wasiwasi nalo katika nchi yetu. *Public space* inazidi ku-*shrink* kila siku, fursa za maoni zinazidi kupotea. Tumetunga *Access To Information Act* miaka kama 10 nyuma

huko au saba nyuma mpaka leo hatujatunga kanuni. Kwa hiyo bado mwananchi hawezi ku-*access information* ambayo anaitaka kutoka Serikalini. Vilevile uhuru wa vyombo vya habari ambao umekuwa ukilalamikiwa sana. Kwamba vyombo vya habari vinaogopa kuandika, ingawa unaweza ukasema uhuru upo lakini watu wanaogopa. Pia mfumo wa mahakama; tuna mashekhe leo miaka saba wako jela hata kesi haijaanza. Kwahiyo hii inatutia doa kwa watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi sasa imekuja hii *issue* ya Serikali za Mitaa; mimi nahisi hii ni aibu kwa taifa, kwasababu huwezekani unakata asilimia 96 ya wagombea; *at least* kwa chama cha ACT na CHADEMA asilimia tano; halafu anakuja Waziri na *simple statement* ambaye kabla yake alisema hakuna kilichobadilika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh naambiwa muda hauko upande wako

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Ulinipa dakika 10 Mheshimiwa?

**SPIKA:** Yuko katibu anaangalia

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Nitazona katika *clip in shaa allah. (Makoff)*

**SPIKA:** Anaangalia hapa maneno; ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh. Mheshimiwa Dkt Sware dakika tano, endelea tu

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi name niweze kutoa mawazo yangu katika mapendekezo ya mpango ulio mbele yetu. Nilifikiria kwanza nina dakika 10 au 15 sina uhakika na dakika tano. Basi nitajitadi basi nilikuwa na mambo matano kwa ujumla wake.

**MWENYEKITI:** Jitahidi zitakuwa dakika saba ili umalize.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana jambo la kwanza nilikuwa nataka niligusia ni kuhusu ufuatiliaji na tathmini (*monitoring and evaluation*) ya mpango wetu ulio mbele yetu. Mpango huu ni *proposal* ya kumaliza mpango wa miaka mitano 2016/2017, 2020/2021, lakini kwa bahati mbaya kilichoandikwa humu ndani kwenye ule mpango wa miaka mitano ni kwamba tungeweza kufanya tathmini ya mpango huu wa pili wa maendeleo wa taifa wa miaka hii ambayo tunaenda kuimalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni ngumu kufuatilia mapendekezo ya mpango wa kwenda kumaliza kama huku nyuma hatujajitathmini. Mpango wa kwanza umeisha na huu unaenda kuisha ukingoni bila kujitathmini tumewezaje kufanyakazi. Kuna umuhimu mkubwa sana wa kufanya tathmini kwa kuwa tathmini ndiyo inakupa dira ya nini tunafanya maelekeo yetu yakoje, kuna mabadiliko ambayo tunatakiwa tuyachukue ili tuweze kuboresha na kuweza kufanikisha malengo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mpango wa miaka mitano umeandika vizuri sana, hauna hata kasoro, kwa kweli umekaa *technically correct*. Sasa shida inakuja kwenye utekelezaji; kwa mfano ukurasa 128 (7.4.4) unaongelea mahususi kuhusu tathmini ya mpango wa pili huu wa maendeleo ambao tunaenda kuhitimisha, na kipengele cha pili pale kinasema kuwa kutakuwa namapitio ya muda wa kati wa utekelezaji; na tumeji-*commit* katika mpango huu kwamba tutaanzisha Mkutano wa Rais wa Mpango wa Pili wa Maendeleo katika muda wa kati wa utekelezaji ili kuangalia namna bora ya kubadili ama itaonekana ulazima wa kufanyia *review*. Sasa inakuwa ni ngumu kuendelea kutoa mapendekezo ilhali yale mapendekezo hatuyaoni yanafanyikaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ninataka niligusia ambalo linahusiana na tathmini ni kwamba kumekuwa na changamoto nyingi sana ya upatikanaji wa fedha za maendeleo, maendeleo ndio huo

utekelezaji wa mpango. Katika wizara na taasisi nyingi tumeshindwa kufika malengo, tuko *below* 50. Sasa tuna mpango ambao unaendana na nini tumekiamua na bajeti kiasi gani kiweze kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona tuna changamoto ya kibajeti katika kutekeleza shughuli za maendeleo. Nilikuwa nategemea kwamba tungekuwa tumefanya tathmini ili tujiangalie ukusanyaji wetu wa mapato na mapungufu yake ni yapi ili tuweze kuboresha. Kwahiyo tunaenda kumaliza huu mpango wa pili lakini hatujui bado tunachangamoto za kimapato. Sasa ingekuwa ni vizuri basi; najua wataalamu wapo na uwezo huo tunao; tukapata huo mchanganuo kwamba *setbacks* zilikuwa ni nini ili kwamba huu mpango wa miaka mitano tunakwenda kuumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, kama tungekuwa tumefanya tathmini tungeweza kujionesha kwamba tumeutekeleza kwa asilimia ngapi katika sekta mbalimbali. Sasa hivi ni vigumu kusema kwamba sekta ya kilimo ina *perform* kiasi gani. Moja ya mfano, katika sekta ya kilimo ambayo ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu tunaoimba kila siku, ambao unaweza sasa kuubeba huo mpango wetu wa kusema uchumi wa viwanda. Tulijiwekea *target* kwamba tunapomaliza miaka hii mitano ya mpango kilimo chetu kingekuwa kimefikia kukua kwa asilimia 7.6 japokuwa huku pia huku pia napo inasomeka asilimia kumi naa! Hata hivyo ukiangalia kwa miaka hii mitatu iliyopita ile asilimia imeshuka, na huu mwaka ulioishia kilimo kimekua kwa asilimia 5.3. Sasa tulikuwa nategemea kwamba tunapokaa hapa kama kamati tunatokaje ili kupandisha viwango hivyoambao tulijiwekea katika hii miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu na ambalo naomba niligusie ni kuhusu masuala ya ardhi. Imeandikwa pia vizuri sana katika kitabu chetu cha mpango ambapo sekta ya ardhi tumeona kwamba ni *key* katika maendeleo ya kiuchumi kwasababu ni rasilimali ambayo tunaiishi na tunaweza kuzalisha katika hiyo ardhi. Hata hivyo kumekuwa

na migongano mingi ya jinsi ambavyo tunaweza tukaitumia ardhi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unaweza ukarejea, ukurasa wa 110 kumekuja na njia mbalimbali na maboresho mbalimbali katika usimamizi wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika IV, V, VI, Serikali iliji-*commit* kuimarisha mfuko wa fidia wa ardhi ili kuondoa ucheleweshwaji wa malipo ya fidia baada ya kufanyiwa tathmini. Namba tano tuli-*commit* kwamba kuna haja ya kufanya mapitio ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.4 na Sheria ya Ardhi Na. 5; na *commitment* ya sita tuliweka kwamba kuhakikisha mipango sahihi ya matumizi bora ya usimamizi wa ardhi. Sasa tusipo-*invest* kwenye matumizi bora na usimamizi bora wa ardhi; tumeongea katikakamati yetu hata hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani Bungeni imeongelea hiyo *component*; inabidi sasa tuwekeze. Tunasema tu tunaenda kufanya mambo ya viwanda, shughuli yoyote ya rasilimali yoyote lakini kama ile ardhi ina shida hatuwezi kuvuka; kama tunavyokwenda kuboresha miundombinu. Tumeona kuna *tensions* nyingi katika kutengeneza miundombinu ili kukuza uchumi lakini unaleta shida ya fidia kwa wananchi. Tumeona migogoro mbalimbali ya rasilimali kama ni kilimo au wafugaji kwenye masuala ya ardhi. Tumeona jinsi matumizi mabaya ya ardhi yanavyoleta matokeo ya mafuriko na kadhalika, yanaenda kuturudisha nyuma badala ya kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba Serikali iangalie hili kwa upya. Kwamba kuna umuhimu sasa wa kuwekeza katika matumizi bora ya ardhi, tuwe tuna *proper planning* ya ardhi ili kuweza kutuvusha hapo na isiwe kikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la nne nafikiri, au ni la tano, linauhusiano moja kwa moja pia na ardhi. Mimi niko kwenye Chama cha Wabunge ambacho kinapigania masuala ya kutokomeza Malaria (*TAPAMA*). Moja ya *issue* ambayo tunaizungumzia, imekuja sasa wiki hii

katika majadiliano yetu, ni jinsi mambo ya sekta ya afya yanavyo *link* moja kwa moja na sekta ya ardhi. Mfano bora ni kwenye masuala ya malaria. Serikali inatumia gharama kiasi gani katika kudhibiti malaria au katika kuleta tiba ya malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia, kinachosababisha Serikali inawekeza sana katika tiba katika afya ni kwasababu tunakosa matumizi bora ya ardhi; na wengiambao wanaguswa na kutokuwa na matumizi bora ya ardhi ni watu wa kima cha chini, na hawa watu wa kima cha chini ndio watu walio *more prone* kwenye magonjwa kama ni ya mlipuko au ni malaria. Sasa tukiwa tunamaboresho ya matumizi bora ya ardhi *plus* kuboresha makazi ya hawa wananchi basi tunaweza tukatokokeza haya magonjwa ambayo yanaturudisha nyuma kama wananchi kwasababu magonjwa haya yanaenda kutu-*affect*akili katika utendaji kazi na kutumia rasilimali kubwa ya nchi. Kwahiyo naomba Serikali iangalie jinsi yaku-*link up* matumizi bora ya ardhi na shughuli za kiuchumi na shughuli za kiafya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

*(Hapa kengele lililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Sware

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SWARE:**Mheshimia Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunashukuru sana. Mheshimiwa Norman Sigalla atafatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau.

**MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii kuchangia kidogo kuhusu Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza kwanza shukrani kwa Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri anayoendelea kufanya mpaka sasa hivi. Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nikapata nafasi ya kushiriki ziara ya siku 21 ya mafunzo ya uendeshaji wa ndege, bandari pamoja na reli (*SGR*) pale China. Nilichojifunza ni nini? Nilichojifunza ni kwamba Bandari ya Bagamoyo ni mpango halisi wa Wachina wa kutaka kuisaidia Tanzania kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba Serikali ina macho/sura nyingi inavyoangalia jambo hili lakini jambo lenyewe hili usahihi kabisa ni kwamba niliongea na Wachina wakanionesha michoro ile, wakaonesha jinsi ambavyo Bandari ya Bagamoyo itakuwa inalenga kukwamua uchumi wa Tanzania. Pia wakaonesha kwamba tayari kuna makubaliano ya Mawaziri wetu wa Uchukuzi na nchi za Burundi na DRC Congo ya jinsi ya kuhakikisha kwamba wana-*ferry* chuma Msongati kwa kutumia Bandari ya Bagamoyo. Kwa hiyo, wao walipokuwa wanapeleka nguvu kuhakikisha kwamba wanajenga reli ya *SGR* wanafikiria zaidi kwenda Uvinza, Msongati, Burundi kwa sababu tayari kuna makubaliano ya kimkataba ya nchi ya Tanzania na Burundi. Pia kuna makubaliano ya mkataba kwenda Kalemi kwa sababu ya nchi ya Congo DRC na Tanzania pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba suala la Bandari ya Bagamoyo ni ni muhimu sana kwa Tanzania. Sina hakika kama Serikali ina taarifa sahihi kuhusu jambo hili kwa sababu tumekaa pale siku 21, siku 21 za mafunzo ni nyingi sana kwa mtu mzima lakini tumekaa pale tukajadiliana na tukaoneshwa waziwazi jinsi ambavyo Bandari ya Dar es Salaam itazidiwa nguvu kama chuma cha Msongati kitachimbwa inabidi kipelekwe Bandari ya Bagamoyo ifanye *ferrying* ya chuma kile. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri sana ijulikane hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mradi wa Chuma wa Mchuchuma na Liganga na nimesema mara nyingi hapa, huu ndiyo mradi ambao sisi Watanzania ni wa kujivunia. Napata shida sana kuelewa kwa nini Serikali inapata shida kupeleka fedha na kutia saina mikataba ya Chuma cha Mchuchuma na Liganga kwa sababu mradi huu upo wazi. Ni kweli kabisa kama mchangiaji mwingine alivyosema kwamba miradi hii inasaidia sana kuongeza ajira za watu wetu kwa wingi sana. Bandari ya Bagamoyo, Mchuchuma na Liganga ni miradi ambayo itaongeza ajira kubwa sana kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ni kweli *you cannot do anything now without* China, ndio ukweli. Ukweli wa mambo kwa uchumi wa sasa hivi ukifanya *skeleton* ya uchumi wa dunia unavyokua huwezi ukajitenga na China, haiwezekani. China kwa sasa hivi *is a leading country* kwa uchumi. Nasikitika sana kusema hivyo kwa sababu China walinifikisha mahali ambapo waliona nafaa kuwa Mwenyekiti wa nchi 16 walioenda China lakini pia walionona mimi kama ni *unique person* kwa sababu natoka Tanzania nchi ambayo wao wanaipenda. Kwa hiyo, wakaniambia kwamba wanakusudia kuifanya Tanzania kuwa ndio *hub* ya uchumi wa China Afrika kwa sababu reli inayojengwa Nigeria (Enugu) kuja Bujumbura inaunganishwa na reli inayokuja Msongati kwenda Bagamoyo, ndiyo *master plan* yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wao walikusudia kwamba Tanzania itakuwa ndio *hub* ya uchumi wa China Afrika. Walisikitika sana kuona kwamba Kenya wamekuja *of late* wamekubaliana kutengeneza reli ya kutoka Mombasa kwenda Nairobi kwa sababu mpango ulioanza ni wa kwao wa Dar es Salaam kwenda huko tunapopeleka lakini Kenya wakaja nyuma yake wakajenga reli ya kutoka Mombasa mpaka Nairobi na imeshakamilika na wanatengeneza fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie kwa makini sana juu ya China. China ni nchi



ambayo inatupenda sana sisi na sisi tuna mahusiano ya damu na China, sio mahusiano ya kubahatisha. China kama akikosea tunaweza kuwaambia, tukiwaambia wanakubali na wanaelewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania na China tuna mahusiano ya muda mrefu, mahusiano ya Mwalimu Nyerere na Mao Tse Tung ni ya muda mrefu. Kwa hiyo, ni hawa hawa waliojenga SGR hii ta TAZARA ya Dar es Salaam kwenda Zambia na wamejenga miaka hiyo wakati hatuna uwezo. Kwa hiyo, leo hii kwa nini tuone kwamba wao ni shida? Nafikiri lazima Serikali iangalie vizuri ili kufika mahali ambapo tunaweza tukafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo tutafanikiwa sana. Tanzania ni nchi bora sana lakini tutumie kwa usahihi nafasi na fursa ambazo tunazo. Tusipotumia kwa usahihi fursa tulizonazo tutapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana ku-*resort into these plans* ili tuweze kwenda nazo mbele, tuisikie maneno ya watu. Maneno ya watu wengi ni kutufanya sisi Tanzania tusifanikiwe. Wanasema China imefanya hivi, wanatoa mifano ya China kununua mgodi wa Zambia, tunaoujua vizuri uchumi wa China tunasema siyo kweli, kilichotokea Zambia ni kingine na Tanzania tunafanya vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali yangu ya Tanzania ikubali ushauri huu iutekeleze mradi wa Bagamoyo na chuma Msongati. Mungu awabariki sana. Amina. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Norman Sigalla kwa hotuba yako nzuri sana katika suala hili la Mpango. Kwa kweli na mimi niweke neno kwa nusu dakika hivi. Mlinipa nafasi ya kuwa Spika wenu, miezi mitatu iliyopita nilienda China kwa niaba yenu ikiwa ni ziara ya kwanza rasmi ya Spika wa Bunge la Tanzania kutembelea China

kuanzia tupate uhuru. Kwa hiyo, nilipata nafasi ya kuwa karibu sana na wenye maamuzi.

Nchi ya China inaongozwa na watu saba kwa sababu *its 1.4 billion people they cannot entrust one or two persons*, wana hiyo *panel* ya watu saba. Kwa hiyo, kwa niaba yenu nimepata nafasi ya kuwa karibu sana na hao watu saba, sio wote lakini baadhi yao.

Waliniambia hivi, Mwalimu Nyerere alikwenda pale China kwa mara ya kwanza 1965 wakiwa wametengwa na dunia wakati ule, walifurahi sana Wachina. Alipomuomba Mao kujenga reli ya TAZARA japo *per capita income* kati ya China na Tanzania wakati ule ilikuwa inafanana dola 100 lakini walikubali kuja kujenga reli kwa ile furaha waliyokuwa nayo na Mwalimu amekwenda China katika maisha yake mara 13, wananiambia wao. Wanasema wakati ule tulikuwa masikini, leo sisi tajiri na ninyi ndugu zetu bado tunakumbuka kwamba wenzetu tuliokuwa pamoja bado mpo kule. Yaliyobakia huko hata sitawaambieni lakini hawa watu ni ndugu zetu *it's up to us*. (Makofi)

Duniani tunajua iko *western lobby*, Marekani *lobby*, *European lobby they are very powerful. They can encircle anybody*, wanaweza wakatuzunguka sisi hapa yaani tukawa tunasema hawa Wachina kumbe tu kuna watu wanakuzunguka dhidi ya rafiki/ndugu yako wewe unakua hujui unafikiri ni vitu vibaya kumbe watu wanakuzunguka kwa nia yao mbaya. Mimi nahisi Serikali tuangalie sana hawa waliotutawala waliotufanya sisi makoloni yao.

Mtanzania gani anachukua makontena ya bidhaa Marekani kuleta hapa? Yupi anatoka Ufaransa kuleta makontena hapa? Nani anakwenda *shopping* Uingereza kwenda kuleta bidhaa hapa za biashara? Kila mtu anakwenda China. Kama wananchi wote wafanyabiashara tunaelekea huko ila Serikali haiangalii huko, wewe huoni kuna tatizo? Lazima kuna shida mahali.

Hii habari ya China tusii-*neglect* katika Mpango wetu tu-*take opportunity* ambayo ni kubwa sana. *1.4 billion people* huwezi ku-*compare* na ile aliyokuwa anasema rafiki yangu Ali Saleh sijui ya wapi Uturuki; Mturuki anakwenda China kukopa hela, Marekani anakwenda China kukopa hela; China pale sasa hivi uchumi unakwenda mpaka unachemka, inabidi kupoza. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hii ni *opportunity* ambayo kwa kweli tusiipoteze na ni ndugu zetu huo ndiyo ukweli. Hata hivyo, kwenye *negotiations* Watanzania tukae vizuri. Inapofika mahali pa kupanga watu wa kwenda kwenye *negotiations* tupange vizuri.

Zamani tulikuwa tunapeleka watu *senior*, mradi mtu ni *principal* kumbe chuo kikuu alipata *gentleman degree* lakini sasa ameshakuwa *senior* lakini ni *gentleman* bado, makarai matupu. Wenzetu kwenye *negotiations* wanapeleka hata kama ni vijana *first class*, A tupu, unawapanga pale hata kama wamemaliza *university* mwaka jana, mwaka juzi unawa-*train* vizuri wale ndiyo wanakuwa *front thinkers*, wanajua nini cha kufanya. Sasa tusikariri vyeo tu, mimi Mkurugenzi, ulipata nini huko, ulifaulu nini huko? (*Makofi*)

Kwenye *negotiations* tunaangalia *form four* ulipataje? *Form four* makarai matupu unaenda ku-*negotiate* nini? Haiwezekani! Mtanisamehe Waheshimiwa lakini yapo mambo ambayo lazima upeleke *brains* zako maana ni watu wako, *brains* unazi-*forward* pale. Mniwie radhi Waheshimiwa lakini nadhani ndiyo tunashauri hivyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mbaraka Dau nilikutaja, tafadhali.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii. Nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia uzima na afya ili leo tuweze kujadiliana masuala yanayohusu nchi nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana mtoa hoja Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Dkt. Kijaji kwa namna walivyoutendea haki Mpango huu ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu pia ziende kwa Waziri mwenye dhamana ya ujenzi kabla sijaanza kuujadili Mpango wetu huu. Namshukuru sana Waziri mwenye dhamana ya ujenzi, kivuko chetu kile cha Nyamisati kimeshaanza kujengwa na tumeahidiwa mwezi wa pili kitakuwa tayari. Kwa hiyo, nina kila aina ya sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na watu wote pale Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, sasa nianze kuchangia Mpango. Umekuwa ukisisitiza mara kwa mara hapa kuhusu suala la namna gani sisi Wabunge tunaweza tukaingiza *input* zetu ili huu Mpango uwe bora zaidi. Waheshimiwa Wabunge mara nyingi wamekuwa wakizungumza upande wa matumizi zaidi, kila mtu anakuja barabara siji gati kuliko namna gani tunaweza kuboresha Mpango wetu ukawa na mapato zaidi ili kuweza kufidia hii miradi ambayo sote hapa kila mmoja anavuta mradi unaomhusu kwenye Jimbo lake. Mimi nitakuja na mapendekezo ya namna bora ambavyo tunaweza tukauboresha Mpango huu ili Serikali ipate mapato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kwenye eneo la uvuvi wa bahari kuu. Amezungumza kwa muhtasari sana ndugu yangu Mheshimiwa Ally Keissy pale. Kwanza nianze kukushukuru wewe binafsi, ulinifanya mmoja wa wajumbe katika ile Kamati inayochunguza namna gani Serikali inaweza ikanufaika na uvuvi wa bahari kuu, tumekutana na mambo mengi sana na ningeomba sana ile taarifa kama itawezekana tuifanye *public* kwa sababu kuna mambo mazuri mengi sana mle. Hata mimi mwenyewe pamoja na kuwa ni mjumbe basi huwa naihitaji hata kuipitia na kuidurusu lakini inakuwa ni shida kidogo kwa sababu bado haijawa *public*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa kwenye Mpango kwa nukta chache sana, nadhani nukta tatu ama nne kuhusu uvuvi wa bahari kuu. Jambo la kwanza Serikali inaangalia uwezekano wa kujenga bandari ya uvuvi. Jambo la pili kufufua shirika letu lile la meli la *TAFICO*. Jambo la tatu ni namna gani tunaweza tukapata vifaranga vya samaki na namna za kuvifuga kwenye vizimba. Haya yote ni mambo mazuri lakini naomba tuangalie namna gani tunaweza tuka-*prioritize* mambo haya. Tukiwachukua yote kwa ujumla wake inawezekana pengine gharama zikawa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kwanza tu-*focus* kwenye bandari ya uvuvi peke yake, tupate bandari ya uvuvi. Watu wengine walisema kwa nini Bandari ya Dar es Salaam msiweke magati mawili au matatu na kule Zanzibar nako kuwe na gati maalum kwa ajili ya meli za uvuvi, haiendi hivyo. *Typical* bandari ya uvuvi ni *fully fledge* bandari, inakuwa na *logistics center* zake nyuma kule. Samaki huwezi ukawachanganya na bandari ya *cargo*, huku kuna mbolea, huku unashusha sijui *chemical* gani halafu kuna gati lingine tena unashusha bidhaa ya samaki, hatutopata *accreditation* ile ya *European Union* kupeleka vyakula nje kwa sababu kutakuwa na *contamination* kutokana na mazingira ya bandari ya mizigo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapozungumzia bandari ya uvuvi tunazungumzia kitu kikubwa sana, *very complex* na tungeomba Waziri alijue hilo. Kwa bahati mbaya sana mpaka leo hii Serikali bado haijajua hata *site* bandari itajengwa wapi. Tumeshatenga fedha katika bajeti kama tatu zilizopita kwa ajili ya upembuzi yakinifu, walau kupata kujua bandari tunaenda kujenga wapi, Kilwa, Dar es Salaam, Bagamoyo, Mafia au wapi? Mpaka leo hilo tu halijaamuliwa. Bajeti hii tunayoitekeleza tayari kuna fedha za upembuzi yakinifu nadhani shilingi milioni 300 au shilingi 500, *I stand to be corrected*, za namna ambavyo mshauri atapatikana ili aweze kutushauri bandari inajengwa wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa dakika chache sana tuiangalie *overview* ya ile biashara yenyewe ya uvuvi wa bahari kuu. Eneo letu linaloitwa *EEZ (Exclusive Economic Zone)* la Tanzania ni zaidi ya kilomita za mraba 300,000 yaani hiyo ni nchi ndogo 10/15, hilo eneo lote ni la kwetu sisi. Kwa masikitiko makubwa eneo hilo lime-*lay idle*, hakuna kinachoendelea kule kwenye *EEZ* yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amelizungumza Mheshimiwa Ally Saleh pale kwa muhtasari kwamba Serikali na nashukuru Waziri mwenye dhamana yupo hapa, Serikali mwaka 2016 waliweka kitu kinaitwa *royalty* ya 0.4 kwa kila samaki. Samaki wanaovuliwa ni aina ya jodari (*tuna*) basi, soko la dunia halitaki samaki mwingine yoyote asiyekuwa jodari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa walipo-*introduce royalty* ya 0.4 wale wenye meli kubwa ambao ili aje kuvua kwenye pwani yetu (*EEZ*) walikuwa wanalipa leseni moja ni mpaka Dola za Kimarekani 36,000 na kwa wakati mmoja kwenye *EEZ* yetu zinaweza zikawepo kule meli zaidi ya 100, unaweza ukazidisha dola 36,000 mara meli 100, hiyo ni kwa ajili ya leseni tu na tulikuwa tunapata hizo. Hata hivyo, hapa katikati mwaka 2016 tukaweka 0.4 kwa maana katika kila kilo ya jodari 0.4 inabidi iende Serikalini pamoja na yale malipo ya leseni, wale mabwana wakakasirika wakaondoka. Kwa hiyo huu ni mwaka nadhani wa pili au wa tatu, hakuna kinachoendelea kule kwenye *EEZ* yetu na samaki kama wanavyosema watu wengine siyo bidhaa ambayo ni kama dhahabu, ukichimba itaisha, samaki ni wanapita (*gyratory*), usimpovua wewe atakwenda Somalia atavuliwa, kwa hiyo, sisi tunakosa kwenye hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliuliza jambo hili kwenye Kamati na Mheshimiwa Mpango atakumbuka nikaambiwa 0.4 imeshafutwa bwana Dau hujui, toka mwezi wa Nne imefutwa, nikawaambia haiwezekani Bunge la Bajeti tumezungumza 0.4 hapa na Waziri mwenye dhamana akasema tunaangalia uwezekano wa kuifuta hapa katikati, nadhani jana, majuzi nikaambiwa kuna maendeleo

yanaendelea huko 0.4 imefutwa. Sasa naomba jioni tutakapokuja, Mawaziri watakapoanza ku-*react* na hizi taarifa basi watuhakikishie 0.4 imefutwa au haijafutwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watuhakikishie ili tujue kwa sababu tunachopoteza ni kingi na tusipotoza haina maana kwamba, maana yake afadhali ile kauli unayosema Mwalimu Nyerere alisema hii dhahabu kama hatuna ufundi wa kuichimba ikae tu watakuja kuichimba vizazi vijavyo, lakini kwenye samaki hakuko hivyo, usipomvuna wewe ataenda kuvunwa Namibia. Kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa basi atusaidie namna gani ya kuona 0.4 inaondolewa na bandari ya uvuvi mchakato wake unanza mara moja. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hizi tozo kwa ujumla wake naomba Waziri wa Fedha na Mipango aziangalie, hizi *Sectoral Ministries* kila mmoja anakuja na tozo yake, inakuwa ni vurugu! Kwenye utalii kule, sijui *TANAPA* Waziri wa Maliasili na Utalii naye anaweka tozo zake, huku Waziri Mifugo na Uvuvi anaweka tozo huku, sijui Waziri gani naye akiona kidogo tu mambo yanakwenda vibaya anaweka tozo. Kunakuwa na utitiri wa tozo, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, ndiyo waratibu hizi tozo, hizi tozo kadri zinavyozidi kuongezeka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dau naambiwa eti ni kengele ya pili, lakini malizia nakupa dakika mbili umalizie.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi la mwisho kwa dakika moja tu, nilishaongea na Mheshimiwa Waziri Mpango, hii leo naongea mara ya nne na nilimwambia kwenye Kamati sitaongea tena kuhusu suala hili. Kuna chanzo cha mapato kipo Mafia pale ambacho watalii wanatozwa kuingia katika maeneo ya hifadhi ya bahari, kila mtalii analipa dola 24. Tunamwomba achukue

yeye kile chanzo, tunampa sisi chanzo kile aongeze mapato ya Serikali, awaambie *TRA* waende wakakusanye wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, nakushukuru sana kwa nafasi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Hebu hilo la mwisho yaani wakusanye badala ya *TANAPA* au?

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana badala kuna Taasisi inaitwa Hifadhi ya Bahari (*MPRU*) ambao kimsingi wao kazi yao ni kuhifadhi maeneo na mazalia ya samaki, sasa tunapowapa kazi...

**MWENYEKITI:** Badala ya kule kwa Luhaga Mpina enhe?

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Ndiyo, sawasawa.

**MWENYEKITI:** Aaa, sawasawa. (*Kicheko*)

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa badala ya wao kuendelea kukusanya mapato, tunaona ile kazi ya mapato ni kazi ya *TRA*, wafanye *TRA*, halafu sisi tushughulike na uhifadhi.

**MWENYEKITI:** Nimekusikia Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nimekusikia Mheshimiwa. (*Kicheko*)

Wataona wenyewe, maana yake ni Serikali hao hao. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Venance Mwamoto, tafadhali.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze



kuchangia kidogo, nafikiri mchango wangu utakuwa siyo mrefu sana. Kwanza kabisa kama ambavyo wenzangu wametangulia, tupongeze kwa jitihada kubwa ambazo zimefanywa katika Awamu hii, mambo mengi yamefanyika tukianza kwenye majimbo yetu, mambo makubwa yamefanyika ambayo kwa kweli kwa muda mfupi Serikali imeonesha jinsi ambavyo fedha zimetumika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kujikita kwenye viwanda, niipongeze Serikali yetu kwa jinsi ambavyo iliamua kujikita kwenye suala zima la viwanda, kazi imefanyika na niseme wazi kwamba jitihada zimefanyika na viwanda vingi vimeanzishwa. Kikubwa ambacho ningependa kujua, mpaka sasa ni viwanda vingapi tayari vimeshaanzishwa? Kwa maana ya viwanda vikubwa ambavyo vinaenda kusaidia kuuinua uchumi wetu; viwanda vya kati na vidogo na je, sheria tumeshatunga za kulinda viwanda vyetu, kwa mfano, malighafi na upatikanaji wake? Nasema hivi kwa sababu ukiangalia viwanda vingi vitakuwa vikitegemea malighafi aidha kutoka ndani au nje, tumejipangaje kubadili sheria kwa sababu kwenye sheria, nyingi zimebaki kama zilivyokuwa kwa mfano sheria za kusafirisha malighafi nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano kuna Kiwanda kama cha Pareto pale Mafinga. Kiwanda kile kinategemea malighafi ya Tanzania, lakini sheria zamani hazikatazi malighafi hiyo pareto maua yale kusafirishwa nje, kuuzwa nchi zingine na tumeshuhudia sasa kiwanda kama hicho kinakosa malighafi na hivyo kushindwa kujiendesha kama ambavyo inatakiwa. Kwa hiyo, niombe tu tuangalie upya sheria zetu, lakini pia tuangalie hata bei za umeme kwa viwanda vyetu ambavyo vinakuja pamoja na kuwa tuna mategemeo makubwa baada ya kumaliza ujengaji wa bwawa, lakini tunatakiwa tuangalie mapema kwamba tutavilinda vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kodi; tuangalie sasa kama tutakuwa tumejenga viwanda na kuna malighafi ambazo zinatoka nje, tuangalie jinsi ambavyo tunaweza tukasaidia viwanda vyetu kupunguza kodi ili waweze

kuingiza malighafi ili viwanda vyetu vijijendeshe, bila kufanya hivyo itakuwa hakuna tulichokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka tu kujua kwa sababu tuko kwenye Mpango huu, nijue hali ya ushiriki wa watu akinamama na watu wenye ulemavu kwenye viwanda vyetu jinsi ambavyo watalindwa, kwa sababu ukiangalia unaweza ukakuta watu wenye ulemavu hawajawekewa mpango maalum na wao ni binadamu na wengine wana akili zaidi ya watu ambao wazima. Kwa hiyo Serikali iwe na mpango mkakati kabisa kwamba kiasi gani na asilimia ngapi wataajiriwa kwa sababu walio wengi siyo kwamba hawana uwezo kabisa, wana uwezo wa kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa tuangalie vilevile ni kuhusu unyanyaswaji wa wanawake na watoto katika Mpango wetu, kwa sababu ukiangalia wanawake na watoto ni watu ambao wamekuwa wakinyanyaswa kila pande na wao ukiangalia ndiyo ambao wanasaidia kwenye uchumi wetu, hasa huu wa viwanda. Ajira nyingi sana zinategemea akinamama wengi wataajiriwa, lakini tusipowawekea mkakati madhubuti wa kuhakikisha tunalinda usalama wao inawezekana uchumi wetu ukawa na shida. Nasema hivi kwa sababu tumeangalia Jeshi la Polisi ambavyo limekuwa likifanya kuanzisha Dawati la Jinsia jinsi ambavyo limeweza kusaidia kuinua maisha ya mwanamke hasa vijijini na kuongeza pato la watu. Kwa hiyo tuangalie hata katika Viwanda vyetu si mbaya kukawa na kuna Madawati ya Jinsia ili kulinda wafanyakazi na akinamama ambao wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa China mwaka 1978, uchumi wao ulikuwa sawa na sisi sasa, miaka 41 iliyopita, lakini leo wameshakwenda mbali kama ulivyosema na hii siyo kwamba lelemama, kuna vitu vya msingi vimefanyika. Ukiangalia China suala la rushwa hakuna ukikamatwa na rushwa unachinjwa, ukifanya kosa unapata adhabu ambayo inaonekana. Kwa hiyo na sisi lazima tujifunge mkanda, tunaweza tukapata tabu sasa, kwa sababu hata wale waliojenga reli walikuwa wamekuja

wanavaa suruali ambazo zilikuwa zina viraka zinazofanana, lakini leo hii waliumia wale kwa ajili ya watu wengine ambao wanakula bata sasa. Kwa hiyo na sisi haya ambayo yanapita sasa tukubali, kuna maumivu yake kwa sababu ni mambo mapya. Kwa hiyo tukiumia, tukubali kuumia kwa ajili ya vizazi vyetu ambavyo baadaye vitakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Mheshimiwa Rais juzi alivyokuwa ziarani kule mpakani mwa Zambia, alitoa msaada pale, kwa hiyo haya tusishangae, baada ya miaka mitano, kumi ijayo na sisi tutakuwa tunatoa misaada kwenye nchi nyingine badala ya kuendelea kuomba misaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuliongelea ni kwa mujibu wa Sheria za Usajili wa Makampuni, Na. 12 ya mwaka 2002; Kampuni iliyosajiliwa inatakiwa katika kipindi cha kuanzia mwaka mmoja ifanye marejesho kwa Msajili maana yake *BRELA* yapo makampuni mengi yanayotaka kulipa marejesho ya Serikali kwa awamu kama ilivyo katika Mamlaka za *TRA* na Ardhi. Sasa kwa nini Serikali isikubali makampuni hayo yakalipa kwa awamu, kwa sababu ukiangalia kuna utoroshwaji mwingi wa fedha na yanashindwa kulipa, sasa matokeo yake kuna makampuni yanadaiwa mpaka miaka kumi hayajarejesha. Kwa hiyo nafikiri ni vizuri sasa sheria hii ikaangaliwa upya ili wao pia walipe kama vile ambavyo *TRA* inayatoza makampuni yale kulipa kwa awamu kwa sababu mzigo unapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana pamoja na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kazi kubwa ambayo wanafanya, kama wanavyosema wengine ni kwamba mwanzo tulikuwa hatuwaelewi, tulikuwa tunawachukia sana, lakini sasa hivi tunawapongeza, endeleeni kukaza uzi ili nchi hii iende. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwamoto. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nashukuru tunaendelea vizuri na uchangiaji wetu, tutamalizia hili zoezi jioni ya leo, nitawaomba turudi hapa ili tuweze kuwasikia na wenzetu Serikali wakichangia ili tuweze kumaliza vizuri Mpango wetu tukijua kwamba Mpango huu ndiyo unakamilisha ule Mpango wa miaka mitano na ndiyo msingi wa bajeti yetu inayokuja.

Kwa hiyo msemaji Mkuu upande wa Serikali atakuwa ni Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, lakini niseme tu kama kuna upande wa Mawaziri ambapo nadhani ni vizuri pia mkasaidia, hatujibi *as search*, tunapokea lakini yako mambo labda yalisemwa au tulisema ambayo mnadhani kwamba vizuri kidogo katika kupeana uelewa mkayafafanua, nafasi hiyo mimi kama meza nakupeni na mkiona haina haja pia haina shida, ni ninyi kujipanga tu, lakini jioni tutaendelea na uchangiaji wale wote ambao mmeleta majina yenu hapa kuomba kusema, mtapata nafasi kwa uhakika kabisa, wote, ninayo majina yote kabisa.

Jioni nitaanza na Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Nsanzugwanko, Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Frank Mwakajoka, Mheshimiwa Rhoda Kunchela na kadhalika. Kwa hiyo tuwahi tu jioni ili kwa pamoja tuje tuhitimishe uwasilishaji huu muhimu, au mjadala huu muhimu wa ushauri kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudia kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Kessy, alichangia hapa kwamba kwenye mazoezi kule baadhi ya watu ni watoro, baadhi ya watu wanakwenda kuhudhuria mazoezi lakini hawafanyi na kadhalika, ni kweli kutakuwa na safari lakini pia ni kweli kwamba tunafuatilia kwa karibu na tunajua nani anafanya mazoezi, nani anafanya mchezo, tunafahamu. Kwa hiyo wakati huo ukifika tukianza kupunguzana punguzana wala tusilalamike kwa sababu ndiyo hali halisi tunajua kinachoendelea. *(Makofi)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, ningewashauri tuache mambo ya sekondari, sisi ni watu wazima kama tulivyoshauriwa hapa ili tutakapokwenda kule Uganda tunakutana na wenzetu Wabunge wa Kenya, Burundi, Rwanda na kadhalika, isiwe sasa Tanzania ikisimama huku inashindwa, ikisimama sijui kwenye mchezo wa *basketball* inashindwa ikienda *Netball* ni kushindwa, *football* ndiyo usipime. Inakuwa haipendezi hata kidogo, inajenga dharau fulani hivi, sasa kwa nini tudharaulike bwana, bora hata tusiende kuliko kwenda na watu ambao hawafanyi mazoezi ila wanang'ang'ania kwenda kwa sababu zetu zile zile, zile tunazozijuaga sisi wenyewe, zile sababu zipo tunazifahamu lakini pia si ufanye mazoezi kidogo ukienda kule angalau kidogo uweze kuwakilisha Bunge letu na jina letu.

Tunamshukuru sana Mama Kikwete kwa kweli ni mdau sana wa michezo, sasa kama Mama Kikwete anajitahidi. Anajitahidi, anafika na nini sasa wenzangu na mimi hasa upande wa Wabunge akinamama nadhani ni vizuri tukajitahidi kadri inavyowezekana wale ambao tuna nia ya kwenda. *(Makofi)*

Basi, baada ya maneno hayo naomba sasa nitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni ya leo. Wale wa Kamati ya Kanuni tunaendelea na kikao kama kawaida kwenye ukumbi wetu, kwa hiyo tukitoka hapa tunaunganisha kikao cha Kamati ya Kanuni. Pia niwakumbushe Waheshimiwa wale ambao mna mapendekezo ya mabadiliko ya Kanuni ndiyo wakati wake, muwapatie tu Wajumbe wa Kamati ya Kanuni waje nayo.

*(Saa 6.56 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

### **KAMATI YA MIPANGO**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea Subiri! Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Saba Kikao cha Tano, sasa Kamati ya Bunge Zima.

Waheshimiwa Wabunge tukae, sasa Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na utaratibu wetu wa asubuhi, nilishamtaja Mheshimiwa Cecilia Paresso nakupa dakika kumi!

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa na nashukuru kwa kuwa mchangiaji wa kwanza jioni hii. Dhima ya Mpango wetu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano ni kuangalia suala zima la uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi huu wa viwanda utaendana na ukuaji wa uchumi lakini na maendeleo ya watu. Tunajadili Mpango huo mwisho wa miaka mitano, ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani ingekuwa ni vema sana Serikali ikajitathmini katika miaka minne ya utekelezaji wa Mpango; je, tumetekeleza kwa kiwango kipi, tumekwama wapi na tunafikiri nini turekebishe ili yale malengo tuliyojiwekea kwa miaka mitano sasa tuuweke kwenye Mpango huu ambao umebaki wa mwaka mmoja ili kufidia kuziba mapungufu yaliyojitokeza katika Mpango uliopita. Nilidhani wangepanya hivi ingeweza kusaidia sana kujipima kwamba, katika miaka mitano mipango yetu ya miaka mitano ni kiwango gani tupo na tunaendelea vipi, hali yetu ya uchumi ikoje, maendeleo ya watu wetu kwa ujumla yakoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni dai la muda mrefu hasa Kambi ya Upinzani, tumekuwa tukidai sana kuwepo na sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Taifa. Tumedai muda mrefu na hii sheria itasaidi mfano tukifanya tathmini tukaona kuna upungufu fulani na upungufu kama unahitajika kuzibwa na sheria, basi ni muhimu sasa tukawa na sheria ya utekelezaji wa Mpango huu. Tukiwa na sheria hii maana yake pia tutakuwa na uwajibikaji wa kutosha kwa watekelezaji wa Mpango huu lakini tutasaidia kufanya *reallocation* mbalimbali za bajeti ambazo ziko nje ya mpango. Maana yake mpango ule ambao utakuwa umepitishwa Bungeni kama tutakuwa tuna sheria kwa kiwango kikubwa itaziba hii mianya mingine ya kuibua miradi mingine au mipango mingine mingi mingi ambayo kwa kweli kwa kiasi kikubwa inaenda kuathiri bajeti ambayo tumejiwekea au bajeti ambayo imepitishwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama nilivyosema tukiwa na sheria kutakuwa na uwajibikaji wa kutosha, Serikali itawajibika kwa kuhakikisha kwa kweli mipango inatekelezwa kwa kiwango kikubwa na kwa asilimia hata mia moja ikiwezekana inaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kutokutekelezwa kwa miradi ya maendeleo. Tumeona, tunashindwa kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo kwa sababu

tunakuwa na mipango mingi ambayo haiendani na bajeti, haiendani na makusanyo yetu ya ndani, lakini tunakuwa na mipango mingi na miradi mingine mikubwa ambayo kwa kweli kwa kiwango kikubwa hatutaweza kutokana na fedha zetu kutekeleza. Ndiyo maana nikatoa rai hapa mwanzo kwamba ni lazima tufanye kwanza tathmini tuone tumejikwaa wapi, tumeshindwa nini ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia Bunge limekuwa likiidhinisha bajeti hapa lakini utekelezaji wa bajeti hiyo hasa kwenye miradi ya maendeleo kwa kweli ni kiwango cha chini sana. Ukirejea hotuba ya Kambi yetu ya Upinzani inaeleza mfano, kwenye Wizara ya Kilimo na Sekta nzima ya kilimo. Tukielewa umuhimu wa Sekta ya Kilimo hapa nchini tunajua ndiyo watazania wengi wanategemea kilimo lakini kilimo hiki ndiyo tunategemea. Kama tunataka viwanda maana yake tunategemea kilimo tupate malighafi, viwanda viweze kuendelea na hatimaye hicho tunachokisema kwamba tunataka uchumi wa viwanda ili kuchochea maendeleo ya watu na hali ya uchumi kwa ujumla tuweze kufikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakuwa hatutekelezi miradi ya maendeleo, kama tutakuwa Bunge lako linaidhinisha bajeti hapa halafu hazifiki kwenye wizara husika maana yake tutakuwa hatupigi hatua tunarudi nyuma. Kwa hiyo, ni muhimu sana sana tukaangalia kuwa na miradi michache ambayo tunajua tunaweza kutekeleza na miradi hiyo ikapitishiwa fedha hapa Bungeni na kwa kweli ikatoka kwa asilimia mia moja. Kwa hiyo, ukienda kwenye Wizara ya Kilimo, ukienda kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ukienda kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara, wizara zote ambazo zinafungamana na hicho ambacho tunakitaka, uchumi wa viwanda zote fedha zake za miradi ya maendeleo kwa kweli hazijafika hata asilimia 60, 70 au asilimia 100. Kwa hiyo, ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, Serikali sasa hivi inatekeleza miradi mikubwa mitatu, kuna *Stiegler's*



*Gorge*, kuna SGR na ununuzi wa ndege, hii yote ni miradi mikubwa ambayo inahitaji fedha nyingi. Sasa tunakuwa na miradi mikubwa kwa mara moja ambayo inahitaji fedha nyingi maana yake ni kwamba fedha zozote zinazopatikana zinaenda kwenye miradi mikubwa. Halafu huku kwingine kwenye miradi midogo midogo ambayo kwa kiwango kikubwa ina mgusa mwananchi wa kawaida haifikiwi na hatuwafikii watu wa kawaida. Kwa hiyo, rai yangu kwa Serikali kwamba mnapokuwa na miradi mikubwa mje na mkakati wa ziada wa kuonesha ni namna gani miradi mikubwa inaweza ikatekelezwa, ni namna gani itakuwa *financed* ili miradi hii iweze kutekelezwa. Ni muhimu sana ili tusiweze kuathiri mambo mengine, utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirudi kwenye Serikali zetu za Mitaa kuna hali mbaya sana. Tuligemea kwamba, na tunategemea kwamba Serikali za Mitaa ndiyo kwa kiwango kikubwa ndiyo wananchi wako kule, ndiyo kwa kiwango kikubwa tunategemea miradi muhimu ambayo inamgusa mwananchi mmoja mmoja; maji, barabara, kilimo, masoko, kwa kiwango kikubwa mwananchi kule kwenye Serikali za Mitaa ndiyo inamgusa. Serikali za Mitaa hizi sasa hivi zimekuwa hoi bin taabani, hakuna kitu, fedha zote za makusanyo zimebebwa. (Makofi)

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy taarifa nimekuona.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba anasema Serikali yetu haipeleki miradi katika wilaya. Tangu uhuru haijajengwa hospitali za wilaya 67, tumejenga zahanati hazina hesabu, sasa nashangaa anasema hatupeleki wakati miaka yote 45 sijui hakuna... kama Namanyere tulikuwa hatuna hospitali ya wilaya acha kwake. Juzi ametoa hospitali ya wilaya pale Ubungo tena kwa mpinzani, sasa anasema wapi hatupeleki miradi midogo midogo!

**MWENYEKITI:** Amesahau kidogo unajua tena hayo mambo, Mheshimiwa Cecilia si unajua alikuwa kwenye utaratibu maalum! Mheshimiwa Cecilia. *(Kicheko)*

Tunatumaini mjukuu hajambo! Endelea Mheshimiwa Cecilia. *(Kicheko)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante taarifa ya Mheshimiwa Keissy siipokei na siipokei kwanini! Ukifanya tathmini kwa sababu si toka tumepata uhuru nchi hii inaongozwa na Chama cha Mapinduzi, nchi hii ndiyo inakusanya kodi. Ukifanya tathmini toka tumepata uhuru mpaka leo yaani tulipaswa Tanzania hii kuwa ulaya, kama kwingine maana yake ni tumechelewa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unapoongelea Namanyere ndiyo wamepata hospitali ya wilaya wamechelewa sana, walipaswa wapate kwenye miaka labda ya 80 huko, 70, miaka ya 90 mnaongelea habari za hospitali za rufaa kwenye maeneo yenu sasa namna gani ya kuboresha. Kwa hiyo, kwa mtazamo wa kwamba ipo inafanyika, imechelewa kufanyika, ilipaswa ifanyike mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niendeleo kwenye Serikali zetu za Mitaa nadhani ni rai sasa kwa Serikali kuzitazama upya Serikali zetu za Mitaa, vile vyanzo vingi ambavyo mmevinyang'anya mvirudishie ili viweze kujiendesha. Namna gani itaendesha, namna gani itatumikia wananchi, leo kuna baadhi ya halmashauri hata Vikao vya Baraza la Madiwani kwa mujibu wa sheria havifanyiki kwa sababu hakuna fedha, havifanyiki kwa sababu mapato ni madogo, yale yanayopatikana kidogo yanachuliwa. Siyo tu kuchukuliwa wakati mwingine maagizo yanayokuja kwa kiwango kikubwa kinaenda kufanya nini, kuharibu bajeti ambayo imewekwa kwenye Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, bado Serikali zetu za mitaa zina hali mbaya zinapaswa kwa kweli kwa kiwango kikubwa kubebwa na kusaidiwa na kurudishiwa fedha zile ambazo zitakusanywa na Serikali Kuu, zinazotakiwa kurudi kwa mujibu wa sheria

zikarudi zikatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu yalikuwa ni hayo machache, nashukuru sana kwa nafasi ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Pareso nakushukuru sana. Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King na Mheshimiwa Rhoda ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi hii ili nichanguie mpango ambao umeletwa kwetu kwa mujibu wa Ibara ya 94 kama ilivyo kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauunga mkono sana mpango huu, kwa sababu ndiyo utaratibu wetu humu Bungeni, kwamba mara bajeti inayofuata, lazima kuwe na mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Mpango, ameeleza vizuri sana naomba nisome kidogo tu. Katika mwaka 2021, Serikali itasimamia vipaumbele vifuatavyo; kuimarisha na kusimamia mfumo wa ukusanyaji wa mapato, lakini akaenda mbali zaidi, akasema, malengo ya mpango wa bajeti yanalenga kuimarisha makusanyo kwa kutekeleza hatua za kiutawala zikiwemo kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa wawekezaji kuimarisha uzimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, lakini akaendelea akasema, usimamizi wa sheria ya kodi, kupunguza upotevu wa mapato na kuyaanisha na kupunguza tozo ya ada mbalimbali zikiwemo za wakala wa Serikali ya matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la nidhamu ya matumizi ya umma ya fedha za Serikali, nianze kwanza kukupongeza sana sana Mheshimiwa Spika wetu ambaye

ni Mwenyekiti wetu kwa kikao cha leo, kwa mambo matatu ambayo wewe umeonyesha kwa dhahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, jambo la kutuletea hizi *tabulates* hizi ndani ya Bunge, umepunguza sana sana matumizi ya karatasi ambayo yalikuwa yanatumia fedha nyingi sana za Serikali, ilielezwa kwamba matumizi yake kwa mwaka ni karibu bilioni 1.2. Sasa bilioni 1. 2 kama fedha hizi leo hatutumii tena, zitakwenda kwenye mipango mingine, kwa hiyo, nikushukuru sana pamoja na Ofisi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, hapo awali, Serikali tukiwa Bungeni, Wabunge wako, tulikuwa tunafanya vikao vyetu wakati wa kamati, tunafanya vikao vyetu nje ya maeneo ya Bunge, tulikuwa tunafanya *UDOM*, wengine wanakwenda Hazina, wengine sijui wanakwenda Mipango, wengine wapi, hiyo yote ilikuwa ni kutumia fedha visivyo, fedha za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa busara zako, ukaamua kwamba kuanzia sasa Kamati zote za Bunge, shughuli zake za kibunge zitafanyika katika majengo ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru sana, huwezi ukajua, kwa sababu huwezi kuiona moja kwa moja, fedha ambazo tulikuwa tunazitumia, hata sisi wenyewe Wabunge, tulikuwa tunatoka huko tuliko, tunakwenda *UDOM*, mara unapotea mara unarudi, unakuja tena hapa, mara unakwenda, matumizi yale tulikuwa tunatumia fedha lakini tunatumia na muda, kwa sasa, muda wetu ni mfupi sana unaotumika, tunatumia muda mwingi lakini tunatumia vizuri, kwa sababu shughuli za kamati za Bunge zinafanyika ndani ya eneo la Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, mtu mwingine anaweza akaona ni kitu cha kawaida, lakini siyo cha kawaida, ukiwa na miaka 10, miaka 20, umri unakwenda, kupanda zile ngazi za kwenda ghorofa ya nne, hasa mzee

wangu Mheshimiwa Lubeleje, bahati nzuri sijui leo hayupo, kupanda zile ngazi kwenda ghorofa ya nne, iikuwa ni *issue*.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa busara zako na ofisi yako, hivi sasa leo kwenye jengo la utawala, lakini pia hata kwenye eneo ambalo kamati za Bunge zinafanyika, kote kuna *lift*, tunakushukuru sana sana kwa kuboresha.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishauri Serikali, kama tunataka tukusanye mapato yetu vizuri, yapo maeneo ambayo Serikali imeyaacha. Kwa mfano, ukipita hii njia ya kwenda Dar es Salaam, utakuna na malori ya mafuta, utakutana na malori ya mizigo, yenye namba, siyo za Tanzania, yenye namba za nchi za jirani, lakini ukienda kwenye ule mlango wa hicho kichwa cha gari, mmiliki wa hilo gari, tuna jina la mtanzania!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali inapoteza mapato mengi kweli kweli na hili eneo hili, ukienda kwa wale wenywe wanakwambia kwamba malori haya yanaposajiliwa nje, Serikali inakosa mapato ya ndani, Serikali inakosa fedha ambazo malori hayo yangeweza kununua mafuta hapa Tanzania, tunakosa ajira na vitu vingine vingi.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali, tunajuliza tu, hivi kwanini haya malori, kama lori hili lilikuwa la Mheshimiwa Ndassa, au lori hili lilikuwa la Mheshimiwa Ndugai la mafuta, badala ya kulisajili Tanzania nakwenda kulisajili nchi za nje, lazima kutakuwa na tatizo tu, lakini nyumbani kwangu ni Dar es Salaam, lakini lori lakwangu, ambalo nikilisajili kwa Tanzania, Tanzania itapata mapato. Mafuta yale, maana yake sasa hivi utaratibu wanaofanya, yale mafuta, hawachukui tena hapa, wanachukua hokohuko, wanakuja wamejaza, kama lita 400, wanakuja kuchukua mizigo na kurudi, mafuta hayo lita 400, ambayo sisi tunatumia kama kwenye *road tall*, sasa mapato hayo yanapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali, hebu turudi nyuma, ili tushauriane vizuri zaidi, ili malori haya ya mafuta na malori ya mizigo, yaweze kusajiliwa hapa, kama kuna tatizo sehemu fulani, basi turekebishe, kwa sababu hicho ni moja ya chanzo cha mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, ili twende vizuri zaidi, katika kusimamia nidhamu na matumizi ya Serikali na haya mapato ili lazima yapatikane, lazima kuna mambo ya kufanya, ya kusimamia. Suala zima la rushwa, rushwa bado ipo, kuna mianya mingi ya rushwa ambayo inasababisha mapato yetu kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali, suala zima la ruswa, lakini pia uaminifu kwa wafanyanyazi, uzalendo kwa wafanyakazi wa Serikali, kwa sababu tunataka mapato yetu yaende mbele zaidi, lakini tukitazama kwa miradi ambayo tumeiainisha miradi mikubwa hii, reli, bwawa, ndege na mengine, bila kuwa na vyanzo imara vya mapato, hatuwezi kufikia ile *target* ambayo tunataka ifikie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Serikali, wale watu wote ambao wanasimamia maeneo hayo, lazima nidhamu ya matumizi iwepo, wizi, rushwa usipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho, kwa sababu kengele imelia, nikuombe sana na Bunge letu Tukufu, *TRA* huwa tunawapa malengo, kwamba lengo lenu kwa mwezi huu ni kiasi fulani, halamshauri zetu lengo lenu ni kiasi fulani, sijui, sina uhakika, kama maeneo mengine yana utaratibu wa kuwekewa malengo. Sasa ombi langu, kwa sababu tunazo taasisi za Serikali, kama *TANAPA*, Ngorongoro na mengine, hebu, lazima tuwe na kautaratibu kazuri ka kuweka, siyo kuweka wao, kwa sababu taasisi hizi tunategemea ili ziongeze pato letu, tunategemea zitoe gawio, sasa kama watakuwa wanajipangia wao bajeti yao, *target* yao kwamba wakati wanaweza wakaenda mbele zaidi, kama walivyofanya *TCRA* Septemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuwa wamejipangia chini lakini wakakusanya trioni 1.8, au 1.7. Kwa hiyo, hata mashirika haya ya umma, ambayo tunategemea tupate gawio kutoka kwa hizi taasisi, bado malengo yao yanaweza Serikali ikayapitia kupita kwa TR, akapitia akasema, hapa wewe hapana umedanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima pia, hilo gawio, siyo wao ndiyo waseme kwamba sisi tutatoa gawio hili, hapana, Serikali iseme! Kwa kufanya hivyo, mtakuwa mmewasaidia kupunguza matumizi yasiyokuwa na utaratibu tukiaacha wakajiendea tu yale matarajio yetu hatuwezi kuyafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo, naipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana anayofanya. Nje na ndani sisi sote tunakubali kwamba hili ni jembe la Tanzania, siyo vinginevyo. Nawaomba hata ndugu zetu, hata kama hutaki kukubali, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ni Rais wa nchi hii, anafanya kazi nzuri, kla mtu anaona na kusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watu wa nje wanasifia, wewe uliyeko ndani utashindwa kusifia? Basi hata kama hutaki kusema, hata ukiwa nje sema basi kwamba Mheshimiwa Dkt. John Magufuli Pombe hoyee! Hata ukiwa nje!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndassa na hasa ulivyomalizia, tunakushukuru sana kumkumbuka Mheshimiwa Rais wetu katika jambo hili la Mpango. Mheshimiwa Ali Hassan King nilishakutaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Rhoda na Mheshimiwa Nsanzugwanko ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kupata pumzi zake na leo kusimama hapa, lakini pia namshukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Mpango wa Maendeleo. Kabla ya yote, napenda niipongese Serikali kwa hatua kubwa sana za maendeleo ambazo imechukua na sasa tunaona kwamba hatua tunazokwenda, tunakwenda vizuri. Kwa hiyo, naishukuru sana Wizara ya Fedha pamoja na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli. Tunamwombea Mungu aendelee kuchapa kazi na aendelee kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemu unasema kwamba penye nia pana njia. Kwa nini nikasema hayo? Ukiwa una nia ya kitu, basi njia ya kulitekeleza kile kitu itatokea. Sasa naishauri Serikali, tumeweka shilingi trilioni 107 katika Mpango ule wa Miaka Mitano kwenye ugharamiaji, lakini tukaweka shilingi trilioni 59 kwa ajili ya Serikali kwamba ndio itagharamia huo Mpango; lakini shilingi trilioni 48 ndizo ambazo zitatumika na Sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nije katika sekta binafsi, je, kuna jitihada za kutosha kuhamasisha sekta hii kugharamia huu Mpango? Kwa sababu cha Serikali tunakijua, tutakuja kwenye bajeti hapa, tutapitiasha mipango kwenye bajeti, itakapopita tutajua kwamba hii ni kasma ya Serikali katika kugharamia Mpango, tumeiona. Isipokuwa hatuioni wazi wazi sekta binafsi inavyotumika kugharamia Mpango huu. Kwa maana hiyo, hata hizi *figures* ambazo tumeziweka, ina maana labda tuje tujumuishe mwisho baada ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali iwe na umakini na ichukue hatua za kutosha katika kuhamasisha sekta binafsi. Sekta binafsi hazijahamasishwa vya kusha na huu Mpango ni mipango yetu, imewekwa kwa ajili ya Serikali na sekta binafsi. Kwa hiyo, hilo nilikuwa naliomba. Kwa mwaka ukichukua *average*, sekta binafsi ilipaswa ichangie kwenye Mpango huu shilingi trilioni 9.6.



Sasa je, tunazipata hizi? Kama tunazipata, sasa tumeshakwenda miaka mitatu, tumebakia na miaka miwili, hizo shilingi trilion 48 za sekta binafsi zitapatikana? Kwa hiyo, naishauri na naiomba Serikali itumie kasi kubwa zaidi katika kuhamasisha miradi ambayo imepangwa kufanywa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, kuna msemu unaitwa nia na azma. Azma, unaweza ukaazimia tu, lakini nia unatia nia wakati kile kitendo kiko njiani kwenye kukitekeleza. Nimesema hivi kwa sababu kuna mambo humu yanaonesha kama ni azma siyo ya nia. Huu Mpango umeandikwa kwa ajili ya mwaka unaokuja. Sasa kuna mambo yameandikwa lakini utekelezaji wake huwezi kuja kuyaona, kwa sababu yatafanywa na sekta binafsi. Sasa naiomba Serikali ijaribu kuangalia kitu ambacho wana nia nacho, kile cha azma tukiache kule kwenye Mpango Mkuu, yale mambo ni mengi, sasa mengine yameazimiwa, lakini hayajitiliwa nia kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee kitu kimoja katika msemu huu, kuna kitu kwa Kiingereza wanaita *scope*. Umetajwa mradi hapa wa bandari ya uvuvi wa bahari kuu, ununuzi wa meli; najjuliza, hii *scope* itakuwemo ndani ya mwaka unaokuja yote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa wa 66 umetajwa uvuvi wa bahari kuu katika kitabu cha Mpango. Sasa kama kitu tuna nia nacho, basi tukiandike kile ambacho tuna nia nacho kuliko tukiweka *scope* kubwa halafu baadaye tukaja kushindwa kuifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, naishukuru Serikali kwa kuleta Mpango huu na kuyaona hayo mengine na kuyaweka, lakini tunahitaji tuboreshe. Tuweke kitu ambacho kitafanyika kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni mambo mawili, bandari zetu na reli. Tunajenga reli, ni sawa, ni kitu kizuri, lakini mapato

ambayo tulitarajia tuyapate kule yalikuwa ni makubwa. *Speed* ambayo tunaenda nayo au tuliyoanza nayo nahisi bado ni ndogo. Kwa sababu tulisema itakapofika mwaka 2025, tuwe tuna kipato cha kati. Mwaka 2025 kwa mujibu wa Mpango huu, iwe tuna ukuaji wa asilimia 10. Itatoka vipi hiyo asilimia 10? Ni kama tutaziweka bandari zetu vizuri pamoja na reli. Angalau hii mipango imepangwa humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaweza ikaja ikatufungua katika kufikia hiyo asilimia 10, lakini Mpango huu wa miaka mitano ambao tumeenda nao tuliolenga hiyo asilimia 10, sasa tumebakia na miaka miwili: Je, tunaweza tukaifikia hii asilimia 10? Kama tunataka kuifikia, hata kama kwa kuchelewa kidogo, basi tujaribu kuangalia bandari zetu pamoja na reli ambazo zitachukua mzigo kupeleka nje. Tanzania ni nchi ambayo imebarikiwa, iko katika eneo zuri, tuna majirani ambao wanatutumia vizuri. Kwa hiyo, nasi ili tuweze kupata uchumi wa nchi hizo, ina maana ni lazima bandari zetu na reli ziwe zinakwenda sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, niongelee viwanja vya ndege na ununuzi wa ndege. Tunaishukuru Serikali, ni kweli tumenunua ndege, tunapongeza, lakini bado zile ndege haziko *busy* vya kutosha. Ili ndege ziwe zinaleta faida na ufanisi, ina maana kwamba ziwe angani, zisiwe kwenye zimepaki. Sasa ndege zetu zinapaki sana. Tatizo ni kitu gani? Ni viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru viwanja vya ndege vya kanda vimejengwa vikubwa ambapo ndege zetu zinakwenda, lakini tujaribu kuwa na viwanja vya ndege vikubwa vya mikoa ili hizi ndege nazo zitumike vizuri ziweze kusaidia uchumi katika nchi hii. Kwa hiyo, Serikali imesema kwamba itasimika taa za kuongezea ndege, ndio; lakini tujaribua kuangalia kwa mikoa sasa. Kanda ya Kusini tumeona, Kaskazini kuna kiwanja kikubwa, tumekiona; Kanda ya Kati, kitakuwepo kiwanja hapa na hiki kingine kimeboreshwa; lakini tujaribu kutizama kwa mikoa, kwa sababu huu uchumi wetu tunaotaka uende, kama

tutakuwa na hizi ndege na viwanja vya ndege vikikaa sawa, tutakuwa tunao uwezo mkubwa sana wa kukuza mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimekusudia niliongelee ni uvuvi wa bahari kuu. Uvuvi wa bahari kuu ni sehemu ambayo hatujaenda na mkakati mzuri wa kuweza kusema kwamba tutakwenda kuukamata uvuvi huo wa bahari kuu au uchumi huo unaopatikana kutokana na uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *page* ya 66 amesema Mheshimiwa Dkt. Mpango kwamba wao watajenga bandari au Serikali itajenga bandari, itanunua meli za uvuvi. Tulikuwa tunaomba ingeshirikishwa na sekta binafsi. Acha Serikali ijenge bandari, lakini ununuzi wa meli kwa nini tusiachie sekta binafsi? Kwa sababu kujenga bandari peke yake ni shughuli; na kama nilivyosema kwamba hata hapa *scope* yake mimi kidogo naona haikukaa vizuri sana, kwa sababu limesemwa jambo moja pana sana na kutekelezeka kwake katika Mpango na bajeti hii nahisi itakuwa siyo rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali ijaribu kubinafsisha baadhi ya mambo, siyo lazima kwamba Serikali inunue meli, inaweza ikaweka hayo mazingira mazuri kwa ajili ya upatikanaji wa huo uvuvi wa bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine katika uvuvi wa bahari kuu, naiomba sana Serikali itoe tamko au iseme wazi, ule mrahaba wa 0.4; mrahaba ule unavunja shughuli zote za uvuvi wa bahari kuu. Tulikuwa tunapokea meli 81 ambapo kila meli inalipa dola 36,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi baada ya kuweka huo mrahaba, hakuna meli zinazokuja. Hiyo imeweka kwa Kanuni. Sasa tulikuwa tunaomba Serikali hebu iwe wazi, iondoe hicho kitu, *at least* tuwe tuweze kupata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza katika hotuba yake aliyoitoa ukurasa wa sita, alizungumzia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali King, malizia sasa hapo.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono...

**MWENYEKITI:** Nasema malizia dakika zimeisha.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ingeweza kukusanya mapato mazuri sana kutokana na hiko kitu. Kwa hiyo Serikali iwe wazi, hiyo Kanuni kama ipo ieondolewe kwa sababu tunakosa uchumi kutokana na uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ahsante sana.  
*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan King. Mheshimiwa Rhoda nilikutaja, dakika tano, utafuata Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami niweze kuchangia kidogo Mpango. Nitachangia katika maeneo mawili au matatu, lakini jambo la kwanza nilitaka kuzungumzia kupitia hiki kitabu cha Mpango; ukisoma ukurasa wa 10 wameelezea maendeleo ya miundombinu katika Taifa letu. Nami niseme, Mheshimiwa Waziri amesainishaa baadhi ya mikoa ambayo mpaka sasa hakuna muunganiko wa lami kwa maana ya mikoa, hasa ukiangalia Mkoa wa Tabora, Ruvuma, Lindi, Mtwara pamoja na Tabora, Katavi, Kigoma na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kupitia huu Mpango, kwa sababu katika mikoa hii bado kuna changamoto ya miunganiko hii ya barabara; na jambo hili la suala la miundombinu katika hii mikoa ambayo imebaki nyuma, inaleta ukakasi na inaendelea kuwatesa wananchi kwa maana ya kwamba wanashindwa kufanya biashara na ukizingatia katika kanda hizi, asilimia kubwa ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Mpango huu, kwa sababu umeainisha kabisa kwamba katika mikoa hii imebaki nyuma ili sasa wakazi hawa wa mikoa hii nao wapate ahueni ya maisha kupitia masuala ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia masuala ya fidia, miundombinu ya barabara nilitamani sana iendane na masuala ya kufungamanisha uchumi wao na wananchi, kwa maana tunaposema maendeleo ya vitu, iendane sambamba na maendeleo ya uchumi wa wananchi, kwa maana ya *personal development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika maeneo mengi ambayo yanahusiana na masuala ya fidia kwa maana ya wananchi ambao walikumbwa na bomoa bomoa katika mikoa mbalimbali, kwa mfano Mkoa wa Mwanza, Dar es Salaam, Katavi na mikoa mingine ambayo bomoa bomoa imepita; ni kweli wananchi wanazihitaji barabara lakini katika mikoa ambayo bomoa bomoa imepita wananchi wengi wamebaki ni masikini. Sasa lengo la Serikali ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu uchumi mnaosema umekua kwa asilimia 7.0 ni uchumi wa aina gani? Tunahitaji kuona mafanikio au uchumi wa wananchi unakwenda moja kwa moja kwa wananchi kwa maana ya kwamba msivunjie nyumba wananchi ambao wamejenga kwa gharama kubwa, leo wanaishi katika nyumba za kupanga. Katika jambo hili mnapokuwa mnafanya tathmini na hata wananchi ambao wanakuwa wameachwa, wameshindwa kufanyiwa tathimini, mweze kuwalipa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo suala la uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Jambo hili limekuwa ni changamoto na mpaka sasa kuna taharuki kwa wananchi ambao waliingia kwenye mchakato huo. Kwa hiyo, naiomba Serikali, kwa sbabu mnatangaza amani ambapo mnatumia nguvu kubwa kuwaaminisha watu kwamba katika uchaguzi huu kila kitu kiko sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makovu na majeraha ya watu ambao wameumia kwenye uchaguzi huu *especially* katika Mkoa wangu wa Katavi, tarehe 5 Novemba, 2019 Mtendaji aliagiza watu wakawavamie vijana wa CHADEMA; na mpaka sasa kuna kijana ambaye anaitwa Dominic Bazilio Mwila alipigwa na Mgambo mpaka akafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme katika hayo marekebisho mnayoyatoa, kwamba tunahitaji kufanya maridhiano ya pamoja, naomba kabisa, kama kweli mnahitaji kuwa na maridhiano ya pamoja na kuwe na amani katika Taifa hili, mwache kuumiza watu na majeraha ambayo wanayapata. Leo hii tutarudi kwenye uchaguzi, lakini watu wana majeraha, watu wameumizwa, watu wako ndani na siyo katika Mkoa wa Katavi tu peke yake...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rhoda, mtu alipigwa na mgambo huko kwa mambo yao huko. Sasa ukituambia au ukiwaambia waache, sasa kweli unaamini hawa wamemtuma huyo mgambo amuue huyo ndugu yetu! Endelea tu kuchangia.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaendana sambamba kabisa na masuala ya uchaguzi, ndiyo maana nikasema, kama mnahitaji amani mnayoitangaza, wasimamizi na wahusika waliotumia mamlaka yao kufanya majanga haya kwenye maeneo mbalimbali, siyo mkoa wa Katavi peke yake, mpaka na mikoa mingine, naomba kabisa katika masuala ya maridhiano kwenye mambo haya ya suala la uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tupunguze majeraha na kutumia nguvu ambayo Serikali inatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika maeneo ambayo kuna upungufu, hawa Watendaji au Makatibu Tarafa, Wasimamizi Uchaguzi...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Rhoda, kuna taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa Mheshimiwa Rhoda taarifa kwamba kwanza tuwe wakweli kwenye Bunge hili, suala la kusema kwamba watu wanauawa, kulikuwa hakuna uchaguzi sehemu yoyote unaofanyika, kulikuwa kilichofanyika ni ujazaji wa fomu sasa huyo mtu aliyenda kuuawa kwa kujaza fomu, kulikuwa kumetokea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine hapa jamani tuwe tunasema ukweli. Haya mambo, vitu vinaenda kwenye nchi za watu. Tanzania inachafuka kwa mambo ya uongo. Hakuna uchaguzi uliofanyika, ni ujazaji wa fomu. Huyu mtu aliuawa wapi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** inawezekana walikuwa wanagombea mpango kando au nini, ndiyo anachosema Mheshimiwa Rhoda. Malizia, bado dakika moja tu.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo na mchango wangu. Ninachokiongelea hapa, kifo cha mtu huyu kinahusishwa na masuala ya uchaguzi kwa sababu kama nilivyosema mwamzo, Katibu Tarafa pamoja na Watendaji walitoa magizo kwenda kuwashughulikia wagombea CHADEMA.

Kwa hiyo, kesi ipo, Ndiyo maana nasema katika maridhiano haya, katika mipango ya Serikali kuhakikisha mnatuliza uchafuzi uliotokea, naomba kabisa m-*deal*/katika maeneo ambayo kweli hali siyo shwari na Serikali ione haja ya kuweza kutatua migogoro ambayao ipo na inaendelea. (*Makofi*)

(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Kama Serikali ingekuwa na mkono wake, mbona kuna kesi sasa? Hiyo inadhahirisha kwamba haki ina-*take place*. Mtu anayeua, hilo lake hilo.

Mheshimiwa Frank Mwakajoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia siku ya leo. Nafikiri leo tunajadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa. Nina mambo matatu ambayo nataka kujadili siku ya leo. Jambo la kwanza kabisa, nataka kuanza na Utawala Bora. Tunavyojadili Mpango, tunajadili mambo muhimu sana kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli tu ni kwamba utawala bora ndiyo itakuwa dira na itakuwa mwongozo mzuri sana kuhakikisha kwamba tunatekeleza Mapendekezo ya Mpango huu ambao tunajadili siku ya leo. Kama hatutaweza kulinda utawala bora katika Taifa hili, tutakuwa tunafanya mchezo ambao hautaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza haya kwa sababu, ili wawekezaji waweze kufika katika nchi, hii ni lazima kuhakikisha kwamba utawala bora unakuwa ni kipaumbele, pia utulivu na amani katika nchi yetu lazima viwe kipaumbele zaidi. Ninazungumzia utawala bora kwa sababu ni lazima tuhakikishe kwamba sheria zinasimamiwa vizuri na zinafuatwa katika Taifa hili.



Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuzungumzia tu kuhusiana na suala la mchakato wa uchaguzi ambao ulikuwa unaendelea kwenye nchi yetu na ambao unaendelea mpaka sasa hivi. Nimemsikia Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI akizungumzia hali halisi ya kwamba wale wote waliojaza fomu na kurudisha na wale ambao hawakuteuliwa lakini walijaza fomu na kurudisha, waendeleo na uchaguzi. Yako matatizo mengi sana yaliyojitokeza kwenye mchakato huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kabisa, kwa mfano ukifika kwenye Mji wangu wa Tunduma na Wilaya ya Mbozi, kuna baadhi ya Kata kama sita Watendaji hawakuonekana kabisa na hakuna aliyechukua fomu katika maeneo hayo. Kwa hiyo, fomu hazikuchukuliwa kwa sababu milango ilikuwa imefungwa na hakuna mtu yeyote aliyepata fomu. Watu walishinda pale kuanzia asubuhi mpaka jioni na maeneo mengine ambamo Watendaji walikutwa, waliwaita Polisi wakawakamata na wananchi sasa hivi wanasota wako rumande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna matatizo makubwa sana. Tulikuwa tunataka tupate ufafanuzi, kwa mfano yale maeneo ambayo watu hawakupewa ruhusa kabisa ya kwenda kuchukua fomu, namna gani watakwenda kushiriki uchaguzi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia maeneo mengine, ni wale watu ambao walikataliwa kabisa wasirudishe fomu hizo, ni namna gani wangeweza kushiriki uchaguzi huo. Kwa hiyo, wakati unazungumza maneno haya, tumekwenda kwa Mheshimiwa Jafo zaidi ya mara tatu, tumemkuta Mheshimiwa Waziri, lakini pia tumemkuta Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tumemweleza matatizo haya tukiongozana na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, lakini hakuna kilichoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulistaajabu sana, wasimamizi wa uchaguzi ambao wamepewa fursa ya kusimamia uchaguzi huo wa Serikali za Mitaa wamepewa

kazi na Ofisi ya TAMISEMI, lakini cha kushazangaza maelekezo ambayo Mheshimiwa Waziri alikuwa anasema anawalekeza, hawakuweza kutekeleza hata moja. Sasa tunakwendaje kwenye uchaguzi wa namna hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli utaratibu uliokuwa ukiendelea ni utaratibu wa kihuni ambao kwa kweli haustahili kabisa. Ninashangaa kwamba mpaka sasa hivi Serikali haijachukua hatua kwa hao watu ambao wamekwenda kuvuruga mchakato wa uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo naomba sana, kwenye suala la utawala bora ni muhimu tukaeshimu sheria tunazo zitunga wenyewe, lakini pia na kanuni na taratibu mbalimbali ambazo tunakuwa nazo ili kujenga imani pamoja na kujenga umoja na mshikamano ulio katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka pia kuzungumzia kuhusiana na suala la uchumi. Nimesikia mara nyingi sana Mheshimiwa Rais anazungumzia kuhusiana na vita ya uchumi. Vita ya uchumi tunayoizungumzia ni kuhakikisha kwamba fursa yoyote inayopatikana kwenye nchi ni lazima tuitumie kwa muda mwafaka; tumekuwa tunachelewa sana kufanya maamuzi katika taifa hili. Mara nyingi mipango mingi; na nimepata taarifa mbalimbali ambazo si rasmi; wanasema mipango tunayoipanga katika taifa hili inakwenda kutumika kwenye nchi nyingine na wanafanya vizuri, lakini sisi tumekuwa ni wazito na wagumu wa kuamua ni namna gani tunaweza tukatekeleza fursa na mipango mbalimbali ambayo inapatikana na ambayo tunaipanga katika taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano kidogo, na wewe mwenyewe umekuwa unasisitiza sana; kwa mfano kama Bandari ya Bagamoyo, tumekuwa na hofu na tunapiga kampeni ya hofu badala ya kuingia. Tuna wataalamu wengi na tuna wasomi wengi. Hivi kweli wameshindwa kupata ukweli? Wameshindwa kupata uhakika wa namna gani tunaweza tukahakikisha kwamba

fursa ya Bandari ya Bagamoyo tukatekeleza, na tusifikiri kwamba tuko peke yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Beira kule Mozambique wana nafasi wanaweza wakafanya hayo tukienda Mombasa wanaweza wakafanya hayo hasa ni lazima twende na wakati tunashindwaje kujadili na watu tunawasomi wengi wa kutosha tumeshindwaje kujadili na watu ili miradi hii ambayo inaweza ikainua uchumi wa taifa iweze kutekelezwa katika taifa letu tunaona haya mambo hayatekelezeki na kila wakati tunaona kimya.

Mheshimwa Mwenyekiti, lakini yapo mambo mengine ambayo tunaona kabisa kwamba yanasababisha uchumi wetu usisonge mbele. Kwa mfano sasa kuna tume/kamati uliunda kwa ajili ya kuchunguza masuala ya madini, wakaenda Mererani wakaangalia mambo mabaya yaliyokuwepo kule na wakasema wanaweza wakafika mahala wakasitisha ule mgodi ili kujadili kwa manufaa ya taifa hii. Hata hivyo ni miaka mitatu leo au mwaka wa nne leo hakuna kinachoendelea; mgodi umesimama, wafanyakazi zaidi ya 400 wamefukuzwa kazi na hawajapewa hata mafao yao mpaka sasa hivi lakini kazi aiendelei na migodi ile imesimama na hakuna kinachozalishwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tufike mahala kama taifa tujuwe kwamba tunapokuwa tunahitaji uchumi upande ni lazima tuhakikishe kwamba tuna fanya haraka kwenye fursa ambazo tunazo. Leo tuna mgodi lakini hamna kinachoendelea; tanzanite imekaa pale inaoza watu wanaochimba pale hawaeleweki wanasema tunajadili, miaka mitatu mnajadili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na huo mgodi si kwamba labda anamiliki mbia peke yake, ni sisi nay eye; sisi tuna asilimia 50 na yeye anaasilimia 50, lakini tunashindwa kujadili kitu kama hicho kitu kidogo tunakaa miaka 3. Wananchi wetu ambao ni Watanzania waliokuwa wanafanya kazi pale zaidi ya 400 wameshindwa kulea familia zao na

kupeleka watoto wao shuleni kwa sababu ya majadiliano, ni siri ambayo mpaka leo hatuelewi. Kwahiyo tunaomba sana Wizara ya fedha pamoja na Serikali watuambie ni kwanini mpaka leo hawajafikia makubaliano kwenye majadiliano ya Mgodji wa Tanzanite ili uweze kuzalisha na kuhakikisha kwamba unachangia Pato la Taifa kwa kipindi ambacho tumekuwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine; tumeshangaa sana, tunasema kwamba tuna madini na tunataka madini yachangie Pato la Taifa; na kila mwaka tunapanga bajeti humu ndani lakini fedha hazijawahi kwenda. Waziri wa fedha pia atuambie ni kwanini hapeleki fedha ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kuinua uchumi kwa kutumia madini? miaka yote mwaka wa kwanza mpaka wa tatu mpaka miaka minne hakuna kilichoendelea. Mwaka jana tulitenga takriban bilioni sita ili waweze kufanya shughuli za maendeleo katika migodi yetu lakini haikwenda hata shilingi; na hata mwaka juzi pia. Sasa maaana yake ni nini? Kama kweli tukaanzisha shirika la kusimamia madini katika nchi kuhakikisha migodi yetu inafanya kazi na tunapata pato kubwa la taifa kutokana na madini lakini hatupeleki fedha. Kwahiyo mambo haya ni lazima tuyatazame sana, na kama Watanzania tuchangamkie fursa; tunapokuwa na mradi wowote ni lazima kuhakikisha kwamba twende na muda. Tunavyozidi kuchelewa ndivyo ambavyo tunachelewa kufanya maendeleo katika taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni kuhusiana na kilimo. Asilimia 65 ya Watanzania ni wakulima, wafugaji na wavuvi; fedha zimekuwa zinatengwa kila mwaka; nitoe mfano wa miaka mitatu tu. Mwaka wa 2016/2017 tulitenga ndani ya Bunge hapa bilioni 101 lakini fedha iliyokwenda kwenye shughuli za maendeleo bilioni tatu peke yake. Mwaka 2017/2018 tulitenga shilingi bilioni 150, fedha iliyokwenda kwenye kilimo ilikwenda bilioni 16 peke yake. Pia mwaka 2018/2019 tulitenga fedha hapa bilioni 95 lakini fedha iliyokwenda ni takriban bilioni 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 65 ya Watanzania ambao ni kundi kubwa kuliko kundi lolote katika nchi hii hawapelekewi fedha; sasa leo tunasema tunakwenda kwenye uchumi wa kati; tunawezaje kwenda kwenye uchumi wa kati kama wananchi hawa ambao ni kundi kubwa wangeweza kuzalisha lakini pia wangeweza kuchangia Pato la Taifa hawapelekewi fedha. Kwahiyo tunaomba sana; tunapozungumzia uchumi ni lazima tuhakikishe kwamba tunalenga maeneo muhimu ambayo yanaweza yakainua uchumi wa taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ni lazima tukubaliane, leo katika takwimu za Serikali vijana wetu wanaomaliza kwenye vyo mbalimbali hapa nchini ni takriban 800,000, lakini watu wanaoingia kwenye ajira rasmi ni takriban watu 40,000 watu takriban 760,000 hawana kazi; hawa watu wanakwenda kwenye kilimo na uvuvi lakini fedha haziendi kule tunasema tunataka kujenga taifa linaweza likatusaidia kuinua wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo mapendekezo ya mpango tunayoyaangalia leo...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni kengele ya pili.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, hauoneshi ni namna gani tunakwenda kwenye uchumi wa kati, inaonekana tunazungumza ndani ya Bunge lakini utekelezaji kwakweli hauko sawa sawa. Tunaomba uwe mkali lakini uendelee kutoa maagizo tukishirikiana na sisi Waheshimiwa Wabunge ili tuhakikishe kwamba Serikali hii inafanya yale tunayoyapitisha ndani ya Bunge hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Frank Mwakajoka, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba niwape hongera sana wenzetu wa Serikali kwa mpango wao huu waliotuletea hapa. Nianze kwa kuwapongeza watu wa Wizara ya Kilimo na biashara, leo tarehe 11 yale madai yote ya korosho yamelipwa na wakulima sisi; na mimi mkulima; kupitia *cashew nut payments code 704* imelipwa, kwa hiyo, ahadi ya Mheshimiwa Rais Magufuli imetekelezeka hongereni sana na sisi wakulima tunaendelea kukaza mwendo, Hasunga hongereni sana kwa kazi ilikuwa ni kitu kabisa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo machache, nina mawili tu. Kwanza nilitaka nirejee maneno yako uliyoyasema asubuhi kuhusu China; ulivyosema nimekusikia vizuri. Kama nimekuelewa vizuri nadhani Mbunge yeyote mwenye maarifa amekuelewa vizuri, na bila shaka Serikali imeelewa vizuri. Kwasababu China inapaswa iwe ndicho chanzo chetu cha mtaji wa miradi mikubwa ya maendeleo. Lakini ni kwanini mpaka sasa, tunapozungumza, hata TAZARA iliyojengwa na Mwalimu Nyerere ina mgogoro mkubwa sana. Ni mahali gani tumeshindwa kuzungumza na Wachina hawa tukaelewana wakati wachina hawa kihistoria kwa kweli ni ndugu zetu na kuna maelewano ya kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu wewe pia ni kiongozi wetu humu mimi napata hisia kwamba tuwashawishi viongozi wetu wakubwa wakatembelee China, ili kama kuna kitu hakieleweki wakakifungue wakubwa hawa. Wachina hawa tunaweza tukawatimia vizuri na wangeweza kutusaidia kwa mambo mengi, hasa masuala haya ya kimtaji kwa sababu uchumi wetu ndio unajijenga, unahitaji ku-*stabilize*, vinginevyo naona kama tutapata shida. Hii kukopa kwenye benki, fanya hiki inatuletea shida kubwa sana. Ni vyema twende China tukazungumze nao, tukakope mkopo mkubwa na wamuda mrefu ili kuweza kukwamua masuala haya tunayotaka kuyafanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri hoja yako ya asubuhi imenikuna sana; nawe kwasababu mnakaa na wakubwa mnakunywa kahawa nadhani kuna haja ya kuipeleka na kwao kule waweze kuelewa vizuri; umetueleza kitu kizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa niliseme pia amelizunguza ndugu yangu Mwakajoka hapa. Waziri wa Fedha fursa hazitusubiri, fursa zipo kesho hazipo. Nasema hivi kwa sababu; nizungumzie suala ya reli ya kati kwa mfano, SGR inayojengwa ni kitu chema sana, Rais Dkt. John Pombe Magufuli huyu ameamua uwamuzi wa busara kabisa kutujengea reli ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini reli hii ni mradi mkubwa na manufaa yake ni ya muda mrefu kidogo. Hii reli itakuwa na manufaa ya kiuchumi kama itafika Kigoma kwa ajili ya kuchukuwa mzigo mzito uliopo mashariki mwa DRC. Reli hii itakuwa na faida tawi lake hili la kutoka Tabora Kaliua kwende Kalema mpaka Kasanga Port kwa ajili ya kutape mzigo uliopo kusini mashariki ya DRC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majirani zetu wote fursa wanayoitazama ni hiyo hiyo. Utasikia ooo! leo hii mzigo mkubwa unaopita bandari ya Dar es Salaam ni wa nchi ya Uganda! Zipo taarifa ambazo ninauhakika nazo kabisa; asilimia 60 wa ule mzigo unatoka Mashariki Kaskazini ya DRC ambao wangeweza kuja kutumia Bandari yetu ya Kigoma na wakaja kutumia Bandari yetu ya Kasanga kwenye Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Keissy amezungumza Bandari ya Kigoma leo tunachozungumza, na Waziri wa Fedha unajua; kwamba Bandari ya Kigoma *Modernization* ya Kigoma pot kuna pakeji ya msaada kutoka Jamhuri ya watu wa Japan. Hata hivyo mradi ule umekwama na sababu zake za kukwama ni vikwazo eti! Wanadaiwa mitambo yao walipe kodi za

TRA. Wale wajapani walikuwa *negotiation* na Serikali huu ni mwezi wa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ningependa kujua kwakweli, *on a serious note*, ni kitu gani kimekwamisha *modernization* ya *Port* ya Kigoma ilhali wenzetu Wajapani wapo tayari kutusaidia ku-*modernization* bandari ile kwa maslahi mapana ya uchumi wa nchi yetu. Kwamba mzigo sasa utoke ngambo ya pili ya DRC uje Bandari ya Kigoma uje kwenye reli ya SGR itakayojengwa kupeleka mzigo nchi za China na mashariki ya mbali; hilo ni jambo ambalo ningependa tuendelee kulizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii zana ya majirani zetu, sina haya ya kuwataja, kujenga barabara kujenga reli na matawi yake wanakuja kudhohofisha, maana tutakuwa tunapokea mizigo kutoka nchi ya tatu. *Origin*, nchi ya pili na sisi tunakuwa nchi ya tatu ilhali tuna fursa ya kuja moja kwa moja sisi kutoka DRC na kuja katika nchi ya Tanzania; fursa hizi mziangalie. Nina matumaini kule hazina mtakaa chini na wataalamu mliangalie kwa mapana na marefu haya; mumshauri Mheshimiwa Rais juu ya jambo hili sasa, jambo hili maslahi yake ni mapana sana kwa taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu ndege. Tulikuwa wote wakati tunapokea *Dreamliner*, nadhani wewe ni shahidi na wote mliokuwepo, kwamba kilikuwa ni kitu chema mno, kitu ambacho kila mmoja alifurahi. *Dreamliner* inatoka Marekani inatumia masaa 16 kufika Dar es Salaam, *non stop* na kila kitu kinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu iko hivi; Mheshimiwa Waziri wa Fedha ununuzi wa ndege ni jambo jema mno, jambo jema sana. Hata hivyo ndege hizi lazima tuzifungamanishe mambo mengine, ndege hizi lazima tuzifungamanishe na wenzetu wa utalii ili ndege hizi ziweze kuwa na faida. Vinginevyo ndege peke yake hizi zitafika mahali itakwenda Mumbai haina abiria wa kutosha, itakwenda Guangzhou haina abiria wa kutosha. Kwa hiyo kuna haja wenzetu wa Serikali hasa Wizara ya Fedha



wazungumze na mashirika rafiki kama vile *Precision Air*, *Rwanda Air*, na zimbambwe *Airway*, na sisi Dar es Salaam iwe *hub* katika *International travel*, vinginevyo ndege hizi zitakosa biashara inayotarajiwa.

Mheshimiwe Mwenyekiti, ndege tuliyopanda siku ile ukiiangalia inabeba abiria 260 *non stop* Dar es Salaam Guangzhou, *non stop* Dar es Salaam mpaka Mombai. Sasa ndege hizi sisi wenyewe hatuwezi lazima tufikiri kibiashara; kwamba abiria kutoka Lubumbashi, Lusaka, Lilongwe, Bunjumbura na Entebe wanakuja Dar es Salaam halafu Dar es Salaam, halafu Dar es Salaam ndiyo inakuwa ndiyo kitivo na eneo la *hub*. Kama ilivyo Dubai, sisi lazima tuwe Dubai nyingine katika nchi za maziwa makubwa ili ndege zetu ziweze kuwa na faida kubwa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa na li-link na hili hili...

**MWENYEKITI:** Pia katika hilo hili hawa Lubumbashi Waziri wa Uchukuzi akumbuke kujenga hoteli ya watu wa *transit* haraka sana, endelea Mheshimiwa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa kabisa, ahsante sana; na hilo unalolisema, ukiiangalia tulichowekeza kwenye ujenzi wa rada tuna rada nne zinafanya kazi. Viwanja vya ndege vyetu vingi havina taa za usiku na matokeo yake ndege zetu nyingi zinafanya kazi mchana usiku hazifanyi kazi; na abiria kutoka Goma Congo kutoka Bukavu; na kwa wale wasiojua, Mji wa Bukavu ni mkubwa kama Dar es Salaam, ni miji mikubwa sana hii. Hawa watu wangeweza kuwa wanakuja kwa ndege za kusafiri mpaka usiku. Tafsiri yake ni kwamba Bandari ya Kigoma sasa ijengewe *facility* ya ndege kutua usiku ili ndege zifanye usiku na mchana ili ndege zetu kubwa zile ziweze kuwa na faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa rada, ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Julius Kambarage Nyerere, *terminal* III uweke na ndege hizi tumetumia takribani tirioni 2.7. Sasa

lazima wenzetu wa hazina mfikiri kibiashara, muwe na mpango wa muda mfupi, muda wa kati na hakika tuwe na mpango wa muda mrefu kwa sababu hizi ni fursa, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kafungua fursa, hizi ndege wenzetu wanashangaa. Juzi nilikuwa nazungumza nabalozi mmoja wa nchi jirani akawa ananiuliza ninyi mmewezaje; nikamwambia hiyo ni *Magulification of Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya ni makubwa, na wenzetu wa Wizara ya Fedha, Wizara ya Uchukuzi, Mama Kairuki, wa uwekezaji, muanze kufikiri kibiashara. Juzi nimefurahi kusikia Waziri wetu wa biashara alikuwa China, nimefurahi sana, alikuwa anataeleza mambo ya kule China. Mawaziri msafiri msikae ndani. Ndege asiposafiri hawezi kujua mtama umekomaa wapi; na kadiri Mawaziri mnavyosafiri mnakuwa wa kisasa zaidi na namnakuwa mnaifahamu dunia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa leo nilifikiri nizungumze hayo, nakushukuru, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko. Mheshimiwa Goodluck Mlinga atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza,

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba nitoe nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kutuchagulia Mkaguzi na Mdhhibiti kuu wa Hesabu za Serikali mpya na mchapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwape udhibitisho; Ofisi ya CAG haikuwa safi kama walivyokuwa wanaifikiria. Nataka niwape mfano; mfumo wetu wa ukaguzi katika halmashauri zetu ukaguzi wa miradi unafanyika kwa *sampling*, yaani katika miradi kumi unakaguliwa miradi mitatu, ile miradi mitatu ndiyo inatoa *remarks* ya ile miradi kumi; sasa pale ndipo mianya ya rushwa inapopitia. Inatolewa pesa inakaguliwa miradi mizuri mibovu inaachwa, hatimaye *remarks* inatoka hati safi lakini vitu vinakuwa

hovy. Kwahiyo naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutuchagulia CAG mpya; na napenda nimuambie kuwa aendelee kufanya *reform* katika ofisi ya CAG ili wananchi wapate haki zao na huduma wanazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili nataka niongelee elimu. Tanzania ina idadi kubwa ya watu wanaokadiriwa kuwa milioni 55 na watu wazima wanaokadiriwa kuwa zaidi ya milioni 25, lakini *production* iliyoko katika nchi yetu haiendani na idadi ya watu waliopo; kwanini idadi ya watu haiendani na *production* iliyopo? ni kwasababu kubwa ya elimu ambayo wanaipata; yaani mitaala yetu ya elimu hai-*fit* nchi yetu ya Tanzania na nje. Kwa mfano shule ya msingi wanafunzi wanafundishwa darasa la kwanza mpaka *form four* lakini akienda mtaani hawezi hakafanya kitu kwa sababu mitaala ya elimu haimuruhusu yeye kwenda kuwa *productive* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili napendekeza mwanafunzi wa darasa la kwanza mpaka *form four* ukiacha masomo ya msingi anayosoma awe anapewa elimu ya msingi ambayo itamwezesha kutumia rasilimali inayozunguka maeneo yake. Kwa mfano, maeneo ya Kanda ya Ziwa wanafunzi wa elimu ya msingi wafundishwe uvuvi na uchimbaji wa madini ya dhahabu; maeneo ya Lindi wafundishwe kilimo bora kama cha korosho; maeneo ya Mara na Singida wafundishwe uvuvi wa kisasa; Dodoma wafundishwe uvuvi wa kisasa katika elimu ya msingi ili asipoendelea chuo aweze kupambana na maisha; maeneo kama Rukwa wafundishwe tiba asili. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa chuo kikuu, leo hii tumeshuhudia wanafunzi wanaomaliza chuo kikuu ni zaidi ya laki tano kwa mwaka lakini hawa wanafunzi wanapokwenda mtaani...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnacheka lakini tiba asili inalipa kwelikweli.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** *Worldwide* inalipa sana.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Sawasawa.

**MWENYEKITI:** Kabisa, angalieni dawa za Mchina ziko dunia yote. Endelea Mheshimiwa Mlinga, walikuwa wanacheka dawa za asili kwa Rukwa lakini mimi nawaambia ile ni mtaji mkubwa. Ukienda Nairobi unakuta mabango yameandikwa mganga maarufu kutoka Tanzania (Rukwa). Endelea Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hata wale wenye shida ya nguvu za nanihii tiba asili ndiyo imekuwa mtatuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa chuo kikuu, leo hii tumeshuhudia utitiri wa vyuo vikuu lakini kozi ambazo wanaziweka katika vyuo hivyo haziko *productive* katika nchi yetu. Leo hii tunasikia Wizara ya Elimu wanatangaza walimu wa *arts* hatuwahitaji tena lakini vyuo bado vinazalisha wanafunzi wa *arts* na bado vinakwenda kudahili wanafunzi tena wanapewa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza mitaala yetu ya elimu ya chuo kikuu iwe inatolewa kulingana na mahitaji ya nchi yetu. Kwa mfano, mtu anamaliza *Business Administration* hawezi kuanzisha hata genge la nyanya; mtu anamaliza *Public Administration* hata uongozi wa familia yake hawezi, watoto wanavuta bangi. Wanasheria, tumeshuhudia wako Wabunge wanasheria lakini wanaongoza kwa kufanya makosa, kila siku wako mahakamani.

Kwa hiyo, napendekeza hata vyuo vikuu mitaala iendane na mahitaji ya nchi yetu yaani watu wanapotoka hapo wawe *productive* na siyo kuvunja sheria na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la mapato napendekeza kwenye kipengele kimoja tu, tunapoteza mapato mengi sana katika nchi yetu. Nitolee mfano, tuna madereva wengi sana katika nchi yetu zaidi ya laki tano, lakini wengi wameajiriwa katika ajira ambazo siyo rasmi. Kwa mfano, madereva teksi wako zaidi ya 4,000 hawalipii kodi, *NSSF* wala matibabu. Madereva wa daladala zaidi ya 20,000 hawalipi kodi. Madereva wa mabasi makubwa zaidi ya 5,000; madereva wa mabasi ya kati zaidi ya 5,000 na madereva wa Noah zaidi ya 16,000 lakini hawalipi kodi. Napendekeza kwa mfano vile vitambulisho tulivyowapa Wamachinga tungewapa na madereva ili wawe wanalipia hata laki moja kwa mwaka ili iwe kwa ajili *Pay As You Earn*, *NHIF* na *NSSF* ambayo itawasaidia hata wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nataka nipendekeze kwenye utafiti. Benki yetu Kuu ya Tanzania tuna Kitengo cha Utafiti lakini wanafanya tafiti matokeo yake ripoti wanazifungia kwenye makabati. Tumeshuhudia tuna mazao kama tumbaku ni *crisis* katika soko; tuna korosho ni *crisis* katika soko; tuna pamba *crisis* ni katika soko, lakini *BoT* tangu imeanzishwa kuna Kitengo cha Utafiti, sasa tuwaulize wanafanya nini zaidi ya kupokea mishahara tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza tafiti wanazozifanya *BoT* katika mambo mbalimbali ya *mining*, kilimo, biashara, hizo ripoti wawe wanaziweka wazi. Tuna matajiri katika nchi yetu; ikusanye matajiri na benki, iweke ripoti katikati itoe ushauri watu wakopeshwe hela matokeo yake wafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda *EPZA* nikakuta wanaagiza nyuzi kutoka India wakasema wao pamba inayozalishwa Tanzania yote zingekuwa zinatengenezwa nyuzi wana uwezo wa kuzinunua zote. Sasa waulize *BoT* wanashindwa kumshauri hata Mohamed Dewji akapewa mkopo akatengeneza kiwanda cha nyuzi akanunua pamba zote za Wasukuma zikatengenezwa nyuzi akapeleka *EPZA* wakaenda kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunategemea nyuzi kutoka India wakati Wasukuma kule na watu wengine hawana sehemu ya kuuza pamba zao. Kwa hiyo, napendekeza hiki Kitengo cha Utafiti cha *BoT* wafanye kazi yao, waache kupokea mishahara waweke ripoti wazi matajiri tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Goodluck Mlinga kwa mchango wako mzuri. Kwa kweli wakati mwingine mambo mengine anayosema Mheshimiwa Mlinga yaani mtu anamaliza *CBE* hapa hawezi hata kufungua genge la nyanya, mtihani huo, lazima tujilize hii inakujaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza nilikwishakutaja, utafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia naomba niungane na wenzangu niipongeze Serikali nzima kwa maana ya Rais na Serikali yote ambayo imetuletea Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ambayo nataka niishauri Serikali kwa sababu tunapojadili Mpango maana yake ni kuboresha rasimu hii, ndiyo *process* ya *budgeting* inaanza hivyo. Nianze na suala zima la *disaster preparedness*. Nimeona katika Mpango ambao Waziri ametuletea, nadhani ukurasa wa 85, sikumbuki vizuri lakini napenda nijikite hapo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga miundombinu, tena ya gharama kubwa; viwanja hivi vya ndege, barabara, madaraja, miundombinu ya umeme, mabwawa makubwa kama haya ya *Stiegler's Gorge*; miundombinu yote hii inataka pesa nyingi. Nachotaka kusema kwa kuwa

tunajenga miundombinu hii lazima pia tuwe na utamaduni wa kuulinda miundombinu yetu tunayojenga kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama siku za nyuma Serikali ilikuwa na lugha ya *maintenance* sasa hivi ni kama lugha hiyo inaanza kupotea. Kwa mfano zamani tulikuwa na *Public Works Department* inajenga barabara lakini kila mwaka kulikuwa na *periodic maintenance* na wanapita wanatengeneza; ile yote ilikuwa ni kuhakikisha kwamba miundombinu hii inayojengwa kwa gharama kubwa inatunzwa na inalindwa ili baadaye tusije tena kutumia pesa nyingi za bajeti ambazo tumepanga kwa ajili ya maendeleo kutengeneza miundombinu ambayo imeharibika. Kwa kufanya hivi tutaokoa gharama kubwa au kuepusha ile pesa ambayo imepangwa kwa bajeti ya mwaka huu tunaanza kuitumia kwenye kurekebisha miundombinu ambayo imeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna majanga mengi, yako mafuriko ambayo kama tumekuwa tunafuatilia yamegharimu Serikali pesa nyingi, watu wamekufa, hata Kenya mambo haya yamewapata; yapo majanga yanayotokana na moto, yapo matetemeko, zipo radi, lakini vyote hivi vinapotokea lazima viigharimu Serikali, lazima Serikali irudi tena kwa sababu huwezi kuacha kitu kimekwishatokea ukasema tukiache kwa sababu hakimo katika mpango wa maendeleo. Kwa hiyo, nachotaka kuishauri Serikali yangu ni kwamba lazima tujenge utamaduni wa kuwa na utayari wa kupambana na majanga yanapojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano huu mradi mkubwa ambao tunaujenga wa *Stiegler's Gorge*, mradi huu kwa kweli ni mfano mzuri. Ukitazama mradi kama huu tungekuwa na *approach* kama hii katika miradi mingi maana yake katika kuwa *prepared* kwa kujenga miradi hii siyo lazima kuweka bajeti tu kwa ajili ya kusubiri janga litokee maana majanga ni matukio, matukio ndiyo hayo majanga. Hata hivyo, katika utamaduni ule wa wa kusanifu miradi,

kwa mfano, unajenga mradi wa bwawa, unatengeneza mradi ambao ni *multipurpose*, mradi kama wa Bwawa la Rufiji, utafua umeme, utatoa maji ya kunywa, maji ya kumwagilia; mradi huo unaweza kutengeneza *flood control* kwa maana ya kwamba hata haya mafuriko mengine ambayo yanajitokeza utakuwa umeyapunguza kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, *approach* hii ya kutengeneza miradi ambayo ni jumishi inaweza kutufanya tukawa tayari kupambana na majanga kila yanapotokea. Kwa hiyo, natamani kuona kwamba katika miradi tunayojenga tunajiwekea utaratibu wa kujikinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*declare interest*; niko katika Kamati ya LAAC, nimetembelea miundombinu mingi midogomidogo; ujenzi wa madarasa, ujenzi wa *health centers, public buildings* nyingi, lakini sehemu zote ambazo nimepita kama nimeona nyingi labda ni moja au mbili, hata kukumbuka tu kuweka kitu kidogo kama mtego wa radi, hatukumbuki. Kila wakati unasikia radi imepiga darasani watoto wamekufa, walimu wameumia lakini unakuta hata kitu kidogo kama hicho tu; kuweka mtego wa radi kwenye jengo ambalo ni la *public*, kwenye makanisa yetu, hatukumbuki kuweka vitu kama hivyo. Kwa hiyo, nataka nijikite hapo, kwenye suala la *disaster preparedness* Serikali kwa kweli hata kama sio lazima kuweka kitengo na kukigharamia sana lakini kila sekta basi angalau ijikite katika kujiandaa na kupambana na majanga yanapotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni suala la kugharamia kilimo. Kilimo ndiyo kila kitu lakini Wabunge wengi wamelalamika, fedha tunazotenga kwa ajili ya kilimo bado hazikidhi mahitaji. Fedha tunazotenga kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji, tuna *23.4 million hectares*, tumefanya hekta laki sita tu lakini fedha tunazotenga kwa ajili ya shughuli ni ndogo na bado tunataka twende katika uchumi wa viwanda, ili tujenge uchumi wa viwanda lazima kilimo nacho tukipe msisitizo. Tutenge fedha za utafiti kwa ajili ya pembejeo, tutenge fedha za kilimo kwa ajili ya maghala, kujenga *silos* ili kilimo



hiki kikue kiweze kutusaidia kutoa *inputs* kwa ajili ya viwanda hivi tunavyotaka kuvijenga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wanachama wa SADC. Nakumbuka mwaka 2003 kulikuwa na mkutano Maputo, pale Maputo nchi zote wanachama walitoka na Azimio la Maputo 2003 (*Maputo Declaration*). *Maputo Declaration* iliazimia na sisi tulisaini kwamba kila nchi mwanachama itenge asilimia 10 ya bajeti yake kwa ajili ya kugharamia kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio lazima kwa mwaka mara moja utenge asilimia 10 lakini kuanzia mwaka 2003 mpaka leo natamani kuona *on an incremental basis towards ten percent*, kwamba kila mwaka tumeongeza kiasi gani ili angalau tufikie asilimia 10 ya bajeti zetu kwenda kwenye kilimo. Hilo namuomba Mheshimiwa Waziri na Waziri wa Kilimo waliangalie kwa sababu ni sisi wenyewe tulikubali kwamba tutatenga asilimia 10 kupeleka kwenye kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa bado niko kwenye kugharamia kilimo, naomba nizungumzie suala la Mfuko wa Kuhimili Bei za Mazao. Asubuhi nimemsikia Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, alisema vizuri tu kwamba *intervention* ya Serikali kwenye masuala haya ya masoko ya mazao haitakuwa tena kama ilivyokuwa. Nami nakubaliana naye kwa sababu lazima turuhusu soko liji-*regulate* lakini masoko ya mazao ni *very fragile*. Matatizo yanapotokea lazima tuwe na utaratibu wa kuhimili mtikisiko wa bei hizi, hasahasa bei zinapoanguka katika masoko ya dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka fulani tulikubaliana kwamba tuanzishe Mfuko wa Kuhimili Bei za Mazao. Tukasema tuanze na mazao mkakati manne ya kahawa, korosho, tumbaku na pamba. Nakumbuka Wabunge wengi walikubaliana na jambo hili lakini tangu tumelizungumza na nafikiri mpaka leo sijapata mrejesho kwamba hivi uanzishaji wa utaratibu huu wa Mfuko wa

Kuhimili Bei za Mazao angalau kusaidia wakulima ku-*absorb shocks* umefikia wapi?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Malizia Engineer.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa jambo moja tu, nalo ni suala la usimamizi wa miradi (*contract management*). Hii *culture* ya usimamizi wa miradi (*contract management*) bado inatugharimu. Narudia tena kusema niko katika Kamati ya LAAC lakini mambo nayoyaona huko hasa kwa miradi midogomidogo Serikali inaingia hasara kubwa sana kutokana na *poor contract management*. Miradi mingi inaingia kwenye gharama ambazo sio za lazima, inaingia kwenye *variation orders* ambazo siyo za lazima. Yote hii inatokana na miradi ambayo haiwi *managed* vizuri. Kwa hiyo, ipo haja kabisa kusimamia suala hili la kusimamia miradi kwa ajili ya kuokoa fedha na gharama za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa haya machache, sisi tunasema kusema mengi sio kuyamaliza, mengine tutaendelea kuchangia, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na baada ya hapo tutamwita Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niseme kidogo kuhusu Mpango huu wa Serikali ambao umeletwa mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wanafanya.

Kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana ya kusimamia mapato pamoja na kupanga mipango ambayo imetufikisha mahali tulipofika. Niseme pia hata huu Mpango ambao wameuleta 2020/2021 ni mzuri na naunga mkono *a hundred percent*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiona Mawaziri wanafanya vizuri, watendaji wakuu wa Serikali wanafanya vizuri, ujue kwamba nyuma yao kuna kiongozi wao. Nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, ambaye anafanya kazi nzuri mno na ndiyo maana Mawaziri nao wanafanya kazi nzuri. Tumeshuhudia mambo mengi yanafanyika hapa nchini kwenye sekta nyingi; afya, elimu, nidhamu Serikalini, vita dhidi ya rushwa, umeme na kadhalika lakini kwa kipekee miradi mikubwa ya kimkakati; reli ya kisasa, Mradi wa Kufua Umeme *Stiegler's Gorge*, kufufua Shirika la Ndege *Air Tanzania* kwa kununua ndege nane mpaka sasa. Sina haja ya kuyazungumza sana haya kwa sababu kila mmoja anayaona, kila mmoja anayafahamu lakini itoshe kusema kwamba tunampongeza Rais kwa kazi nzuri na tunamuomba maisha marefu na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ni *comment* kidogo kwenye Mpango huu na nianze na kilimo. Kilimo ndicho kimebeba Watanzania katika ajira kwani idadi kubwa ya Watanzania wanategemea kilimo na toka tunapata uhuru tumekuwa tunaimba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu. Yamepita maazimio mengi; Azimio la Iringa (Siasa ni Kilimo) na baadaye juzijuzi likaja Azimio la Kilimo Kwanza mpaka magari ya Wabunge na Mawaziri yakaitwa kwa jina hilo la Kilimo Kwanza lakini pamoja na hivyo bado kilimo hakijakaa sawa ni kwa sababu hatujaweka msukumo unaostahili kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani pale mwanzoni tulidhani kwamba *mechanization alone* ingetusaidia lakini kumbe kilimo cha kutegemea mawingu, kutegemea mvua hakitatufikisha mahali. Ndiyo maana mpaka leo toka

tumepata uhuru kilimo chetu bado kinasuasua na niseme sasa wakati umefika kwenye Mpango huu wa 2020/2021 Wizara iangalie namna ambayo itaweka msukumo mkubwa kwenye *irrigation*. Tunaomba Serikali iwekwe nguvu nyingi kwenye miundombinu ya *irrigation* ili tubadilike tuache kungojea mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mazao ya *traditional cash crops*, kahawa, pamba, tumbaku, wenzangu wamesema yamedorora. Kule kwetu kahawa ndiyo kabisa, tulikuwa tunaitegemea zamani lakini kahawa imekwisha kabisa kabisa na sababu kubwa ni pamoja na *population boom*. Yale mashamba ambayo yalikuwepo wamezaliwa watoto wengi badala ya mashamba sasa ni *plots*, kwa hiyo hakuna mahali pa kulima kahawa. Badala yake wananchi vijana wame-*resort* kwenye *hot cultural farming*. Nilipata faraja kubwa sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo juzi aliposema kwamba wanaleta Muswada wa kuanzisha mamlaka ambayo tunaamini ita-*coordinate* na ku-*promote hot cultural farming*. Suala hilo ni la msingi na lifanyike haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeshuhudia vijana wanalima mboga mboga zao ukifika wakati wa kuvuna yale mazao yanaozea shambani kwa sababu barabara zimeharibika. Barabara za vijijini ni za kutengeneza, kwa hiyo msukumo mkubwa upelekwe katika kutengeneza miundombinu ya kufuata yale mashamba ambayo vijana wanahangaika, wanalima karoti, wanalima nyanya na pilipili hoho na kila kitu lakini mwisho wa siku yale mazao yanaoza kwa kukosa usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya kazi nzuri sana kwenye miundombinu, barabara, madaraja na hata miradi mikakati ambayo imeshatekelezwa imefanyika vizuri. Nilisikia siku moja Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi akasema, sera sasa hivi imelenga kuunganisha mikoa kwa barabara za lami tu, lakini nikasema kwamba sera siyo *static* ni *dynamic* inaweza ikabadilishwa kidogo pale ambapo barabara inaonekana inaweza ikastawisha wananchi

mradi utekelezwe. Hapa nitoe mfano, barabara ya King'ori – Malula kwenda King'ori Madukani kwenda Maruvango, kwenda Ngarenanyuki, Ngabobo, Uwiro inakwenda mpaka Oldonyo Sambu, barabara hii iko kilomita mbili kutoka *junction* ya KIA na mpaka wa Arusha na Kilimanjaro. Barabara hii inaunganisha barabara kuu ya Arusha – Moshi – Dar es Salaam na barabara ya Arusha kwenda Namanga – Nairobi na inazunguka Mlima Meru. Wale wananchi wote pale walikuwa wameachwa hawana miundombinu ambayo inaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, barabara hii iko kando kando ya hifadhi ya Arusha *National Park*, barabara hii ikijengwa kwa kiwango cha lami itatusaidia, itaongeza idadi ya watalii ambao wataingia pale Arusha *National Park* na kuongeza kipato cha Taifa kupitia utalii. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri kwenye Mpango huu wa 2020/2021 asiisahau hii barabara, ina umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kweli imefanya kazi nzuri sana katika kuwapa wananchi maji lakini miradi ya maji tumeona inachukua muda mrefu, mingine mpaka Mheshimiwa Waziri anakuja anaingilia kati, anavunja mikataba ile, kwa hiyo usimamizi wa ile mikataba kidogo umekuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba huku tunakoelekea tujaribu kubadilisha mfumo, tutumie *Force Account* kwa sababu nimeona, nimeshuhudia kazi ikifanyika kwa mafanikio makubwa sana kwenye sekta ya afya. Vituo vingi vya afya vimejengwa kwa kutumia *Force Account* na ile miradi imetekelezwa vizuri kwa haraka haraka bila kupoteza muda na bila kutoa nafasi ya *price variation*.

Kwa hiyo nisema tu kwamba huku tunakokwenda hasa kwenye eneo la sekta ya maji, tubadilike kidogo tutumie *Force Account* ambayo ni...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pallangyo kwa mchango wako.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Getere, mchangiaji wetu wa mwisho atafuata Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango huu wa bajeti. Michango hii watu wengi wameizungumza vizuri lakini nilikuwa naangalia katika nchi yetu hapa kwamba uchumi wake unakuwaje, unakuwa kwa 6.8 mpaka *seven point*. Wanauchumi wanasema uchumi ukikua lazima uendane na mipango ya wananchi katika maeneo yao.

Nilikuwa naangalia maeneo mbalimbali sijui kwa nini nchi yetu haiendi kwenye vyanzo halisi vya kupata uchumi wetu unavyokwenda. Ukiangalia katika maziwa yetu, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria, ukinda Norway, ukienda Algeria, nilikuwa naangalia hapa Algeria ni nchi kama ya tatu hivi kiuchumi, lakini maeneo mengi inayotegemea katika uchumi wake ni suala la samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi uki-*invest* milioni 40 katika samaki unaweza ukapata samaki 200 na samaki 200 ukipata unaelekea kuzungumza habari ya bilioni mbili. Kwa hiyo nafikiri kwamba, sasa uchumi wetu uende sana kutafuta fedha za ku-*invest* katika maeneo ambayo tunaweza kupata faida kwa wakati muafaka. Vijana wetu wengi hawana ajira, lakini maeneo yetu mengi yana ajira. Tuna suala la kilimo, ukiangalia sasa Misri ndiyo nchi inaenda kwenye uchumi ambao uko juu kwenye uchumi wetu, lakini uchumi wao mwingi unatokana na *hot culture*, Kenya hivyo hivyo, Angola nayo imeenda kutuzidi kwenye uchumi ingawaje wana mafuta. Kwa hiyo, naomba Wachumi wetu waelekee sana kwenye namna ya kupata fedha ku-*invest* katika maeneo ambayo tunaweza tukapeleka vijana wetu wakafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naiona JKT kama ni eneo ambalo tungelitumia sana kupata uchumi wetu vizuri. Tuna maeneo mengi vijana wetu wanaenda JKT, tungetumia vijana hawa kuwapa mikopo katika maeneo, tuna maeneo mengi mazuri sana. Wale vijana wote wanaokwenda JKT wakitoka pale wameiva kwenye shughuli za kilimo, watu wote tume-*invest* kwenye shughuli za kazi za ofisini kazi ambazo sasa hazipo. Kwa hiyo tubadilishe *mind set* zetu twende kwenye maeneo ambayo tutanufaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi yalikuwa yanazungumzwa hapa, watu wanazungumza *good governance* (utawala bora), lakini utawala bora haujakita kwenye *election* peke yake, umejikita kwenye mambo mengi. Kuna *effective*, kuna *transparency*, kuna *accountability*, kuna mambo mengi yamejikita humo ndani lakini watu wameng'ang'ania mambo ya utawala bora utawala bora, kama vile ni uchaguzi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi za Ulaya sasa zinaangalia uchumi wao, kuna watu wanafikiri kwamba Tanzania haiko kwenye mpango wa kwenda mbele. Sasa hivi tunaangalia kwamba uchumi wa China mwaka 2030 utakuwa umezidi Marekani mara mbili, kuna watu wanaangalia hata Mexico nchi maskini inapokwenda 2030 inakwenda kuikaribia Marekani. Kuna watu wanafikiri kwamba kila wakati sasa sijui ni kuzungumza mambo ya uchaguzi, mambo ya kugombana. Kuna wasomi wamesema haya mambo ya uchaguzi pia yaliletwa na watu ambao wameleta kuvurugana kwenye nchi za Kiafrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nchi nyingi nyingine zipo nchi za utawala wa kifalme hazina uchaguzi. Leo mtu anazungumza uchaguzi umekuwaje, uchaguzi umekuwaje ili mradi wapate msaada. Nataka niwaambie wenzetu nchi za Ulaya sasa hivi kila nchi inagombana, ukienda Marekani wanagombana juu ya utawala bora, sasa Marekani si nchi ya demokrasia, ni nchi ya utawala

wa sheria. Ukienda Uingereza inagombana na Black City, ukienda kila mahali wanagombana kwa hiyo wasipokwenda kwenye uchaguzi wajue hakuna mtu atawasaidia, wao waende kwenye uchaguzi, tufanye uchaguzi mambo yaishe tuendeleo na wakati wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanafikiri Mheshimiwa Magufuli amejitokea tu kuwa Rais, Mheshimiwa Magufuli ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyetokana na Chama cha Mapinduzi. Nilisikia siku moja mtu anasema ndege zimekuja nikaona mapambio, nikaona nini, nikamshangaa. Ukisoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 70 inaeleza jinsi gani tumefanya mipango mikakati ya kuwa na viwanja vya ndege vingi na kupata ndege kwa ajili ya mambo yetu hapa. Sisi tunapoona...*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere tatizo siyo uchaguzi, watu wanaangalia matokeo, wameshaangalia wanapigwa ile mbaya. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa wanakamatia hapa chini lakini wanajua kimbembe kiko, si tarehe 24 Novemba wewe utaona matokeo tu! Mheshimiwa endelea. *(Kicheko)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza...

**MWENYEKITI:** Nilikuwa namchokoza Frank hapa!

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli! Kwanza mimi naona hiki Chama cha Upinzani ndani ya Tanzania kinaitwa CHADEMA, hiki chama kinakokwenda kwanza wanazungumza *transparency*, wao wenyewe wanapata mabilion ya fedha hapa kutokana na ruzuku lakini mpaka *today* wameandikiwa barua mbili na Msajili wameshindwa kufanya uchaguzi. Sasa huu utawala bora wanaouzungumza ni upi? Utawala bora wa CCM peke yake au utawala bora mwingine? *(Makofi)*



## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakajoka, Mwakajoka ametoka pangoni. Jamani tumempa ruhusa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, kwanza anasema kwamba mambo ya uchaguzi haya hayafai na sisi pia tulishawaambia kwamba mko wengi ndani ya Bunge leteni Muswada hapa tufute vyama vingi vya siasa ili mbaki na chama kimoja. Mtakaotaka kubaki CCM mbaki na sisi wengine ambao tutakuwa hatutaki tuendeleo na mambo yetu. Ahsante. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini, kaa chini wewe!

**MWENYEKITI:** Jamani aliyepewa taarifa ni Mheshimiwa Mwita Getere, unaipokea taarifa Mheshimiwa Mwita!

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza vyama vyenyewe vitajifuta kama vinavyojifuta sasa hivi, kwa hiyo mimi sioni haja ya kuendelea na mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze, kuna watu wamezungumza hapa fedha haziendi kwenye maeneo yetu ya majimbo, fedha haziendi huko kwenye halmashauri, fedha haziendi wapi, sasa mimi najjuliza; fedha haziendi wapi? Ukienda sekta ya elimu tunatoa bilioni 24 kila mwezi zinakwenda shuleni, ukienda kwenye afya...*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kila halmashauri inapata.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila halmashauri inapata. Ukienda kwenye afya hospitali zinajengwa kila mahali hata Mwakajoka juzi alisema imejengwa kwake, ukienda kwenye reli fedha zinakwenda, ukienda kwenye barabara za changarawe

na lami zinakwenda, ukienda kwenye shughuli za kila mahali zinakwenda. Kwenye madini wamezungumza hapa, watu wanasema *Private Sector*, tushirikiane na *Private Sector* kutengeneza uchumi, sasa mtu anasema tupeleke fedha kwenye madini. Badala ya kusema wale wa madini tuwape nafasi ili *Private Sector* zituletee fedha, yeye anataka tupeleke tena fedha kwenye madini. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita na kwenye ruzuku ya CHADEMA zinaenda pia.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku ya CHADEMA pia zinaenda huko huko ndani. (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoona sasa hivi suala la hawa wenzetu wamejichanganya kuhusu Mheshimiwa Rais wetu. Rais wetu amejiongeza kukusanya mapato ya kutosha kwa ajili ya kupeleka maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja, siku moja tumekwenda pale Muhimbili, mtu anasema hapa panadaiwa bilioni nne hazijaja hapa, bajeti haijaja ya bilioni nne. Bilioni nne kabla ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuwa madarakani walikuwa wanakusanya bilioni tano, sasa hivi katika sekta ile ya Hospitali ya Muhimbili inakusanya bilioni 11, sasa kama zimeongezeka unapeleka za nini wakati hela zimeongezeka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawajui kubana matumizi pia ni sehemu ya kuongeza fedha kwenye maeneo mbalimbali. Kwa hiyo nafikiri kwamba wenzetu wanajichanganya na hali halisi ilivyo na katika huo utawala bora wako watu wanasema ile *Citizen*, Watanzania wanategemea nini. Kama wameona Rais aliyepo na chama kilichopo kimebadilika kinaenda kuwaletea matumaini wawe na vyama vingine vya kufanya biashara gani! Leo hata mngepeleka Polisi Ngorongoro, hata mngepeleka polisi pale Monduli kuna maeneo hata ungepeleka fomu 300 hazichukuliwi. Maana pale hawachagui vyama, wazee

ndiyo wanasema, ukienda Ngorongoro wao walishamaliza uchaguzi wanasema wewe ni Mwenyekiti, wewe utakuwa Diwani, wewe utakuwa Mbunge, sasa unaenda kufanya biashara gani kule ndani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona chama kinaitwa sijui ni *NCCR* Mageuzi, hakipo. Yule mzee naye ampumzike aende pole pole tulishampa na madaraka siku nyingi hapa ndani, naye anang'ang'ana kwenda kwenye sehemu ambayo haipo. Atulie mahali pake sisi tumuone bora hata tuweze kumpa Ubalizi, anaanza tena maneno ya kuleta matatizo kwenye nchi yetu hapa. Kwa hiyo tukubaliane kwamba CCM pamoja na kwamba Rais wake...

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita kuna taarifa.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mwita Getere kwamba hata kwangu Serengeti, nimeshangaa sijawahi kuona, vijiji vingi wamepita bila kupingwa hata kwenda kuchukua fomu imeshindikana, wametafuta wagombea wamekosa kabisa. Sijawahi kuona hii, sijawahi kuona kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita unapewa taarifa hiyo, unaipokea?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa kwa sababu mimi ninavyoona, labda kama tunataka, nakuomba, pengine tukae tukubaliane hawa wenzetu walioko humu ndani tunaweza kuwasaidia labda kajimbo kamoja, viwili wakarudi humu ndani. Maana yake hali ya hewa ni mbaya kuliko ilivyo kawaidia, kwa hiyo, ndiyo maana wamekuwa na hali hiyo *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ukweli kama tunataka kuwa na upinzani tutengeneze mazingira ya kuwabakiza wenzetu, vinginevyo wote hawatarudi hapa

ndani. Kwa hiyo, tukubaliane na mazingira hayo, vinginevyo tukubali sasa Tanzania imebadilika, watu wanataka Chama cha Mapinduzi, lakini wasimhusishe Mheshimiwa Rais na uchaguzi. Mheshimiwa Rais anafanya kazi za Serikali, Chama cha Mapinduzi kina viongozi wake, Chama cha Mapinduzi kina Katibu, kuna viongozi, kuna Wabunge sisi tupo tunapambana na mambo yetu. Wenzetu wameshindwa kwenda kupambana kule chini, wanapambana na hali ya hewa ya kwao humu ndani. Wameshindwa kwenda kupambana kwenye majimbo yao wameachia maeneo yameenda, watu wanaogopa. Kwa hiyo, naomba mazingira yatengenezwe, tuone namna gani tutaendelea na upinzani Tanzania, vinginevyo hautakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Aah! Hatari kubwa hii, Mheshimiwa Frank Mwakajoka, amewachangamsha Mheshimiwa Mwita Getere, amewakumbushakumbusha baadhi ya mambo, maana mlikuwa mmepoapoa kidogo. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge nashukuru sana, huo ndiyo mwisho wa uchangiaji wetu wa karibu wiki nzima. Tumeisaidia sana Serikali katika michango mbalimbali, lakini pia tumechangamshana kidogo, si tunaelekea kwenye uchaguzi! Saa nyingine dakika mbili, tatu mipasho kidogo, ndiyo siasa inanoga,. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo sasa tunarudi kwenye *serious note*, kwa kumwita Mheshimiwa Naibu Waziri ili aje hapa mbele aweze kupitia na kupokea michango yetu. Kama mtakavyokumbuka, siku Waziri wa Fedha alipokuwa anawasilisha hapa, hakutoa hoja, aliwasilisha Mpango ili kupokea mapendekezo. Tulichofanya tumetoa mapendekezo, Mheshimiwa Naibu Waziri atayapitia yale ambayo, kwa sababu muda hautoshi ana dakika 45 tu, baada ya hapo atatamka kwamba wameyapokea kama Serikali ili kwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, karibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kutoa shukurani za dhati, kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vema mjadala wa hoja iliyowasilishwa mnamo tarehe 5/11/2019 na Waziri wa Fedha na Mipango ambayo ni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia ama kwa maandishi au kwa kuzungumza. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge 111 wamechangia katika mjadala huu, ambapo Wabunge 95 wamechangia kwa kuzungumza na Wabunge 16 kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyotangulia kusema, lengo la wasilisho la Waziri wa Fedha na Mipango mbele ya Bunge lako Tukufu lilikuwa ni kuomba maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wakiwasilisha mawazo na maoni ya wananchi kuhusu maendeleo ya nchi yao na mgawanyo wa rasilimali fedha ili yazingatiwe katika hatua inayofuata ya kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka ujao wa Fedha, mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali nakiri kuwa lengo hili limefanikiwa kwa kiwango cha hali ya juu sana na narudia kusema, ahsanteni sana kwa michango yenu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2020/2021, Waheshimiwa Wabunge wametoa pia pongezi nyingi sana kwa Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kufanikisha

kwa kiwango cha juu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti tangu Serikali yetu ya Awamu ya Tano iingie madarakani Novemba, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo mkunjufu na kwa unyenyekevu mkubwa sana, napenda kupokea pongezi hizi za Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima napenda kuwashukuru kwa moyo wa dhati kabisa Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuamini katika kusimamia majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika pongezi hizi zilizotolewa na Kamati yako ya Mipango ni matokeo ya miongozo na maelekezo yao ambayo wamekuwa wakitupatia kwa lengo la kuliletea Taifa letu maendeleo. Kwa niaba ya Waziri wangu, pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, napenda kuwaahidi kwamba hatutawaangusha, kwani heshima na dhamana mliyotukabidhi kwa niaba ya Watanzania ni kubwa sana na yenye utukufu ndani yake nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuniadini na kunipa jukumu la kutoa ufafanuzi kwa niaba yake, wa hoja za Waheshimiwa Wabunge siku hii ya leo. Nitumie pia fursa hii kuwashukuru kwa dhati watendaji na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bwana Doto Mgosha James, kwa kuchambua na kutafuta takwimu na taarifa zilizohitajika kutolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu kutambua mchango wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi. Kamati ilitupatia ushauri wa msingi na wa mwanzo ambao Waziri wa Fedha na Mipango alieleza kwa ufupi wakati akiwasilisha hoja hii mbele ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, tumepokea mchango uliotolewa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kwa niaba ya msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu hoja iliyombele yetu. Aidha, nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wewe binafsi kwa mchango wako kama Spika na miongozo yako ambayo umetupatia ndani ya kipindi hiki cha siku tano, lakini pia mchango wako kama Mbunge unayewakilisha wananchi wa Jimbo la Kongwa nasema ahsante sana tumepokea mchango wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majadiliano ya hoja iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu, Serikali imepokea maoni mengi sana kwa uchache tumejitahidi kuyachambua na kuyaweka katika makundi yafuatayo:-

(i) Kundi la kwanza ambapo mchango umewekwa nguvu na Waheshimiwa Wabunge ni kuweka msukumo thabiti kwenye sekta ya kilimo, hususan kuwa na uhakika wa upatikanaji wa pembejeo, mbegu na zana bora, huduma za ugani, mikopo na mitaji, miundombinu ya umwagiliaji na utafiti ili kuongeza uzalishaji, tija, ubora na uhakika wa masoko na bei ya masoko ya wakulima wetu; *(Makofi)*

(ii) Eneo la pili ni kwamba Serikali ichukue hatua ya kuboresha uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maji ili thamani halisi ya fedha inayopelekwa kwenye miradi ya maji iweze kuonekana na hatimaye kufikia malengo ya kutatua changamoto ya muda mrefu ya ukosefu wa maji safi na salama kwa wananchi wetu;

(iii) Kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya kimkakati kama vile umeme, reli na barabara ili kuvutia uwekezaji mahiri na hivyo kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii ndani ya Taifa letu;

(iv) Kuwekeza na kutumia kikamilifu rasilimali za bahari na maziwa (*the blue economy*), hususan uvuvi wa bahari kuu;

(v) Kuboresha mazingira ya kufanya biashara ndani ya Taifa letu; na

(vi) Kuimarisha mfumo wa uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali, naahidi kuwa, wakati wa kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021 tutazingatia ipasavyo maoni na ushauri uliotolewa na Bunge lako Tukufu lilipokaa kama Kamati ya Mipango kwa sekta zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kazi ya Wizara yetu ya Fedha katika siku hizi tano ilikuwa ni kupokea maoni na ushauri, ambao sasa tunakwenda kuutafakari kama serikali nzima na kuufanyia kazi hatimaye kuja na mpango wetu wa maendeleo na bajeti kwa mwaka ujao wa fedha naomba nisiseme mengi sana. Hata hivyo, kama ilivyo ada naomba uniruhusu nitoe ufafanuzi kwa baadhi tu ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza na naamini wengi watashangaa nisipoongelea kuhusu Serikali yetu kuwekeza katika kilimo ili sekta ya kilimo ambayo imepewa msukumo mkubwa na hoja ya kwanza ni Serikali iwekeze zaidi katika sekta ya kilimo ikiwezekana kutenga 10% ya bajeti kama Azimio la Maputo na Azimo la Malabo linavyotuelekeza ili kuiwezesha kukua kwa 6% kama Azimio la Malabo pia linavyotuelekeza na hivyo kuchangia kwa kiwango kikubwa kwenye pato la Taifa letu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunafahamu umuhimu wa sekta ya kilimo na mchango wake mkubwa kwenye ukuaji wa uchumi wetu na pato la Taifa. Lakini ni vizuri kama watazania tukafahamu kuwa ili sekta ya kilimo iweze kukua na kutoa mchango mkubwa kwenye pato la Taifa ni muhimu sana serikali yetu kuwekeza kimbakati katika maeneo makuu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni mafunzo, utafiti pamoja na ugavi. Eneo la pili ni usalama wa chakula, uhifadhi na lishe. Eneo la tatu masoko kwa ajili mazao kwenye soko letu la kilimo. Eneo la nne upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu, eneo la tano miundombinu na elimu ya kuongeza thamani ya mazao yetu. Eneo la sita upatikanaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo, na eneo la saba ni kuwa na miundombinu wezeshi kama vile umeme, maji na umwagiliaji, barabara, reli, madaraja, vivuko na meli pamoja na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inatambua sana na imekuwa ikitenda mengi katika maeneo haya na ninaomba niseme machache ambayo Serikali yetu ya Awamu ya Tano imekuwa ikiyatekeleza ili kuhakikisha ukuaji wetu wa sekta ya kilimo unakua kama tulivyosaini maazimio mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza Serikali yetu imeanza utekelezaji wa Programu ya ASDP II ambapo shilingi bilioni 25.19 ambazo ni fedha za ndani na shilingi trilioni 1.37 fedha za nje zimetumika kati ya mwaka wa fedha 2016/2017 na robo ya kwanza ya mwaka 2019/2020 katika kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Serikali imefadhili jumla ya wanafunzi 3,897 kama yalivyo malengo yetu kwenye *program* hii ASDP II katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ili kuhakikisha tunakuwa na maafisa ugani wa kutosha;

(ii) Tumewekeza pia kwenye Utafiti ambapo tumefanikiwa jumla ya miche 37,816 ya korosho kuzalishwa

na kusambazwa nchini katika mikoa ile ambayo ina *potential* kubwa ya uzalishaji wa korosho. Lakini pia mbegu bora 14 zimegunduliwa na TARI na aina 11 ya mbegu mpya za mpunga zimegunduliwa na kutambulishwa katika skimu 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema akiba ya chakula ni jambo la muhimu sana taifa letu limeona na sisi ni mashahidi tunaona Taifa letu limekuwa na akiba ya chakula ya kutosha kwa sababu ya uwekezaji ambayo serikali ina wekeza. Tumeweza kufikia tani 68,124.69 na ukarabati wa maghala 105 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 31,500 umekamilika ili kuhakikisha chakula chetu kinakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumefanyika ukarabati na ujenzi wa skimu za umwagiliaji. Ambapo skimu 5 zimekamilika ikiwa ni pamoja na barabara za kuingia na kutoka zenye urefu wa kilomita 15 na mafunzo kwa wajumbe 311 wa umoja wa umwagiliaji katika Wilaya za Mvomero, Kilosa na Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina niwaombe Waheshimiwa Wabunge wa utekelezaji wa *ASDP II* yanapatikana katika ukurasa wa 65 - 66 wa Mapendekezo ya Mpango wa 2020/2021 na ukurasa wa 259 – 277 wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi robo ya kwanza ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu haikuishia hapo kwenye utekelezaji wa *ASDP II* peke yake, tumekuwa pia na utekelezaji wa mpango wa kuendeleza wa kuendeleza kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa kati ya 2016/2017 na 2019/2020 kwa fedha za ndani ni pamoja na kuendeleza kongano sita zakuongeza tija katika uzalishaji, thamani ya mazao, usambazaji wa mbolea, masoko na watoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hekta 38,477 za mazao zimelimwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Tumeendelea kutenda mambo mengi ambapo pia tumeweza kufufua vinu vya kusaga nafaka *NMC* Dodoma na Mwanza. Ambapo kwa kinu cha Dodoma kimekamilika na kinu cha Mwanza kimefikia 80% ili kuhakikisha sasa tunaweza kuongeza thamani ya mazao ya wakulima wetu na tumetumia shilingi bilioni 15.53 katika kufufua vinu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu pia imetoa jumla ya shilingi bilioni 9.92 kwa ajili ya kufufua kiwanda cha Ngozi Karanga – Moshi. Kazi ya kutengeneza na kusimika mashine inaendelea hii yote ni katika kuhakikisha mipango yetu ya kuinua kilimo chetu mazao yetu ya kilimo inafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu pia imetekeleza programu ya uendelezaji wa mifumo ya masoko na Huduma za Fedha Vijijini ambapo tumetumia shilingi bilioni 114.28 fedha za nje zimetumika kuboresha miundombinu ya masoko vijijini, kuwajengea uwezo wakulima wapato 83,988 katika vikundi 2,408, taasisi 10 za fedha na vyama vya ushirika vya akiba na mikopo 720 pia vimefikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kulieleza Bunge lako Tukufu yameelezwa mengi kwamba Serikali yetu haitoi kipaumbele kwenye kilimo chetu haya nayaeleza na yameandikwa kwenye *document* ambazo tayari tunazo tuweze kuzipitia ili tuwafikishie wataanzania ujumbe kwamba nini kinafanyika na Serikali yetu ya Awamu wa Tano kuhakikisha kilimo chetu kinakuwa imara na kinatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii iliunganishwa na ukuaji wa sekta hii ya kilimo. Lakini Waheshimiwa Wabunge naomba kwa unyenyekevu mkubwa tupitie vitabu yetu. Kitabu chetu cha Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2017, ukurasa 20. lakini pia taarifa ya hali ya uchumi kwa mwaka 2018 ukurasa 20 pia utaona kwamba, sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 5.6 kati ya mwaka 2014 hadi mwaka 2018 tofauti na ambavyo Waheshimiwa wabunge wengi wamesema sekta hii imekuwa kwa chini ya asilimia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango hiki kinakaribiana na lengo la Malabo ambapo nilisema tulisaini azimio hili la Malabo la kuhakiksha sekta yetu ya kilimo inakuwa kwa angalau la asilimia 6 sisi tupo asilimia 5.6 na taarifa zetu mbalimbali tunazosisambasa na ambazo watanzania wanatakiwa kufikishishwa na kuzisoma zinaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jitihada nilizoieleza tunaendelea kupiga hatua katika nyanja ya uwekezaji, kaika sekta ya kilimo na sekta wezeshi, hususan katika Awamu ya Tano ya uongozi wa Jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Hivyo basi, ni matarajio yetu kuwa, tutavuka lengo hili la Malabo la asilimia sita ndani ya muda mfupi ujao tunachohitajika ni kuisapoti serikali yetu kuongea na watanzania kuongea na wakulima na wafugaji wetu ili wazione fursa zinaletwa mbele yao na serikali yao tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye hoja namba mbili, hoja na mbili ambayo ningependa kuitolea maelezo kidogo ni ile ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi pia wamesema Serikali iangalie uwezekano wa kukopa kupitia *export credit* ili kukamilisha Mradi wa Reli ya Kisasa kwa pamoja badala ya kujenga kidogo kidogo ili kuona matokeo chanya na yenye tija ya uwekezaji huu. Hoja hii ni muhimu sana na kama Serikali tunaipokea lakini lazima tufahamu dhamira njema ya Serikali yetu ya Awamu ya Tano ya kutekeleza mradi huu wa Reli yetu ya Kisasa kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu Awamu ya kwanza ya ujenzi inafanyika kwa kutumia mapato ya ndani na Awamu ya pili inagharimia kwa fedha za mkopo utakaopatikana kwa utaratibu wa *Export Credit Agency* ambao masharti yake ni nafuu tofauti na ilivyodaiwa na Waheshimiwa wabunge kwamba tunakopa kwa masharti ya kibiashara hapana tunakopa mikopo naafuu ili tuweze kutekeleza mradi wetu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa kutekeleza mradi huu kwa awamu unatokana na tathmini ya kitaalam iliyofanyika kuhusu upatikanaji na gharama za mikopo, uwezo wa Serikali wa kuhudumia deni bila kuathiri utekelezaji wa bajeti ya maeneo ya kipaumbele pamoja na uhimilivu wa deni la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakisisitiza sana kuhusu uhimilivu wa deni la Serikali na katika hili naomba niliombe Bunge lako Tukufu lifahamu kwamba kwa mujibu wa sheria ya mikopo, dhamana na misaada sura 134, tunatakiwa kukopa kwa kuzingatia tathimini ya uhimilivu wa deni yaani *debt sustainability analysis* na ukomo wa kawaida ni kati ya dola za kimarekani milioni 800 hadi dola Kimarekani 1,000 kwa mwaka. Hivyo basi, uamuzi wa kukopa fedha za mradi mzima kwa wakati moja tutakwenda kuvunja sheria tuliyoitunga wenyewe lakini pia tutakwenda kupata usumbufu kwenye kuli-*manage* deni letu la Taifa. Naomba tuendeleo kuiamini serikali yetu dhamira yake ni njema katika kuhakikisha mradi wetu unakamilika kwa wakati lakini utekelezwe kwa awamu kama ambavyo Bunge lako tukufu limeletewa mbele yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu ambayo ningependa kuisemea kwa ufupi ni hoja iliyosemwa kwamba utekelezaji wa miradi mikubwa mitatu ya kimkakati ambayo ni mradi wa wa reli ya *standard gauge*, kufua Umeme katika Mto Rufiji na ununuzi wa Ndege za Serikali imechukua shilingi trilioni 4.42 ambayo ni sawa na asilimia 36 ya fedha zote za miradi ya maendeleo. Lakini hoja hii ikasemwa zaidi kwamba miradi hii haina faida za moja kwa moja katika uchumi wa nchi yetu. Hii inatokana na ukweli kwamba malighafi inayotumika kujenga reli yetu ya kisasa ambayo ni chuma na *cement* karibu zote zinatoka nje ya nchi na hivyo fedha zinaondoka katika mzunguko wa ndani na kupelekwa nje kwa ajili ya ununuzi wa malighafi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa watanzania wafahamu ukweli kuhusu miradi hii na faida ambayo

inapatikana wakati wa utekelezaji wa miradi hii na baada ya kukamilika kwa miradi hii. Ni vizuri watanzania wasipotoshwe ukiaacha faida za moja kwa moja kwenye uchumi wetu zitakazopatikana baada ya miradi hii kukamilika, zipo faida ambazo zimeshaonekana tayari kwenye Taifa letu tangu kuanza kwa utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache na ufupi, naomba niseme kwa kila mradi nini Taifa letu limepata? Nianze na mradi wa reli yetu ya kisasa (*Standard Gauge Railway*). Hadi Septemba, 2019 Serikali yetu tunafahamu kwenye mradi huu imetoa shilingi trilioni 2.52 lakini mradi huu umezalisha ajira kwa Watanzania takribani 13,117. Hawa ni Watanzania ambao hawakuwa na ajira. Wamepata ajira kwenye mradi huu na wanaendelea kulipwa kutokana na utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu pia umefungua fursa kwa Wakandarasi na Wazabuni wa ndani zaidi ya 640. Hawa walikuwa hawana kazi. Kupitia mradi huu Wakandarasi hawa wamepata kazi kupitia mradi huu na fedha wanazolipwa zinabaki ndani ya Taifa letu tofauti na ambavyo imesemwa fedha nyingi inaondoka kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni za Wakandarasi hawa 640 zina thamani ya shilingi bilioni 664.7. Tunaweza kuangalia kwa asilimia, ni kiwango kikubwa cha pesa kinachobaki ndani ya Taifa letu kutokana na utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mradi huu pia unakadiriwa kutumia *cement* mifuko milioni tisa na nondo za madaraja kilogramu milioni 115 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Makutupora tu. Malighafi hizi zinatoka ndani ya Taifa letu. Hakuna *cement* inayonunuliwa nje ya nchi kuja kutekeleza mradi huu. Kwa hiyo, viwanda vyetu vinaendelea kuzalisha *cement* kwa kiwango kikubwa

katika utekelezaji na fedha hizi zinaendelea kubaki ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mradi huu utaendelea kutekelezwa kwa kuzingatia masharti ya mkataba ambapo asilimia 30 ya gharama za mradi itatumika katika ununuzi wa huduma na bidhaa kutoka nchini. Kwa hiyo, Serikali yetu chini ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, iko makini katika kila mradi unaotekelezwa kuhakikisha Taifa letu linafaidika na utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa mradi huu, tunafahamu ni mengi tutafaidika nayo, lakini dogo tu ambalo Taifa hili limekuwa likiumia kwa muda mrefu ni gharama za matengenezo ya barabara zetu, tutaokoa takribani kwa mwaka mmoja zaidi ya shilingi bilioni 6.7. Ndiyo dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano, ndiyo dhamira ya Chama cha Mapinduzi, ndiyo dhamira ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuhakikisha kuwa mradi huu unatekelezwa kwa wakati, fedha zake zinatafutwa kwa wakati na ndiyo maana tulijibana na kuhakikisha awamu ya kwanza ya mradi huu inatekelezwa na fedha za Watanzania wenyewe, fedha za walipakodi wa Tanzania wenyewe. Nawashukuru sana Watanzania kwa kuendelea kulipa kodi kwa hiari, kwa kuendelea kujitolea kusimamia miradi yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye mradi wa pili ambao nao tumeambia kwamba fedha zote zinaondoka hazibaki nchini. Ni mradi wa uzalishaji wa umeme kwa nguvu za maji wa Julius Nyerere. Mradi huu hadi Oktoba, 2019, nao pia umetusaidia kuzalisha ajira za Watanzania ambao walikuwa hawana ajira zaidi ya 1,456. Mradi huu pia umeongeza fursa kwa Wakandarasi wa Kampuni zetu za ndani. Kampuni 10 za Kitanzania hadi Oktoba 2019, zimepata kazi kwenye mradi huu wa uzalishaji umeme kwa nguvu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mradi huu tumeona kuna ongezeko la ununuzi wa bidhaa za ndani, mfano,

*cement*, nondo, kokoto, mchanga pamoja na vyakula vya aina mbalimbali ambavyo vinatusaidia kuchochea ukuaji wa sekta yetu ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, Tanzania tunayoiondea na Tanzania tuliyopo ni Tanzania ya viwanda. Hakuna Tanzania ya viwanda bila ya kuwa na umeme wa uhakika, hakuna Tanzania ya viwanda bila ya kuwa na umeme wa bei nafuu. Tunatarajia tutakapokamilisha mradi huu, bei ya umeme itashuka na kwa uhakika tutaweza kuiona Tanzania ya Viwanda ambayo Watanzania wameisubiri kwa muda mrefu. Nitoe tu rai yangu kwa Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo ku-*support* miradi hii kwa dhamira njema kabisa ili kuwapa fursa Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa Shirika la Ndege; mradi huu pia umesaidia sana katika kuzalisha ajira za Watanzania zaidi ya 436 hadi kufikia Septemba 2019. Mradi huu pia umerahisisha huduma ya usafiri ambapo njia 11 za ndani ya nchi; na sita nje ya nchi zimeanzishwa hadi kufikia mwezi Oktoba, 2019. Tunaona mapato yetu yakiongezeka tukiweza kukusanya kutokana na utekelezaji wa uboreshaji huu wa Shirika letu la Ndege, lakini pia kuongezeka kwa idadi ya watalii ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilikuwa no hoja ya pili ambayo ningependa kuitolea maelezo kidogo ili tuondoke tukiwa na ufahamu. Yote ambayo yamependekezwa na Kamati yako ya Mipango juu ya miradi hii tutakwenda kuitekeleza tunapoanza kuandaa Mpango wetu wa Maendeleo wa Mwaka 2020/2021 lakini tukizingatia pia hatuvunji sheria tunapotekeleza miradi yetu hii ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya nne ambayo ningependa kuisemea kidogo ni fedha za kutosha kwa ajili ya *TARURA*. Hili limesemwa karibu na Wabunge wote ndani ya Kamati yako ya Mipango.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inatambua sana umuhimu wa kuboresha barabara za mijini na vijijini ili kuboresha huduma ya usafiri na usafirishaji hususan katika maeneo ya vijijini. Katika kutekeleza azma hii, Serikali yetu imeongeza bajeti ya *TARURA* kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kutoka shilingi bilioni 272.6 mwaka 2018/2019 hadi Shilingi bilioni 285.2 mwaka 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 12.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inafanya mapitio ya mtandao wa barabara nchini ili kubaini mtandao wa barabara za *TANROADS* na zile za *TARURA* na hatimaye kufanya maamuzi juu ya mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara. Tunatambua uhitaji huu na tunakwenda kushughulika nalo tunapokwenda kuanda Mpango wetu wa Maendeleo wa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tano ambayo ningependa pia kuitolea maelezo kidogo ni hoja ambayo pia imesemwa na angalau na Wabunge zaidi ya asilimia 80, nayo ni kuhusu utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kwa njia ya ubia kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ina dhamira njema sana ya kuona Sekta Binafsi inashiriki katika utekelezaji wa miradi yetu mikubwa ya maendeleo na ndiyo maana tulileta sheria hapa, tukafanya marekebisho ya Sheria yetu ya Ubia, Sura 103 na kwa mujibu wa Kanuni ya 29(1) ya Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kama ilivyorekebishwa mwaka 2018 kwa dhamira njema kabisa, miradi yote inayoibuliwa inatakiwa kutangazwa inapofikia hatua ya ununuzi kwa kumpata mbia wa kuwekeza. Kanuni hii imeainisha kuwa miradi hiyo itatangazwa katika vyombo mbalimbali vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpendekezo ya Mpango wetu wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021 ukurasa wa 74, tumeainishwa jumla ya miradi nane ya ubia. Kati ya miradi hiyo ambayo inatarajiwa kutangazwa

kwa mwaka 2019/2020 na utekelezaji wake kuanza 2020/2021:-

(i) Mradi wa uendeshaji wa huduma ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka Jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza;

(ii) Mradi wa Kuzalisha Dawa za Binadamu (*General Pharmaceuticals*), kiwanda tunachotarajia kitajengwa Pwani;

(iii) Mradi wa Kuzalisha Bidhaa za Pamba za Hospitali (*Medical Cotton Products*) ambacho kinatarajiwa kujengwa Mwanza; na

(iv) Mradi wa Kuzalisha Maji Tiba (*IV fluids*) kinachotarajiwa kujengwa kule Jijini Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushahidi huu, siyo kweli kwamba Serikali haitaki kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mfumo wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Serikali ipo tayari kwa kuanza na miradi hii huku tukiendelea kuandaa miradi mingine kama sheria inavyotuelekeza. Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla kwamba, yeyote mwenye Mwekezaji mwenye dhamira njema wawalete wawekezaji hao na Serikali yetu ipo tayari kufanyanao kazi kwa mujibu wa Sheria na kanuni zilizopo na kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Tuko tayari kabisa, tuaomba mtuletee wawekezaji na tutafanyanao kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya sita ambayo pia napenda kuitolea maelezo kidogo, ambayo nayo karibu asilimia 98 ya Waheshimiwa Wabunge wameigusia ni hoja ya mapendekezo kwamba Mpango huu tunaoupendekeza unakuja na mkakati gani wa kutatua tatizo la maji ifikapo mwaka 2020/2021?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wetu huu yanalenga kutatua changamoto ya upatikanaji

wa maji safi na salama, kusimamia vyanzo vya maji, kudhibiti matumizi ya fedha za maji, ikiwa ni pamoja na ubora wa miradi ya maji. Aidha, Mapendekezo ya Mpango wetu yanalenga pia kuongeza kiwango cha upatikanaji maji mijini na vijijini kutoka hali ya sasa ambapo Jiji la Dar es Salaam limefikia asilimia 85, mikoa mingine asilimia 80, Miji Midogo ni asilimia 64 na vijijini ni asilimia 64.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji pamoja na ubora wa miradi ya maji, Mpango tunaoupendekeza mbele ya Bunge lako Tukufu umeainisha kufanya yafuatayo ambapo kama Serikali tumekuwa tukiyarudiarudia na tunakwenda kuyasimamia:-

(i) Tunakwenda kuendelea na usimamizi wa matumizi endelevu ya maji;

(ii) Kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini katika miradi ya maji nchi nzima;

(iii) Kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji vijijini na mijini kwa kukamilisha miradi inayoendelea na kuanza miradi mipya ambayo itapendekezwa ndani ya Mpango tunaokuja nao; na

(iv) Tunakwenda kuimarisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira vijijini, yaani *RUWASA* pamoja na shughuli za mfuko wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote tumeyaeleza katika mapendekezo ya Mpango na tunapokwenda sasa kuandaa Mpango wetu, tunakwenda kuainisha kazi zote zinazokwenda kutekelezwa ndani ya mwaka ujao wa fedha ili kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ningependa kuisemea kidogo ni ile ambayo Waheshimiwa Wabunge pia wameiongelea na kuomba Serikali ifanye marejeo ya vipaumbele vya Kitaifa hususan kwa kuzingatia

Sekta ya Maji, Sekta ya Afya na miundombinu ya barabara hasa barabara za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji, afya na miundombinu kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wetu wamependekeza ni miongoni mwa vipaumbele vya awali kabisa vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yaani Mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 na Serikali yetu imekuwa ikiwezekeza fedha nyingi kwenye sekta hizi. Maeneo hayo kama ilivyopendekesha na Waheshimiwa Wabunge yataendelea kuwa ya kipaumbele kwa Taifa kutokana na umuhimu wake katika kuboresha maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, maeneo hayo yameainishwa vizuri kabisa pia katika kitabu cha Mapendekazo ya Mpango tunaokwenda kujanao ukurasa wa 69. Kinachokosekana ni kazi zinazokwenda kufanyika ambazo zitakwenda kuainishwa baada ya kuwa tayari tumeshapokea maoni na ushauri wa Kamati yako ya Mipango tunapokwenda kuandaa Mpango wetu wa Maendeleo wa Mwaka 2020/2021, tutauleta mwezi wa Tatu kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameisema kwa nguvu ni ukamilishaji wa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi; maboma katika Sekta ya Elimu na Sekta ya Afya. Serikali yetu inatambua nguvu za wananchi zilizowekezwa katika ujenzi wa maboma haya na ndiyo maana kila mwaka tunatenga bajeti na kuitekeleza kwa asilimia kubwa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma yaliyojengwa na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kati ya Julai, 2018 na Oktoba, 2019, Serikali yetu imetoa jumla ya shilingi bilioni 104 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma ya huduma za jamii katika Sekta ya elimu na Afya. Kati ya fedha hizi, shilingi bilioni 38.9 zilitolewa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma 96 ya Vituo vya Afya na shilingi bilioni

29.9 zilitolewa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma ya madarasa 2,392 ya shule zetu za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Serikali kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo, katika Sekta ya Elimu ilitoa shilingi bilioni 35.2 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa 2,760 na matundu ya vyoo 670 kwenye shule zetu za msingi. Tunaendelea kutekeleza bajeti hii kwa mwaka huu wa 2019/2020 ili kuhakikisha maboma yote yanafunikwa na wananchi wetu wanaanza kupata huduma kwenye maeneo haya ambapo waliweka nguvu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo napenda kuisemea kwa ufupi sana ni hoja ambayo karibu asilimia 100 ya Waheshimiwa Wabunge wa upande wa Upinzani walisema kuhusu fedha za miradi ya maendeleo katika Sekta ya Kilimo ambazo zimetolewa kwa asilimia mbili na asilimia 98 hazikuweza kutolewa. Hili naomba nilisemee ili Watanzania waelewe uhalisia, nini Serikali yao inafanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema wakati najibu hoja ya kwanza kabisa kazi nyingi ambazo zimefanyika katika Sekta ya Kilimo; ni vizuri tukatambua kwamba, bajeti ya Sekta ya Kilimo inajumuisha fedha zinazotengwa kwenye Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Fungu 64 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Fungu 99 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi, upande wa Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bajeti ya mwaka 2018/2019, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo ilikuwa shilingi bilioni 108.4 na kiasi kilichotolewa siyo shilingi bilioni mbili kama ilivyosemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wa upande wa Upinzani. Kiasi kilichotolewa ni shilingi bilioni 66.2 ambayo ni sawa na zaidi ya asilimia 61 ya fedha yote ambayo ilitengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kusisitiza kwamba ni muhimu tukawa na takwimu sahihi ili tunaposimama kwenye Bunge lako Tukufu tuweze

kuwaleleza Watanzania dhamira njema ya Serikali yao ya kuweza kukiinua kilimo chetu ili kiendelee kuchangia katika ukuaji wa pato letu la Taifa. Tunatambua sana umuhimu wa Sekta ya Kilimo na kama Serikali tutaendelea kuweka nguvu yetu kubwa huko.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kengele imegonga lakini niseme pia hoja ya mwisho ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamesema ni vizuri tukafanya tathmini, yaani tufanye tathmini tunapokwenda kukamilisha utekelezaji wa Mpango wetu wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Tayari Serikali yetu imeanza zoezi hili la kufanya tathmini ya utekelezaji ya Mpango wetu wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wakati tunaanza kuandaa Mpango wetu wa Tatu wa Maendeleo katika utekelezaji wa Dira yetu ya Taifa mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna tunaloligopa kwa sababu tunajua tumetekeleza mengi katika sekta zote na tuko tayari kama Taifa kuwaeleza Watanzania, dhamira yetu ilikuwa ni kuiondoa Tanzania kutoka kwenye Taifa la kipato cha chini kwenda kwenye Taifa la kipato cha kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Watanzania wakajua kwamba katika taarifa iliyotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika Juni, 2019 inaainisha nchi nne ambazo zimechangia kukua kwa uchumi wa Bara la Afrika. Naomba nizataje hizo nchi nne mbele ya Bunge lako Tukufu. Nchi ya kwanza ni Djibouti, nchi ya pili ni Ethiopia, nchi ya tatu ni ya Rwanda na ya nne ni taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetenda mengi makubwa, wananchi wanajua, Watanzania wanaelewa na walioko nje ya taifa letu wanaona mengi makubwa yanayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano, na

tumekuwa ndani ya nchi nne zilizochangia ukuaji wa asilimia 6.5 wa Pato la Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miradi mikubwa tunayotekeleza naomba niwaambie Watanzania wasiwe na wasiwasi, tumejipanga tunaweza kukusanya mapato yetu wenyewe, tu natekeleza miradi mingi. Miradi ya afya tunatekeleza; zaidi ya hospitali 67 tumejenga, hii ni kwa ajili ya wananchi wenyewe. Zaidi ya vituo vya afya 352 tumevijenga. Mwaka huu tunakwenda kujenga zaidi ya hospitali nyingine 19 za halmashauri zetu. Hii yote ni kuwafikia Watanzania, ni kuhakikisha kwamba Watanzania wanafikiwa na maendeleo kama ambavyo sisi viongozi wao na viongozi wetu wa kitaifa wanavyotuelekeza kuyatenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na jambo moja ambalo tumekuwa tukilisisitiza kwa muda mrefu lakini linarudiwa rudiwa sana kutamkwa katika Bunge lako tukufu. Hoja yenyewe ni pale ambapo Kambi Rasmi...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja.

**MWENYEKITI:** Malizia tu Mheshimiwa, nakuongezea dakika tano.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni pale ambapo Kambi Rasmi ya Upinzani inaposema Seriakli yetu inavunja Katiba kwa kutokuleta sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango. Leo nimeongea taratibu sana na nimekuwa mpole sana ili niweze kueleweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba niseme, Serikali yetu imekuwa ikiheshimu Ibara inayotajwa na Kambi Rasmi ya Upinzani, Ibara ya 63 (3) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 iliyoweka sharti

ya kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa kufanya yafuatayo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, tunalishukuru Bunge lako Tukufu, mwaka 2015 Bunge letu lillipitisha Sheria ya Bajeti Sura 439 ambayo inasimamia uandaaji, uidhinishaji, utekelezaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, hiyo ni sheria ya kwanza inayosimamia utekelezaji wa Mipango ya muda mrefu na Mipango ya muda mfupi inayopangwa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kila mwaka Serikali yetu huwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Fedha unaobainisha vyanzo mbalimbali vya mapato vitakavyotumika kugharamia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka husika. Naomba tutambue mpango wa maendeleo unatafsiriwa kwenye bajeti ya mwaka husika. Kwahiyo sheria zinazoletwa kwenye kutekeleza bajeti ya mwaka husika ndiyo sheria zinazosimamia utekelezaji wa mpango ule wa mwaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kila mwaka Serikali yetu bila kukaidi tumekuwa tukiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa Mwaka Unaofuata kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Kwahiyo naomba niseme nikisimama kwa nguvu zote kifua mbele kwamba hatujavunja Katiba wala sheria yoyote ndani ya nchi yetu kwa sababu tunasema yale yote tuliyoelekezwa na taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwa Waheshimiwa Wabunge waliotueleza kwamba mpango wetu mapendekezo haya hayakuainisha *deliverables* au *outcomes*. Haya ni mapendekezo, tumechukua maoni, tunakwenda kuyafanyia kazi, tutakapokuja na Mpango wetu tutaieleza. Nitoe mfano ambao ulitolewa wakati wa kuchangia kwamba Sekta ya kilimo na likatajwa zao la



pamba kwamba hatuna *deliverables* kama Serikali yaani tunakwenda tu hatujui tunaelekea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua Mpango wa Maendeleo wa mwaka huu tunaoutekeleza ukienda ukurasa wa 86 kwenye kilimo cha kahawa na pamba imeainishwa wazi wazi wapi tupo na wapi tunaelekea. Kwahiyo naomba niseme tumejipanga vizuri, Serikali ya Awamu ya Tano inaongozwa kiuadilifu kabisa na tunaandaa mipango yetu inayotakiwa kwa ajili ya utekelzaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe tena kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021. Aidha nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wetu tuisite kuendelea kutoa maoni na ushauri wa kuboresha Mpango wetu huu kwani sasa kazi ndiyo imeanza; tunaenda kutekeleza yale yote ambayo mmetuelekeza. Siku zote kama Wizara/ Serikali tunathamini sana maoni, ushauri na mapendekezo yenu. Tuko tayari kuyapokea muda wowote. Kama nilivyoainisha hapo awali, Serikali itazingatia maoni na ushauri wenu wote lakini bila kuvunja sheria na kanuni za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika dhamira yake ya kujenga Tanzania mpya, Tanzania ya kipato cha Kati, Tanzania ya viwanda. Yanawezekana, tumeanza kuyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuwahimiza wananchi wetu kushiriki katika shughuli za maendeleo ili kujiletea mabadiliko chanya katika maisha yao na Taifa letu kwa ujumla lakini bila kusahau

kwamba hakuna taifa ambalo liliwahi kuwa huru bila kuwa na mapato yake imara ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Watanzania wanaponunua waombe risiti na wale wanaouza waweze kutoa risiti ili tuendeleo kukusanya mapato ya Taifa letu. Aidha, mwisho kabisa natoa wito kwa Watanzania wote kushiriki kwa amani na salama kabisa katika uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa tarehe 24, Novemba 2019 kwani uchaguzi wa Serikali za Mitaa ndio msingi imara wa uchaguzi Mkuu ujao mwaka 2020 japo umeshaonesha kuna *green light* kwa chama kile kile cha kijani kuendelea kufanya vizuri. Tuendeleo kusimama imara tunakwenda kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya naomba nikushukuru tena na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha Dkt. Ashatu Kijaji kwa kupokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge na kuahidi kwamba mnaenda kuyazingatia katika kuja na Mpango hapo baadaye. Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote hawa, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Serikali kwa ujumla wake na hasa Mheshimiwa Waziri Mpango ambaye hapa mwishoni

hatujaweza kuwa nae kwa sababu kulikuwa na jukumu maalum kabisa la kuitumikia nchi yetu kwa hiyo alilazimika kwenye Afrika Kusini. Sasa yeye pamoja na Naibu wake Dkt. Ashatu Kijaji tunawashukuru sana kwa uvumilivu wao pamoja na wasaidizi wao tulipokuwa kwenye Kamati ya Mipango jinsi ambavyo wamepokea maoni yetu yote. Yale yaliyoongewa kwa ukali, kwa kawaida na mengine yote yanayowahusu na yasiyowahusu n.k lakini kwa uvumilivu mkubwa mmeyapokea, mmeyachuja. Kwa hiyo kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge, tunawashukuruni sana.

Jukumu hili la kujadili huu Mpango ni jukumu la kikatiba; tunafanya hivi kwa niaba ya wananchi kuisaidia nchi yetu kuelekea katika uelekeo ambao unatakiwa; kwa sababu bila Mipango maana yake ni kwamba utakuwa hujui unaelekea wapi. Hata mwananchi mmoja mmoja kwenye familia lazima awe na mpango. Usipokuwa na mpango watu wakakuuliza una mpango gani ukasema sina mpango maana yake ni kwamba bado una tatizo kubwa sana.

Kwahiyo tunashukuru tuko na Mpango wetu wa miaka mitano, tumeutekeleza mwaka hadi mwaka sasa tunaelekea kuwa na Mpango wa mwaka wa mwisho katika utekelezaji huo. Kwa kweli kama mlivyochangia wenyewe, utekelezaji umekuwa mzuri mno, Serikali hii ya Awamu ya Tano imejitahidi kiasi kwamba nchi nzima wananchi wana furaha kubwa na hawaamini macho yao. Wanachotuong'aa ni kwam ba tuendelee sasa na kuwa na mipango bora zaidi na utekelezaji zaidi na zaidi kwasababu tatizo letu kubwa toka nyuma halikuwa mipango. Tatizo letu kubwa lilikuwa mipango yetu mizuri haitekelezwi. Sasa *this time* mipango imekuwa ikitekelezwa, tukipanga kununua ndege, ndege zinateremka kweli na mimi Spika nawaalika na Wabunge tunapokea ndege. Tumepanga kujenga reli *SGR* kweli reli inajengwa usiku na mchana. (*Makofi*)

Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge mmekwenda mmeshuhudia kweli reli inajengwa, tumepanga kujenga

*Stieglers' Gorge* au Bwawa la Mwalimu Nyerere kweli linajengwa usiku na mchana. Kila tulichokipanga, tumepanga wanafunzi wetu wa Vyuo Vikuu tutawapa mabilioni kadhaa, wanakopeshwa.

Tumepanga kupeleka fedha kwenye wilaya kwenye shule, fedha zinakwenda. Tumepanga kuhusu huduma za afya, amesimama Mheshimiwa Kadutu hapa anatupa matumaini anasema jamani Muhimbili sasa hivi ni hospitali. Nani hajui ilikuwa imeonza kabisa. Muhimbili ilikuwa ni pipa lenye matobo hata ujaze maji kiasi gani, halijai. Lakini leo si Muhimbili peke yake; hata mnaotoka kwenye hospitali za Wilaya, kwenye vituo vya afya, kwenye zahanati wanakwambia dawa zinapatikana. Ni hadithi ambayo usingeweza kuiamini, kupatikana kwa dawa kwenye zahanati, kituo cha afya? Hizi ni hatua kubwa sana.

Kwa hiyo, lazima tuwape moyo wenzetu ambao usiku na mchana hawalali kuanzia Mheshimiwa Rais mwenyewe Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, tunawapigia *salute*, mnaofanya kazi sana. Hivi tangu nchi hii ipate uhuru lini mmeona Mawaziri waliosafiri kilometa kwa kilometa ndani na nchi kama hawa? Tuseme tu ule ukweli jamani. Wamepiga masafa hawa watu wa watu, wapi hawajafika? Kabisa, anaingia huyu anatoka huyu, mara wamekuja wawili kwa mpigo, yaani ni hivi! Wamejitahidi jamani, wamejitahidi sana; na ndiyo maana Rais anapotuambia tutembe kifua mbele, tunatembea kifua mbele kweli. Ndiyo maana tunasema huu uchaguzi wa Serikali za mitaa shughuli! Kwa sababu kazi imefanyika sana.

Sasa huu wa mwakani ndiyo kabisaaaa! Yaani kabisaaa! Ndiyo maana tunazungumzia habari ya mipango. Rafiki zangu na nyie anzeni kupanga sasa kurudi CCM ili mambo yawe, si unapanga? Lazima upange. Lazima uangalie tupange, maana yake unaangalia na upepo wenyewe na halisi na nini, unapanga. (*Makofi/Vigelegele/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, basi baada ya kusema maneno haya ya kuhitimisha mambo haya. Tunaendelea na ratiba yetu, mnayo kwenye *tablets* zenu, ratiba yetu iko vile vile. Tunaendelea na Sheria yetu ile Kamati ya Katiba na Sheria walikwishamaliza kazi yao kwa hiyo kesho tunaendelea kama kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo basi naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 01:35 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 12 Novemba, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*